# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 6 Mei, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tisa, leo ni Kikao cha 23, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI -KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mmabo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Ahsante sana. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI -KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya Mtandao)*

Na. 212

### Kuwatambua Watu Wenye Ulemavu Nchini

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata mahitaji ya msingi sawa na watu wasio na ulemavu.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwatambua watu wote wenye ulemavu?

(b) Je, Serikali inatumia njia zipi katika kuhakikisha mahitaji ya msingi yanawafikia watu wenye ulemavu popote walipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia zoezi la sensa ya watu na makazi hutambua wananchi wake wote wakiwemo watu wenye ulemavu. Utambuzi huu hujikita katika kupata takwimu zao, mahali wanapoishi/kupatikana, umri, jinsi, aina za ulemavu na hali halisi ya maisha yao. Kwa mfano, kwenye eneo la takwimu nchini Tanzania, Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inaonesha kuwa Tanzania ilikuwa na jumla ya watu 44,928,923 na kati ya hao, watu wenye ulemavu walikuwa 2,641,802 sawa na asilimia 5.8 ya wananchi wote.

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikitumia njia mbalimbali katika kuhakikisha mahitaji ya msingi ya watu wenye ulemavu yanawafikia popote walipo kama ifuatavyo:-

(i)Kutengeneza na kutekeleza sera, miongozo, sheria na mikakati mbalimbali shirikishi katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma zilizo bora kwa watu wote wenye ulemavu mahali popote walipo.

(ii)Uanzishwaji na uendeshaji wa taasisi mbalimbali za kisheria za watu wenye ulemavu ikiwemo Baraza la Ushauri la Taifa la Watu wenye Ulemavu linaloishauri Serikali juu ya namna bora ya usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu kupitia Sheria Na.9 ya mwaka 2010.

(iii)Kuhuishwa kwa masuala ya watu wenye ulemavu na kufanywa kuwa mtambuka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuanzisha madawati 26 katika ngazi ya Wizara na madawati 19 katika taasisi za Serikali kwa ajili ya kuratibu na kusimamia masuala ya watu wenye Ulemavu.

(iv)Uundwaji wa kamati za kuhudumia watu wenye ulemavu ambazo zimeundwa katika mikoa 26, halmashauri 130, vijiji 5034 na mitaa 2284.

(v)Vyuo vya Ufundi.

Na. 213

**Hitaji la Hospitali ya Wilaya ya Uvinza**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA** aliuliza:-

Wilaya ya Uvinza haina Hospitali ya Wilaya na jitihada za makusudi zimefanyika kukarabati majengo yaliyokuwa ya wakimbizi (Rugufu) ili kuanzisha Hospitali ya Wilaya.

Je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya Wilaya ya Uvinza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilimwa, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza kiasi cha Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ambapo mpaka Machi, 2020 ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, maabara, jengo la wagonjwa wa nje, jengo la utawala, stoo ya kutunzia dawa na jengo la kufulia nguo yamekamilika kwa asilimia 98. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 hospitali hiyo imetengewa kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Na. 214

## Hitaji la Umeme wa Dharura Katika Vituo vya Afya

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Serikali imejenga vituo vingi vya afya hususan katika Mikoa ya Simiyu lakini vituo hivi havina umeme wa dharura ili kutumika wakati umeme wa *TANESCO* utakapokatika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka umeme wa dharura katika vituo vya afya ili kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Meshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2017/ 2018 hadi Machi, 2020 Serikali imejenga, kukarabati, kupanua na kuboresha vituo vya afya 433 nchini. Vituo 114 kati ya 433 vina huduma ya majenereta kwa ajili ya umeme wa dharura. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuvipatia vituo vilivyobaki majenereta kwa ajili ya umeme wa dharura.

Na. 215

## Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Same - Mwanga - Korogwe umesimama kutokana na kukwama kwa vifaa vya ujenzi bandarini kwa takribani miezi kumi tangu Januari, 2019 vikidaiwa kodi na Serikali. Aidha, kodi ya vifaa vya ujenzi wa miradi ya maji iliondolewa kisheria.

Je, ni lini sasa vifaa hivyo vitaruhusiwa kutoka bandarini ili mradi huo muhimu kwa wananchi wa Wilaya za Mwanga na Same waweze kunufaika na mradi huo utakapojengwa na kukamilika?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Jimbo la Mwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Same - Mwanga - Korogwe ni miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa na Serikali kwa lengo la kuondoa kero ya maji kwa wakazi wa miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyo katika eneo la mradi vikiwemo vijiji vya Halmashauri ya Korogwe. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali, *BADEA, OFID, Saudi Fund* na *Kuwait Fund* kwa gharama ya dola za Marekani milioni 300. Mradi huo utakapokamilika utazalisha maji lita milioni 103.7 kwa siku dhidi ya mahitaji ya sasa ya lita milioni 78.4 kwa siku na utawanufaisha wananchi wapatao 438,931 katika Wilaya za Same (246,793), Mwanga (177,085) na Korogwe (15,053).

Mheshimiwa Spika, msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwa ajili ya vifaa vya mradi wa Same - Mwanga - Korogwe ulipatikana tarehe 4 Novemba, 2019. Kwa sasa vifaa husika vimetolewa bandarini na vimefika eneo la mradi ili kuendelea na utekelezaji. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 69. Serikali inaendelea kuhakikisha vifaa vyote vinavyohitajika vinapatikana ili kukamilisha mradi huo ifikapo mwezi Septemba, 2020.

Na. 216

**Kuanzisha Mradi Mkubwa wa Maji – Mto Ruvuma**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu wakazi wa Mji wa Nanyamba wanapata shida kubwa ya maji licha ya kuwa jirani na Mto Ruvuma.

Je ni lini Serikali itaanzisha mradi mkubwa wa maji utakaonufaisha wananchi wa Kata ya Kitaya, Kiromba, Chawi na Mtiniko?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo kwenye mpango wa kujenga mradi mkubwa wa maji kutoka kwenye Mto Ruvuma utakaohudumia zaidi ya vijiji 50 vya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba na Wilaya ya Mtwara. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kupitia fedha za mkopo kutoka Benki ya *AfDB* na kwa sasa upo kwenye hatua za awali za maandalizi.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua kero ya maji kwa muda mfupi kwa wananchi waishio katika Mji wa Nanyamba na Kata za Kitaya, Kiromba, Chawi na Mtiniko, Serikali imetekeleza na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji wakati mradi mkubwa unasubiriwa.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Nanyamba ambao una wakazi wapatao 24,021 unapata huduma ya maji kupitia Mradi wa Mnyawi. Katika kuboresha zaidi huduma ya maji, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Nanyamba Mjini wenye thamani ya shilingi 944,196,493.12 ambapo visima virefu viwili tayari vimechimbwa na ujenzi wa mradi huo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, pia katika kuhakikisha huduma inaboreka zaidi mnamo mwezi Januari, 2020 Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara *(MTUWASA)* imepewa jukumu la kusimamia huduma zote za maji katika Mji huo.

Vilevile Serikali kupitia Wakala wa Maji Vijijini *(RUWASA)* ipo kwenye mpango wa kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Kitaya wenye thamani ya shilingi 350,000,000 kupitia programu ya *P for R*. Mradi huo unategemewa kuanza mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Novemba, 2020.

Na. 217

**Kodi Inayotozwa kwa Shirika la Umeme Zanzibar**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

*ZECO* hununua umeme wa jumla kutoka *TANESCO* lakini wanaponunua umeme hutozwa *VAT* na *TRA* na wanapokwenda kuuza Zanzibar hutozwa tena Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na *ZRB* jambo ambalo hupelekea Shirika hilo kuwa na madeni makubwa.

(a) Je, Serikali inalijua hilo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa kero hiyo?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, masuala ya kodi nchini hutozwa na taasisi za kikodi kulingana na sheria za kodi zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar. Pamoja na hali hiyo Serikali imeendelea kutatua changamoto mbalimbali za kikodi katika biashara ya umeme kati ya Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* na Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO).* Kwa vipindi tofauti Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* zimekuwa zikifanya mapitio ya kodi hizo ili kuleta manufaa kwa pande zote mbili za Muungano.

(b) Mheshimiwa Spika, katika hatua ya kupata ufumbuzi wa kudumu katika jambo hilo, Serikali ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania (SMT) ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kodi na Ushuru Mbalimbali ya mwaka 2019/2020 ambapo umeme unaouzwa kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar uliondolewa Kodi ya Ongezeko ya Thamani *(VAT)* na kubaki asilimia sifuri.

Katika hatua nyingine, Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kupitia Wizara ya Nishati na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati zinasimamia kwa karibu majadiliano yanayoendelea kati ya *TANESCO* na *ZECO* kuhusu bei ya kuuziana umeme ambapo *EWURA* na *ZURA* zinashirikishwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa biashara ya umeme kati ya *TANESCO* na *ZECO* inafanyika kwa ufanisi na kuyanufaisha mashirika hayo yote mawili pamoja na wananchi kwa ujumla. Suala hili limefikishwa katika ngazi za watendaji wakuu wa Serikali zote mbili wakiwemo Makatibu Wakuu.

Na. 218

**Kukamilisha Miradi ya Umeme Katika Vijiji vya Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya umeme katika vijiji ambavyo havijafikiwa katika Halmashauri ya Momba?

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Momba ina jumla ya vijiji 72 kati ya vijiji hivyo vijiji 37 vimepatiwa umeme kupitia miradi ya *TANESCO, REA* Awamu ya Pili na katika *REA* Awamu ya Tatu inayoendelea. Vijiji 35 ambavyo havina umeme vitapata umeme kupitia mzunguko wa pili unaotarajia kuanza mwezi Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji 35 vilivyosalia katika Halmashauri ya Momba zitajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 197.6, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 126, pamoja na ufungaji wa transfoma 36 za KVA 50 na 100 na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 1,427. Gharama za mradi ni Shilingi Bilioni 2.65 na utakamilika mwezi Juni, 2021.

Na. 219

**Hitaji la Mahakama ya Wilaya–Kyerwa na Misenyi**

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI** aliuliza:-

Wilaya ya Kyerwa na Misenyi zilizoko katika Mkoa wa Kagera hazina Mahakama ya Wilaya jambo ambalo linawafanya wananchi wa Wilaya hizo kufuata huduma hiyo katika Wilaya za jirani za Karagwe na Bukoba.

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Wilaya hizo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ni moja ya changamoto inayoikabili Mahakama za Tanzania. Mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za mahakama hapa nchini ni makubwa. Kwa msingi huo, mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na mpango wa ujenzi na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya Kyerwa na Misenyi ni miongoni mwa majengo ya Mahakama za Wilaya 33 ambayo yatajumuisha Mahakama za Mwanzo katika jengo moja. Ujenzi wa majengo haya

umepangwa kuanza mwezi Juni na kukamilika mwezi Desemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Kwa sasa mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyo katika mpango wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, tayari Mshauri Elekezi amefanya mapitio ya michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza kama ilivyopangwa. Hivyo ninaendelea kumuomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira ili majengo haya yakamilike ambayo yatatatua changamoto ya wananchi wa Wilaya hizi kufuata huduma za kimahakama katika Wilaya ya Karagwe na Bukoba.

Na. 220

**Ujenzi wa Nyumba za Askari Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Wizara ya Mambo ya Ndani huwa wana mpango wa kujenga nyumba za askari kwenye miji mikubwa tu.

Je, ni lini zitajengwa nyumba za askari Rukwa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio kweli kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani Nchi huwa na mpango wa kujenga nyumba za askari katika miji mikubwa tu. Mpango wa ujenzi huwa ni kwa maeneo yote yenye uhitaji na kuwekwa vipaumbele kulingana na hali ya mahali ilivyo.

Mheshimiwa Spika, ipo Mikoa, Miji, Wilaya, Tarafa, Kata na Vijiji vinavyohitaji vituo vya polisi na nyumba za kuishi askari

na maeneo hayo yanafahamika ikiwa ni pamoja na Rukwa. Hata hivyo Serikali inao mpango wa kujenga nyumba za askari Rukwa kwa awamu kwa kutumia rasilimali watu na fedha ndani ya Wizara yangu.

Na. 221

**Tatizo la Ukatili wa Kijinsia Nchini**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Ukatili wa kijinsia umekuwa ni changamoto kwa sasa nchini. Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hilo?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua vipo vitendo vya kuwanyanyasa, kuwadhalilisha na kuwadhulumu na vinatafsiriwa kama ukatili ambavyo kwa sehemu kubwa huwaathiri zaidi wanawake na watoto katika jamii zetu. Vitendo hivi vikifanyika kwa mrengo wa jinsia tunaviita ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuzuia na kutokomeza ukatili huo. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Kamati za Ulinzi za Wanawake na Watoto 16,343 kwenye ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM). Kamati hizi zinawajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanawake na watoto. Pia madawati ya jinsia na watoto 427 yameanzishwa katika vituo vya polisi. Sheria ya Elimu imefanyiwa marekebisho mwaka 2016 na kuweka adhabu ya kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kumpa mimba, kuoa au kuolewa na mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Aidha, Serikali imetekeleza Sheria ya Elimu Pasipo Malipo kwa

wanafunzi wa shule za sekondari na msingi ili kuwezesha watoto wa kike na wa kiume kupata elimu bila kujali uwezo wa kiuchumi wa familia. Pia Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa imefanyiwa maboresho na kufanya uchangiaji wa asilimia 10 kuwa wa kisheria kwa kuwezesha mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria Na. 1 ya mwaka 2017. Sheria hii inatoa fursa kwa wanawake waliofanyiwa unyanyasaji au kudhulumiwa kupata haki zao kutokana na huduma za msaada wa kisheria kupitia vyombo vya usimamizi wa sheria. Vilevile Serikali imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kutokomeza ukatili wa kijinsia.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI -KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi ana kazi maalum kabisa na kwa jinsi hiyo hotuba yake itawasilisha na *Chief Whip,* Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Mheshimiwa Jenista Mhagama tafadhali karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, naomba sasa kuwasilisha hotuba kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na fadhila kwa kuendelea kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine tena katika ukumbi huu hapa leo kwa kwa shughuli hii muhimu.

Vilevile kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuniteua na kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu katika kipindi cha Awamu ya Tano.

Nawashukuru pia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge hili Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge la Kumi na Moja kwa mafanikio makubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu ili muweze kuendelea kuliongoza Bunge letu.

Kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge) aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya

Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kutupatia ushauri hakika uongozi wake ulikuwa umakini na wenye weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo kwa sasa inaongozwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani (Mbunge) kwa kuchambua na kushauri juu ya kuboresha mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ninayowasilisha leo hapa bungeni. Wakati wote Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama ndani ya nchi yetu. Lakini Wabunge hao wametoa ushirikiano mkubwa sana kwangu nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kumshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ninayoisimamia Dkt. Florens Martin Turuka ambaye amestaafu utumishi wa umma kwa mujibu wa sheria. Kwa niaba ya Wizara tunamshukuru sana kwa kuitumikia Wizara kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Pia nampongeza Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu haya mapya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mwingulu Lameck Nchemba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, lakini vilevile natoa pongezi za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu mpya wa Bohari ya Dawa Brigedia Jenerali Dkt. Gabriel Saul Mhidize na kabla ya uteuzi wake alikuwa Mkuu wa Hospitali ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi Tanzania, Lugalo. Sambamba na pongezi hizo, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao

muhimu ya kuwatumikia wananchi na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,vilevile naomba kumpongeza Kanali Joseph Peter Bakari kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Michezo ya Kijeshi Duniani ndani ya Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani *(International Military Sports Council)*. Namtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimwa Wabunge, familia na wananchi wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu waliokuwa Wabunge kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi katika nyakati tofauti. Mnamo tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako tukufu liliondokewa na Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, tarehe 20 Aprili, 2020 Bunge liliondokewa na Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na tarehe 29 Aprili, 2020 liliondokewa pia na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve. Vilevile, kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu na kwako Mheshimiwa Spika, Wabunge na wananchi kwa kuondokewa na Waziri wa Katiba na Sheria na Mbunge wa Kuteuliwa Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, aliyefariki tarehe 1 Mei, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Maafisa, askari, watumishi wa Umma wote, familia za wanajeshi, kufuatia vifo vya kuruta kumi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vilivyotokea tarehe 3 Februari, 2020 wakati wakiwa katika mafunzo ya kijeshi huko Msata.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pole kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali Sirro na kwa familia za askari watatu wa Jeshi la Polisi waliofariki tarehe 3 Februari, 2020 kwa ajali ya gari Mkoani Njombe. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze kwa amani roho za marehemu hawa.

Vilevile natoa pole kwa wananchi waliopata majanga na kuondokewa na ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali yaliyosababishwa na madhara ya aina mbalimbali ikiwemo mvua kubwa, ajali na magonjwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa mara nyingine tena ninayo heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kabla sijafanya hivyo, naomba nikumbushe dira, dhima na malengo ya Wizara kama inavyojieleza kwenye kitabu changu aya ya 12 na aya 13**.**

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maazimio ya Bunge na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalam; wakati Kamati yako ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala pia zimezingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ninayowasilisha hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa MIAKA MITANO 2016/2017 – 2020/2021; Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020, sambamba na kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na majukumu mengine ya Wizara. Maelekezo ya Ilani kwa Wizara yameainishwa bayana kwenye Ibara ya 146 nautekelezaji wake umeoneshwa katika kiambatanisho namba 1.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mipaka ya nchi kavu na kwenye maji. Kwa upande wa nchi kavu inapakana na nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji na upande mwingine kwenye maji hususan Bahari ya Hindi inapakana na nchi za Comoro na Shelisheli.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari na hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limeendelea kujidhatiti ipasavyo kudhibiti ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, zipo changamoto chache kwenye baadhi ya maeneo ya mipaka ya nchi zinazohitaji kutatuliwa ili udhibiti wa mipaka yetu uzidi kuimarika na kuimarisha ulinzi na wa nchi yetu na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa alama za mipaka kwa baadhi ya maeneo ya mipaka. Aidha, kuendelea kuwepo kwa migogoro ya viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo na imekuwa sababu mojawapo inayochangia wakimbizi na wahalifu kuingia katika nchi yetu. Hata hivyo, juhudi zinaendelea kufanyika kuhakikisha alama za kudumu za mipaka zinawekwa katika maeneo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni wafugaji kutoka baadhi ya nchi tunazopakana nazo kuendelea kuingiza mifugo yao ndani ya nchi yetu. Mfano, katika Ranchi ya Taifa ya Misenyi iliyopo Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera ambapo wafugaji kutoka Rwanda na Uganda huingiza mifugo kutafuta malisho na maji. Vilevile nchi yetu imekuwa ikiendelea kukumbwa na tatizo la wahamiaji haramu kutoka nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Uganda na usafirishaji haramu wa binadamu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia. Baadhi ya wahamiaji haramu wamekuwa wakijihusisha na uhalifu wa aina mbalimbali. Hata

hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ili kuweza kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako na viongozi wengine wote nchini waendelee kuwaelimisha wananchi hususan maeneo ya mipakani kutoa taarifa kuhusu wahamiaji haramu watakaoonekana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, kama ilivyo hapa nchini na duniani kote kwa ujumla na nchi jirani tunazopakana nazo pia na sisi wenyewe tumekumbwa na janga la ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (Covid-19). Hata hivyo, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu. Maelezo ya kina kuhusu hali ya mipaka ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo yameelezwa kwenye aya 22 na aya 28 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 - ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 81,104,000 katika mafungu yake yote matatu mgawanyo wake ni kama unavyojionesha kwenye hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilifanikiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya thamani ya fedha ya kitanzania shilingi 63,153,000 mgawanyo wake unajionesha kwenye Jedwali Namba. 1 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,854,037,343,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake yote matatu. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,726,037,343,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 128,000,000,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya

maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeoneshwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 1,487,607,866,819.10 sawa na asilimia 80.24 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,381,414,181,653.84 ilikuwa nini kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 106,193,685,165.26 ilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo zilizopokelewa kwa mafungu yote matatu umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi 1,381,414,181,653.84 zimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali kwa maafisa, askari, watumishi wa umma, vijana wa mujibu wa sheria na vijana wa kujitolea. Aidha, fedha hizo zimetumika pia kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi, shughuli za kijeshi na kiulinzi ikiwemo mazoezi, mafunzo na operesheni mbalimbali. Vilevile sehemu ya fedha hizo zimetumika kugharamia huduma ya afya kwa wanajeshi, kuwasafirisha maafisa, askari na watumishi wa umma waliostaafu kuanzia mwezi Juni, 2018. Pia fedha hizo zilitumika kugharamia Maadhimisho ya Miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara, kulipa madeni ya huduma ya simu, wazabuni, maafisa, askari na watumishi wa umma. Maelezo ya kina yameoneshwa kwenye aya 38 hadi 46 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya utekelezaji, pamoja na majukumu ya msingi Wizara yangu imeweza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu la Wizara kuhamia rasmi Dodoma, makao makuu ya nchi ambapo Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi na Wananchi wa Tanzania na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa yalihamia rasmi hapa Dodoma tarehe 8 Novemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania imewezesha timu za Jeshi kushiriki michezo ya

majeshi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2019 ambapo mashindano yalifanyika mwezi Agosti, 2019 nchini Kenya na Baraza la Michezo la Majeshi Duniani mwaka 2019 ambako mashindano yalifanyika mwezi Oktaba, 2019 nchini China.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya vijana 20,413 wa mujibu wa sheria *Operation* Makao Makuu Dodoma walipatiwa mafunzo kwenye kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa hapa nchini. Kati ya vijana hao 15,712 ni wa kiume na 4,701 ni wa kike. Kadhalika vijana wapya wa kujitolea *Operation* Makao Makuu Dodoma wapatao 11,099 wamejiunga na mafunzo ya JKT ambapo kati yao wakiume ni 7761 na wakike ni 3338. Vilevile ujenzi na ukarabati wa kambi za JKT umewezesha kuongezeka kwa vijana wanaoandikishwa kujiunga na mafunzo ya mujibu wa sheria na wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa JKT kujitosheleza kwa chakula; Wizara kupitia JKT imeandaa mkakati wa kujitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia Serikali gharama za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT. Katika mwaka wa 2019/2020 Jeshi la Kujenga Taifa nchini limeanza kutekeleza mkakati huo kwa kuzalisha mazao ya kimkakati ambayo ni mahindi, mpunga, maharage, ufuta na alizeti. Uzalishaji wa mazao hayo unafanywa kupitia mashamba ambayo yako chini ya usimamizi wa Makamanda wa Vikosi jumla ya hekari 8,417 zimelimwa msimu huu katika kambi mbalimbali za JKT. Kati ya hekari hizo hekari 2,200 ni za kimkakati ambapo mahindi ni hekari 1,000 mpunga ni hekari 1,000 na maharage ni hekari 200. Hekari hizo zimelimwa katika Vikosi vya Chita, Morogoro na Milundikwa kule Rukwa. Matarajio ya mavuno katika hekari hizo ni kupata tani 1,800 za mpunga na mahindi na tani 120 za maharage.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo mtambuka yakihusisha mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na yasiyoambukiza, utawala bora na utunzaji wa mazingira umeoneshwa kwenye hotuba yangu ukurasa wa 51 mpaka 57.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara imepokea jumla ya shilingi 106,193,685,165.20, hiyo ikiwa ni asilimia 83 ya fedha zote ambazo zilikuwa zimekadiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 upimaji na uhakiki wa maeneo yanayotwaliwa na Jeshi ambayo yanatakiwa kulipiwa fidia umefanyika na umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia kupitia mashirika yake ya Nyumbu na Mzinga imeendelea kufanya tafiti mbalimbali za uhawishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma mbalimbali nchini angalia kwenye hotuba yangu ukurasa wa 64 na 74.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kukumbana na changamoto mbalimbali ambazo pia tumezipatia ufumbuzi wa namna ya kuzitatua angali katika hotuba yangu aya ya 78 na 79.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 utajikita kwenye maeneo yafuatayo; kuimarisha jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa vya mawasiliano pamoja na rasilimali watu; kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa wanajeshi ikiwemo mafunzo, matunzo ya zana, miundombinu, maslahi, huduma bora za afya, ofisi na makazi; kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili iweze kuchukua vijana wengi zaidi na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, stadi za kazi kwa vijana wa Kitanzania; kuendelea kufanya tafiti na uhawishaji wa taknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa

matumizi ya kijeshi na kiraia; kuendelea kuimarisha, kuratibu jeshi la akiba; kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa yaani *UN* na Umoja wa Afrika *(AU)* na Jumuiya nyingine za Kikanda; kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura na kuendelea kupima, kutathmini na kulipa fidia katika maeneo ya ardhi yaliyotwaliwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wafuatao kwa michango yao katika maandalizi ya hotuba hii na kazi zangu za kila siku. Kwanza kabisa namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasiji Mnyepe, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance Salvatory Mabeyo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Yacoub Hassan Mohamed, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Brigedia Jenerali Charles Menera Mbuge na Wakuu wa Kamandi na Wakuu wa Mashirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Idara na vitengo mbalimbali kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Vilevile napenda kuwashukuru wahisani ambao wamekuwa wakishirikiana na Wizara yangu katika mambo mbalimbali ambao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, India, Marekani, Canada, Ufaransa na Uturuki. Aidha, nashukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za kiulinzi nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Falme za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Jamaica, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Morocco, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaotoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu na kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru sana sana na naomba hapa kuweka msisitizo, wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha miaka mitano tangu wanichague kuwakilisha hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa ndani ya nje ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawatakia kila la heri na fanaka kwenye uchaguzi mkuu ujao na ni matumaini yangu kuwa tutakutana tena hapa Bungeni *Inshallah* kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nitumie nafasi hii kuomba fedha kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 85,103,000 kutoka katika mafungu yake yote matatu angalia Jedwali Namba 3.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida na maendeleo; Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,141,034,489,000 kwa mafungu yote matatu ambapo kati yake shilingi 1,977,084,489,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 164 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, mchanganuo wa kila fungu umeoneshwa katika Jedwali Namba 4.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono nakushukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kusoma hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa umahiri mkubwa na kwa ufasaha mkubwa.

# HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB.), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na fadhila kwa kuendelea kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine tena leo hapa Bungeni kwa shughuli hii muhimu. Vile vile, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, kwa kuniteua na kuendelea kuniamini kushika wadhifa huu katika kipindi cha Awamu ya Tano. Nawashukuru pia Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein,** na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe, Spika wa Bunge hili **Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb.)**, Naibu Spika **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)**, pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge la kumi na moja (11) kwa mafanikio makubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu ili muweze kuendelea kuliongoza Bunge letu katika kutekeleza majukumu yake mazito.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.**), aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuanzia Machi, 2018 hadi Januari, 2020. Katika kipindi chote cha uongozi wake aliiongoza Kamati kwa umakini na weledi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo kwa sasa inaongozwa na **Mhe. Salum Mwinyi Rehani (Mb.),** kwa kuchambua na kushauri juu ya kuboresha mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ninayowasilisha leo hapa bungeni. Wakati wote Kamati hii imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa Vyombo vya Ulinzi vya nchi yetu. Serikali na Wizara kwa ujumla imezingatia ushauri huo. Nawashukuru sana.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kumshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ninayoisimamia **Dkt. Florens Martin Turuka** ambaye amestaafu Utumishi wa Umma kwa Mujibu wa Sheria. Kwa niaba ya Wizara tunamshukuru sana kwa kuitumikia Wizara kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Ni imani yetu kuwa ataendeleza ushirikiano huo huko aliko kwa maslahi ya Taifa. Pia, nampongeza **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi kwa **Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.),** kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.**), kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Sambamba na pongezi hizi, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao muhimu ya kuwatumikia wananchi na Taifa kwa ujumla.

*8.* ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, naomba kumpongeza **Kanali Joseph Peter Bakari** kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Michezo ya Kijeshi Duniani ndani ya Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (International Military Sports Council - CISM). Namtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza hilo.

*9.* ***Mheshimiwa Spika***, naungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako **Mhe. Spika**, Waheshimwa Wabunge, familia na wananchi wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu waliokuwa Wabunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika nyakati tofauti. Mnamo tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu liliondokewa na **Mhe. Rashid Ajali Akbar** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, tarehe 20 Aprili, 2020 Bunge liliondokewa na **Mhe. Mch. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare**, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na tarehe 29 Aprili, 2020 liliondokewa pia na **Mhe. Richard Mganga Ndassa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve. Vile vile, kwa namna ya pekee natoa pole kwa **Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu** na kwako Mhe. Spika, Wabunge na wananchi kwa kuondokewa na Waziri wa Katiba na Sheria na Mbunge wa Kuteuliwa **Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga,** aliyefariki tarehe 01 Mei, 2020.

*10.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa **Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi**, Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, Familia za Wanajeshi, kufuatia vifo vya Kuruta 10 wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vilivyotokea tarehe 03 Februari, 2020 wakati wakiwa katika mafunzo ya Kijeshi huko Msata, Mkoani Pwani. Sambamba na hili, natoa pole kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi **Inspekta Jenerali Simon Sirro** na kwa familia za Askari watatu wa Jeshi la Polisi waliofariki tarehe 03 Februari, 2020 kwa ajali ya gari Mkoani Njombe. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze kwa amani roho za marehemu. Vile vile, natoa pole kwa wananchi waliopata majanga na kuondokewa na ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali yaliyosababishwa na madhara ya mvua kubwa, ajali na magonjwa.

*11.* ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo ya utangulizi kwa mara nyingine ninayo heshima kubwa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/21. Kabla sijafanya hivyo, naomba nielezee kwa kifupi Dira, Dhima na Malengo ya Wizara**.**

## DIRA, DHIMA NA MALENGO YA WIZARA

*12.* ***Mheshimiwa Spika***, **Dira** ya Wizara ya Ulinzi na JKT ni kuendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Vile vile, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi mapana ya nchi yetu yanakuwa salama.

*13.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kufanikisha Dira na Dhima, Malengo ya Wizara yameendelea kuwa yafuatayo:

(a) Kuwa na Jeshi dogo lenye wataalam, zana na vifaa vya kisasa;

(b) Kuendelea kuwajengea vijana wa kitanzania ukakamavu, maadili mema, utaifa, moyo wa uzalendo, na uwezo wa kujitegemea;

(c) Kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali za uhawilishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

(d) Kuimarisha Jeshi la Akiba;

(e) Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha maisha, amani na utulivu nchini; na

(f) Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

*14.* ***Mheshimiwa Spika***, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ilitoa maoni, ushauri na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala huo pia zimezingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/21 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

**UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2015-2020 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17 – 2020/21)**

*15.* **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015-2020, sambamba na kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na majukumu mengine ya Wizara. Maelekezo ya Ilani kwa Wizara yameainishwa bayana kwenye Ibara ya 146 katika vifungu vifuatavyo, naomba ninukuu:

(i). "Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea raslimali watu na raslimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu;

(ii). Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama;

(iii). Kuendelea kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa Mujibu wa Sheria;

(iv). Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika shughuli za Ulinzi wa Amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani;

(v). Kuendeleza na kuimarisha mpango wa ulinzi shirikishi na kuwashirikisha wadau mbalimbali nchini kutoa elimu kwa umma dhidi ya imani potofu zinazosababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi (Albino). Aidha, hatua kali na za haraka za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kujihusisha na uhalifu wa aina hii, ujambazi na vitendo vyenye mwelekeo wa ugaidi; na

(vi). Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka (cross border crimes) hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha (Money Laundering), biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu".

*16.* ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani kwa ufanisi kama ilivyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 1.**

## HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

*17.* ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu ina mipaka ya nchi kavu na kwenye maji. Kwa upande wa nchi kavu inapakana na nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji na upande wa kwenye maji hususan bahari ya Hindi inapakana na nchi za Comoro na Shelisheli.

*18.* ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, hali ya Ulinzi na Usalama wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari na hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limeendelea kujizatiti ipasavyo kudhibiti ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, zipo changamoto chache kwenye baadhi ya maeneo ya mipaka ya nchi zinazohitaji

kutatuliwa ili udhibiti wa mipaka yetu uzidi kuimarika na kuimarisha usalama wa nchi yetu.

*19.* ***Mheshimiwa Spika***, miongoni mwa changamoto hizo ni uharibifu wa alama za mipaka kwa baadhi ya maeneo ya mipaka. Aidha, kuendelea kuwepo kwa migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo imekuwa sababu mojawapo inayochangia wakimbizi na wahalifu kuingia nchini. Hata hivyo, juhudi zinaendelea kufanyika kuhakikisha alama za kudumu za mipaka zinawekwa katika maeneo ya Taifa letu.

*20.* ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto nyingine ni wafugaji kutoka baadhi ya nchi tunazopakana nazo kuendelea kuingiza mifugo yao ndani ya nchi yetu. Mfano, katika Ranchi ya Taifa ya Misenyi iliyopo Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera ambapo wafugaji kutoka Rwanda na Uganda huingiza mifugo kutafuta malisho na maji. Vile vile, nchi yetu imeendelea kukumbwa na tatizo la wahamiaji haramu kutoka nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Uganda na usafirishaji haramu wa binadamu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia. Baadhi ya wahamiaji haramu wamekuwa wakijihusisha na uhalifu wa aina mbalimbali. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ili kudhibiti hali hiyo. Mheshimiwa Spika naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi waendelee kuwaelimisha wananchi hususan maeneo ya mipakani kutoa taarifa kuhusu wahamiaji haramu watakao onekana katika maeneo yao.

*21.* ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hayo, kama ilivyo hapa nchini na duniani kote kwa ujumla na nchi jirani tunazopakana nazo pia zimekumbwa na janga la ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-19). Hata hivyo, Serikali kupitia vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama inaendelea kuchukua hatua madhubuti kuimarisha ulinzi wa mipaka.

**Mpaka wa Mashariki**

*22.* ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka wa Mashariki una urefu wa kilomita **1,424** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya, Visiwa vya Shelisheli, Comoro na Msumbiji. Hali ya Ulinzi na Usalama katika mpaka huu ni shwari. Changamoto zilizopo ni pamoja na; uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi, biashara za magendo na kutumika kama mapitio ya wahamiaji haramu, usafirishaji wa madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu. JWTZ kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Usalama linaendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama ili kukabiliana na changamoto hizo kwa kufanya doria za mara kwa mara. Kutokana na hatua hizo matukio hayo yameendelea kupungua.

**Mpaka wa Kaskazini**

*23.* ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka huu una urefu wa kilomita **1,281.2** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, ipo changamoto ya baadhi ya wavuvi wa Tanzania kukamatwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya nchi jirani. Mfano, tarehe 17 Machi, 2020 wavuvi 73 wakiwa na boti 5 walikamatwa katika Kisiwa cha Rasi Jimbo eneo la Bazo katika Bahari ya Hindi kwa tuhuma za kufanya uvuvi kwenye eneo la Kenya. Kufuatia juhudi za Kidiplomasia kati ya Serikali ya Tanzania na Kenya wavuvi hao waliachiwa huru tarehe 18 Machi, 2020 baada ya kulipa faini.

*24.* ***Mheshimiwa Spika***, aidha, katika mpaka huu eneo la nchi kavu lina vipenyo vingi vinavyoshawishi uwepo wa biashara za magendo, uhamiaji haramu na uhalifu. Vile vile, mwingiliano wa wakazi pamoja na raia wa kigeni wa maeneo ya vijiji vya Mkwaja Kipumbwi (Pangani) na vijiji vya Moa na Jasini (Mkinga) mkoani Tanga unahatarisha usalama wa nchi. JWTZ limeendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama katika maeneo hayo kwa kufanya doria na kuanzisha Viteule vya ulinzi.

*25.* ***Mheshimiwa Spika***, katika mpaka wa Tanzania na Uganda kuna matatizo ya kuharibiwa alama za mipaka (Boundary Pillars - BP) na ujenzi holela unaofanywa na baadhi ya watu

waishio maeneo ya mipakani kwa lengo la kujipatia ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho na makazi. Aidha, matatizo ya mpaka kati ya Tanzania na Uganda yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

**Mpaka wa Magharibi**

*26.* ***Mheshimiwa Spika***, mpaka huu una urefu wa kilomita **1,220** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali ya Ulinzi na Usalama katika mpaka huu ni shwari. Hata hivyo, yamekuwepo matukio ya uhalifu yakiwemo mauaji yaliyofanywa na makundi ya waasi ya *Allied Democratic Forces* (ADF), *Democratic Forces for Liberation of Rwanda* (FDLR), *The Republican Forces of Burundi* (FOREBU), *National Liberation Forces* na MAIMAI. Pia, kumekuwepo na matukio ya ujenzi wa makazi na kilimo ndani ya eneo la mkuza, ambalo linapaswa kuwa wazi kulingana na makubaliano kati ya nchi na nchi. Pamoja na kuwepo hali hiyo JWTZ kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama limeendelea kufuatilia kwa karibu hali ya usalama katika nchi hizo.

**Mpaka wa Kusini**

*27.* ***Mheshimiwa Spika***, mpaka huu una urefu wa kilomita **1,536** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya Ulinzi na Usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, usalama wa mpaka huu unatishiwa na kundi la kigaidi la "**Ansar Al Sunnah Wa Jamaah (AASWJ**)" katika mpaka wa Msumbiji ambalo linaendelea kufanya uhalifu nchini Msumbiji katika Jimbo la Cabo Delgado. Eneo lenye mgogoro lipo jirani na mpaka wa nchi yetu (Mkoa wa Mtwara). Katika hatua ya kuimarisha ulinzi wa mpaka huu, mwezi Machi, 2020, Serikali ilipeleka vikundi vya ulinzi katika maeneo ya Msimbati na Sindano, Mkoa wa Mtwara na Chiwindi katika Wilaya ya Nyasa Mkoa wa Ruvuma.

*28.* ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama wa mpaka wa Tanzania na Malawi imeendelea kuwa shwari kwani hakuna tishio la wazi dhidi ya nchi yetu. Changamoto ya mpaka katika Ziwa Nyasa inaendelea kufanyiwa kazi. Serikali yetu

kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu, ambapo imekubalika kuwa pande husika zisijishughulishe na utafiti wa kiuchumi katika eneo lenye mgogoro.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/20

### Ukusanyaji wa Maduhuli

*29.* **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 81,104,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu kama ifuatavyo:Fungu 38 – NGOME **Shilingi 20,001,000.00,** Fungu 39 - JKT **Shilingi 59,903,000.00** na Fungu 57 - Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

*30.* **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilifanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 67,153,000.00** sawa na **asilimia 82.80** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 – NGOME lilikusanya **Shilingi 11,500,000.00** ambazo zimetokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na kamisheni zinazotokana na JWTZ kuwa wakala wa ukusanyaji wa makato ya bima zinazokatwa kwa Wanajeshi kutoka makampuni mbalimbali ya bima. Fungu 39 – JKT lilikusanya **Shilingi 55,653,000.00** zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na mauzo ya mazao ya kilimo ikiwemo mboga mboga na matunda na Fungu 57 – Wizara, halikuweza kukusanya maduhuli kwa kipindi husika kwa kuwa mapato iliyoyategemea kutokana na pango la kantini kutopatikana kufuatia kufungwa kwa kantini iliyokuwepo Dar es Salaam baada ya watumishi kuhamishiwa Dodoma. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Namba. 1**

**Jedwali Na 1: Makadirio ya Mapato na Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20**

| Fungu | Makadirio ya Mapato 2019/20 | Makusanyo Julai 2019 hadi Machi, 2020 | Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|
| 38 – NGOME | 20,001,000.00 | 11,500,000.00 | 57.00 |
| 39 – JKT | 59,903,000.00 | 55,653,000.00 | 92.90 |
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 | 0 | - |
| **Jumla** | **81,104,000.00** | **67,153,000.00** | **82.80** |

## Matumizi ya Kawaida

31. ***Mheshimiwa* Spika,** katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,854,037,343,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,726,037,343,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **Shilingi 128,000,000,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeoneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2 Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa Fungu**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (TZS) | Matumizi ya Maendeleo (TZS) | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|
| 38-NGOME | 1,406,726,908,000.00 | 6,000,000,000.00 | 1,412,726,908,000.00 |
| 39-JKT | 300,035,425,000.00 | 2,000,000,000.00 | 302,035,425,000.00 |
| 57-Wizara | 19,275,010,000.00 | 120,000,000,000.00 | 139,275,010,000.00 |
| **Jumla** | **1,726,037,343,000.00** | **128,000,000,000.00** | **1,854,037,343,000.00** |

32. ***Mheshimiwa* Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,487,607,866,819.10** sawa na **asilimia 80.24** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,381,414,181,653.84** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 106,193,685,165.26** ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu yote matatu umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

*33.* ***Mheshimiwa* Spika,** fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Shilingi 1,381,414,181,653.84** zimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, Vijana wa Mujibu wa Sheria na wa Kujitolea. Aidha, fedha hizo zimetumika pia kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi, shughuli za kijeshi na kiulinzi ikiwemo mazoezi, mafunzo na operesheni. Vile vile, sehemu ya fedha hizo zimetumika kugharamia huduma ya afya kwa Wanajeshi, kuwasafirisha Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliostaafu kuanzia mwezi Juni, 2018. Pia, fedha hizo zilitumika kugharamia Maadhimisho ya Miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara, kulipa madeni ya huduma ya simu ya TTCL, wazabuni, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma.

*34.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 106,193,685,165.26** sawa na **asilimia 83.00** ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha hizo zimetumika katika kuliimarisha Jeshi kwa ununuzi wa zana na vifaa, kujenga miundombinu muhimu ya Jeshi, ukarabati wa zana na miundombinu ya Jeshi, kugharamia ukamilishwaji wa uundaji wa magari mawili ya zimamoto na kugharamia uwekaji wa umeme kwenye Minara ya Mawasiliano Salama Jeshini kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (Rural Energy Agency – REA). Vile vile, Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi zake.

*35.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, upimaji na uhakiki wa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi ambayo yanatakiwa kulipwa fidia umeendelea kufanyika. Aidha, usuluhishi wa migogoro unaendelea kufanyika katika maeneo ya Chita - Morogoro, Nachingwea - Lindi, Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) - Arusha, Kunduchi (KTC) na Kimbiji– Dar es Salaam. Vile vile, Wizara imefanikiwa kupata Hati Miliki za maeneo mawili ya Jeshi ambayo ni Msasani Beach Club (Dar es Salaam) na Tarime Mjini (Mara). Pia, uthamini umefanyika katika maeneo ya Kigongo Feri na Ilemela - Mwanza, Nyamisangura - Mara na Kaboya – Kagera.

## Maelezo ya Matumizi ya Fedha za Kawaida

*36.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za matumzi ya kawaida kama ifuatavyo:-

### (a) Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi

*37.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika shule na vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwapatia Wanajeshi mafunzo ya awali na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali na uongozi.

*38.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika suala la kuwajengea weledi Maafisa na Askari wetu limeendelea kupewa uzito mkubwa ambapo yamefanyika pia mazoezi mbalimbali ya kitaifa na ya kimataifa yafuatayo: **SHARED ACCORD;** Zoezi hili lilifanyika nchini Rwanda Agosti, 2019, **USHIRIKIANO IMARA 2019;** Zoezi hili la kituo cha uamrishaji (Command Post Exercise) lilifanyika nchini Uganda Novemba, 2019; na maandalizi ya zoezi la **BEACH LANDING OPERATION** yaliyofanyika Bagamoyo, Mapinga kuanzia tarehe 22 Desemba, 2019 hadi 16 Januari, 2020.

### (b) Mafunzo ya Jeshi la Akiba

*39.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limetoa mafunzo kwa Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali. Mafunzo hayo yalijumuisha wananchi kutoka katika mikoa yote ya Tanzania.

### (c) Huduma za Afya na Tiba

*40.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa Maafisa, Askari, Vijana wa JKT, Watumishi wa Umma, familia zao na wananchi kwa ujumla. Aidha, imeendelea kuboresha huduma za afya na tiba kwa kununua dawa na vifaa tiba ili kukidhi mahitaji ya Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Hospitali za Kanda na Vituo vya Tiba Vikosini, ununuzi wa mashine za kusafishia figo na utoaji wa huduma ya usafishaji wa figo. Vile vile, JWTZ limejipanga kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kupambana na ugonjwa wa homa

kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19).

**(d) Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine**

*41.* ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na nchi mbalimbali katika masuala ya kiulinzi na kiusalama katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya maeneo hayo ni mafunzo, misaada ya kitaalam, vifaa, zana na mitambo. Mpaka sasa JWTZ linashirikiana na nchi za Jumuiya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) katika mafunzo na ubadilishanaji wa wataalam. Aidha, JWTZ linapata msaada wa mafunzo kwa Maafisa na Askari kutoka nchi zifuatazo: China, Misri, Marekani, Ujerumani, India, Urusi, Uingereza, Bangladesh, Morocco, Canada, Uholanzi, Indonesia na Jamaica.

*42.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (PLA) ilitoa msaada wa magari idadi arobaini kwa ajili ya Makamanda wa JWTZ pamoja na ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi awamu ya pili. Aidha, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Ujerumani kupitia kikundi cha *Germany Armed Forces Technical Adivisory Group* (GAFTAG) imetoa msaada wa ujenzi wa karakana ya matengenezo ya magari, ujenzi wa Hospitali Kuu ya Kanda Arusha, Ujenzi wa mahanga ya Maafisa na Askari katika Chuo cha Ulinzi wa Amani Kunduchi Dar es Salaam na italijengea Jeshi Hospitali Kuu ya Rufaa ( Level Four Hospital) Jijini Dodoma.

*43.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) inaendesha mafunzo ambapo mpaka sasa inashirikiana na nchi zifuatazo katika mpango wa ubadilishanaji wa washiriki wa kozi hiyo kwa lengo la kubadilishana uzoefu. Baadhi ya nchi hizo ni China, Zimbabwe, Afrika Kusini, Kenya, Misri, Nigeria, Rwanda, Malawi, Zambia, Namibia, Botswana, Burundi na Bangladesh.

**(e) Ushiriki wa JWTZ katika shughuli za Ulinzi wa Amani**

*44.* ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ limeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro kwa kupeleka vikosi, Waangalizi wa Kijeshi, Wanadhimu na Makamanda. Mpaka sasa JWTZ lina Vikosi vya ulinzi wa Amani katika nchi zifuatazo: Lebanon (**UNIFIL),** Sudan (**UNAMID),** Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (**MONUSCO Force Intervention Brigade – FIB)** na Jamhuri ya Afrika ya Kati (**MINUSCA)** . Aidha, Jeshi lina Maafisa Wanadhimu, Waangalizi wa Kijeshi, na Makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Lebanon, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan Kusini na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**(f) Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia Katika Shughuli Mbalimbali za Kitaifa**

*45.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali za maendeleo na huduma za kijamii. Maeneo mbalimbali ambayo JWTZ limeshirikiana na Mamlaka za Kiraia ni: utoaji wa huduma za afya na tiba kwa wananchi ambapo takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba **asilimia 70** ya wanaopata huduma katika Hospitali za Jeshi ni raia; usafirishaji wa korosho kutoka kwenye maghala kupeleka bandarini kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi; usafirishaji wa vitabu vya kiada na ziada kwenda mikoa mbalimbali nchini; ushiriki katika kuboresha huduma katika Taasisi za Serikali; kuhamisha mizigo ya wizara mbalimbali kuja Makao Makuu ya Serikali Dodoma, kusaidia ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu na majengo mbalimbali ya Serikali, na kuondoa miti katika eneo la mradi wa Bwawa la Umeme Rufiji (Julius Nyerere Hydro Power Project).

*46.* ***Mheshimiwa Spika*****,** kupitia Shirika la Mzinga, Wizara imeendelea kusimamia zana na silaha zinazomilikiwa na mashirika mbalimbali yanayoingiza meli katika bandari zetu ili kuzuia matumizi mabaya ya silaha hizo. Jukumu hilo

limekuwa likienda sambamba na utunzaji wa silaha zinazomilikiwa na meli kutoka nje ya nchi mara tu zinapotia nanga kwenye bandari za nchi yetu.

**(g) Maeneo mengine ya utekelezaji**

*47.* ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na majukumu ya msingi, Wizara imeweza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu la Wizara kuhamia rasmi Dodoma ambapo Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) yalihamia tarehe 08 Novemba, 2019.

*48.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia JWTZ imewezesha Timu za Jeshi kushiriki Michezo ya Majeshi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2019, ambapo mashindano yalifanyika mwezi Agosti, 2019 nchini Kenya na Baraza la Michezo ya Majeshi Duniani (International Military Sports Council - CISM) 2019 ambapo mashindano yalifanyika mwezi Oktoba, 2019 nchini China.

**(h) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana**

*49.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya vijana **20,413** wa Mujibu wa Sheria "Operesheni Makao Makuu Dodoma" walipatiwa mafunzo kwenye Kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa. Kati ya vijana hao **15,712** ni wa kiume na **4,701** ni wa kike. Kadhalika, vijana wapya wa kujitolea "Operesheni Makao Makuu Dodoma" wapatao **11,099** wamejiunga na mafunzo ya JKT, ambapo kati yao wa kiume ni **7,761** na wa kike ni **3,338**. Vile vile, Ujenzi na Ukarabati wa Kambi za JKT umewezesha kuongezeka kwa vijana wanaoandikishwa kujiunga na mafunzo ya Mujibu wa Sheria na wa kujitolea.

**(i) Mkakati wa JKT Kujitosheleza kwa Chakula**

*50.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imeandaa mkakati wa kujitosheleza kwa chakula ili kuipunguzia Serikali gharama

za kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT. Katika mwaka 2019/20 Jeshi la Kujenga Taifa limeanza kutekeleza mkakati huo kwa kuzalisha mazao ya kimkakati ambayo ni mahindi, mpunga, maharage, ufuta na alizeti. Uzalishaji wa mazao hayo unafanywa kupitia mashamba ambayo yako chini ya usimamizi wa Makamanda Vikosi. Jumla ya **ekari 8,417** zimelimwa msimu huu katika kambi mbalimbali za JKT. Kati ya ekari hizo, **ekari 2,200** ni za kimkakati ambapo, mahindi ni ekari 1000, mpunga ni ekari 1000 na maharage ni ekari 200. Ekari hizo zimelimwa katika vikosi vya Chita-Morogoro na Milundikwa-Rukwa. Matarajio ya mavuno katika ekari hizo ni kupata tani 1,800 za mpunga na mahindi, na tani 120 za maharage.

### (j) Mapambano Dhidi ya Magonjwa Ambukizi na Yasiyoambukiza

*51.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI pamoja na magonjwa mbalimbali yasiyoambukizwa kama vile kisukari, shinikizo la damu, n.k. Aidha, elimu imekuwa ikitolewa katika vituo na hospitali zenye huduma ya mama na mtoto (Reproductive and Child Health) kwa lengo la kutokomeza maambukizi ya mama kwa mtoto, kushiriki mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa tiba na kutoa ushauri nasaha kwa walioambukizwa na kutoa elimu ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya. Vile vile, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa Watumishi kuhusu ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) na namna ya kujikinga.

*52.* ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, kwa wale wenye Virusi vya UKIMWI wamekuwa wakipatiwa dawa za kupunguza makali ya Virusi (ARV's) bure katika vituo vya huduma na matibabu (Care and Treatment Centres) vilivyo katika Hospitali Kuu za Kanda. Kwa upande wa magonjwa yasiyoambukizwa jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika ikiwemo kutoa elimu ya afya ili kupunguza magonjwa hayo, kupima afya mara kwa mara, kushauri Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma kuacha uvutaji wa sigara, unywaji pombe uliopitiliza na kufanya mazoezi ya mwili na michezo.

**(k) Utawala Bora**

*53.* ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara imeendelea kutekeleza dhana ya Utawala Bora katika maeneo ya kazi kwa kushirikisha watumishi wake kupitia vikao mbalimbali kama vile Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Maadili, Bodi ya Manunuzi na Kamati ya Ajira. Wizara pia imeendelea kuimarisha jitihada za kupambana na rushwa. Kwa upande wa mapambano dhidi ya rushwa, taarifa za kila robo mwaka zimekuwa zikiandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Aidha, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wameendelea kuhimizwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya utendaji kazi bila kusahau uzalendo na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

**(l) Utunzaji wa Mazingira**

*54.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika Mwaka wa Fedha 2019/20, baadhi ya vikosi, shule na vyuo vya kijeshi vimeanza kutumia nishati ya gesi badala ya kutumia kuni na mkaa. Aidha, Jeshi limefanya tathmini ya usambazaji wa mabomba ya gesi ya asili ili kuviwezesha vikosi vyote vinavyopitiwa na bomba la gesi kutumia nishati hiyo.

*55.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inamiliki maeneo mengi na makubwa yenye miti ya asili ambayo hutunzwa kwa kufanya doria mbalimbali, hivyo kufanya maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, mfano eneo la Pongwe Msungura lililopo Msata, Mkoa wa Pwani na Ngerengere lililopo Morogoro. Kwa ujumla maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti na kuchoma mkaa.

*56.* ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika yaliyo chini ya Wizara, *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC) - NYUMBU na MZINGA yanafanya uzalishaji kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira. Uzalishaji huo hutumia njia za kisasa za kutibu maji yenye kemikali (water treatment) yanayotoka viwandani. Vile vile, viwanda vina utaratibu wa kuwapa wafanyakazi wake vifaa kinga na vina mfumo wa kudhibiti sauti ili kuzuia kelele.

*57.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara kupitia Shirika la TATC - NYUMBU imefanikiwa kufanya utafiti na kubuni mashine kwa ajili ya uzalishaji wa nishati mbadala. Mashine hizo ni za *Agrowaste briquette* na *Coal briquette* ambazo zinatumia mabaki ya mashambani, vyakula, vumbi la makaa ya mawe na udongo mfinyanzi kutengeneza mkaa.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

*58.* ***Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za maendeleo kama ifuatavyo:-

**i. Ununuzi wa zana na vifaa, ujenzi na ukarabati wa miundombinu**

*59.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Wizara imeendelea kununua zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi pamoja na kugharamia matengenezo na utunzaji wake kwa ajili ya kuliimarisha Jeshi letu. Aidha***,*** Wizara imeendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, ukamilishaji wa Makao Makuu ya JKT, ujenzi wa kambi ya JKT Kibiti (Pwani) na ukamilishwaji wa ujenzi na ukarabati wa Kambi za JKT zifuatazo: Makuyuni (Arusha); Mpwapwa na Makutupora (Dodoma); Itaka (Songwe); Milundikwa na Luwa (Rukwa); Bulombora (Kigoma); Mbweni (Dar es Salaam); Nachingwea (Lindi); Mafinga (Iringa) na Maramba (Tanga).

**ii. Mawasiliano Salama Jeshini**

*60.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini, pamoja na kukamilisha shughuli za kuunganisha mtandao wa mawasiliano ambapo hadi sasa yanapatikana katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeingia mkataba na *M/S Electrical Transmission and Distribution Construction and Maintenance Company Limited (ETDCO)* ambayo ni Kampuni Tanzu ya TANESCO kuipatia umeme minara 74.

Kampuni hiyo imekwishaanza kusambaza nguzo za umeme kuanzia mkoa wa Dodoma kuelekea mikoa ya Kanda ya Magharibi. Upatikanaji wa Nishati hiyo utawezesha Mawasiliano kupatikana katika vikosi vilivyopo Mikoa tisa iliyobaki kwenye Kanda ya Kusini, Magharibi, Ziwa na Kaskazini.

**iii. Upimaji, Uthamini na Ulipaji Fidia**

*61.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kufanya upimaji na uthamini wa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi ambayo yanatakiwa kulipwa fidia. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara imefanya uthamini katika maeneo ya Kigongo Feri na Ilemela - Mwanza, Nyamisungura –Mara na Kaboya – Kagera pamoja na ufufuaji wa mipaka na upimaji upya (Boundary Restoration and Resurvey) eneo la Kimbiji – Kigamboni. Vile vile, Wizara imefanikiwa kupata Hati Miliki za maeneo mawili ya Jeshi ambayo ni Msasani Beach Club (Dar es Salaam) na Tarime mjini (Mara). Katika kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi, Wizara imeendelea kurekebisha mipaka ya maeneo hususan maeneo ya Jeshi yaliyoko mijini, mfano Kambi ya Kunduchi KTC – Dar es Salaam.

*62.* ***Mheshimiwa Spika***, naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi kuendelea kuwaelimisha wananchi kuacha kuvamia maeneo ya Jeshi.

**iv. Ufuatiliaji na Tathmini**

*63.* **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ilifanya ufuatiliaji na tathmini katika miradi iliyopatiwa fedha kwa ajili ya kupata taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa ujumla unaendelea vizuri. Hata hivyo, kwa baadhi ya miradi kuna changamoto zilizojitokeza na hatua za utatuzi wake ziliainishwa kwa ajili ya kufanikisha ukamilishaji wake.

**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MASHIRIKA YANAYOSIMAMIWA NA WIZARA**

*64.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mashirika yake ya TATC - NYUMBU, MZINGA na SUMAJKT imeendelea kufanya tafiti

na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia.

**Shirika la TATC - NYUMBU**

*65.* ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali kwa matumizi ya kijeshi na kiraia. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Shirika limeendelea kutoa mchango wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa kukarabati vifaa na zana za kijeshi kwa ajili ya vikosi vya ulinzi wa amani, magari ya kivita na vifaa mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Vile vile, Shirika limeweza kuunganisha magari mawili ya zimamoto ambapo gari moja limekamilika na lingine limefikia **asilimia 70.** Shirika pia limeendelea kutengeneza vipuri vya mitambo mbalimbali kwa ajili ya matumizi katika sekta za ulinzi, kilimo, usafirishaji, madini na maji. Pia, Shirika limefanikiwa kutengeneza *terminal traillers* tano kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na *Brake blocks* kwa ajili ya matumizi ya Shirika la Reli Tanzania.

**Shirika la MZINGA**

*66.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika limeendelea na shughuli za uzalishaji wa zao la msingi kwa ajili ya matumizi ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Shirika pia limeendelea kuagiza na kusambaza baruti zinazotumika katika ujenzi na uchimbaji wa madini. Aidha, Shirika linaendelea na utafiti wa uzalishaji wa malighafi na vipuri vinavyotumika katika zao la msingi. Vile vile**,** Shirika limefanya ukarabati wa silaha mbovu kutoka kwa washitiri mbalimbali na kutengeneza mabomu ya kufukuzia wanyama (thunderflash) ambayo hutumiwa zaidi na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa - TANAPA.

*67.* ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia kampuni yake Tanzu ya ujenzi (Mzinga Holding Company Limited), limeendelea na shughuli mbalimbali zikiwemo ujenzi wa majengo ya Taasisi za Umma na Watu Binafsi. Baadhi ya shughuli zinazoendelea katika kipindi hiki ni za ujenzi wa: Hospitali ya Nyamagana

(Mwanza); Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi (Singida); Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu (Manyara); Ofisi ya Halmashauri ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busekelo (Mbeya); majengo ya Hosteli ya Watawa Kashozi (Bukoba); kiwanda cha sukari Kagera; na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Sambamba na shughuli hizo Shirika linafanya ukarabati wa Shule ya Sekondari Kahororo na Shule ya Sekondari Bukoba.

**Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT)**

*68.* ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 SUMAJKT limeendelea kutekeleza shughuli zake katika misingi ya kibiashara kupitia Kampuni Tanzu na Idara zake ambazo ni Kampuni ya Ujenzi (SUMAJKT Construction Company Ltd), Kampuni ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd), Idara ya Viwanda na Mradi wa Matrekta. Katika kipindi husika Shirika limetekeleza shughuli zifuatazo:

*69.* ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT kupitia Kampuni yake tanzu ya SUMAJKT Construction Company Limited (SCCL) limetekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi ikiwemo; Ujenzi wa Vituo vya Madini katika Mikoa ya Tanga (Handeni), Ruvuma (Songea), Katavi (Mpanda), Mbeya (Chunya), Simiyu (Bariadi), Mara (Musoma) na Kagera (Bukoba); ujenzi wa Majengo ya Halmashauri za Wilaya za Kibaha, Kibiti, Mpimbwe, Chamwino, Kondoa, Simanjiro, Kalambo, Mafinga, Mpanda, Nsimbo na Newala. Vile vile, Kampuni hiyo ya ujenzi imetekeleza ujenzi wa majengo katika Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Maabara ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), ujenzi wa Hosteli na Madarasa Chuo Kikuu cha Mzumbe, ujenzi wa sakafu ngumu (Paving) ya Bandari Kavu (Dry Port) Kwala na ukarabati wa Hosteli ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

*70.* ***Mheshimiwa Spika,*** SUMAJKT kupitia *SUMAJKT Construction Company Limited* (SCCL) limefanikiwa kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi kupitia Kanda saba (7) ikiwemo ujenzi wa: madarasa ya Shule ya Sekondari Lindi, Chuo cha Ustawi wa Jamii, Zahanati, Jiko na

Karakana Ikulu, *One Stop Centre* – Mirerani, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kyerwa, Jengo la Utawala DUCE, Hospitali ya Rufaa Katavi, Chuo cha Ualimu Kabanga, hoteli ya kitalii Chato, Hospitali ya Rufaa Bariadi, na Jijini Dodoma ujenzi wa jengo Makao Makuu ya Uhamiaji, Hospitali ya Uhuru, Ofisi ya Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

*71.* ***Mheshimiwa Spika,*** *SUMAJKT Guard Ltd,* hutoa huduma ya ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Mpaka sasa Kampuni imeajiri jumla ya walinzi **10,633** ikilinganishwa na walinzi **8,574** waliokuwepo Juni, 2019. Taasisi zinazopata huduma zimeongezeka kutoka **270** na kufikia **369** hadi kufikia mwezi Machi, 2020.

*72.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, SUMAJKT limeendelea kuimarisha viwanda vyake vikiwemo: Kiwanda cha Ushonaji- Mgulani (National Service Garments Factory) ambacho kinaendelea kushona sare za Wanajeshi ili kupunguza gharama za kuagiza sare hizo nje ya nchi; Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi (SUMAJKT Leather Products) – Mlalakuwa JKT, ambacho huuza bidhaa zake kwa Maafisa na Askari wa JWTZ, Walinzi wa *SUMAJKT Guard Ltd*, Mgambo na Kampuni Binafsi za Ulinzi. Kiwanda cha Maji ya Kunywa Mgulani Dar es Salaam, Kiwanda cha kuchakata nafaka za Mahindi - Mlale (Songea) na Kiwanda cha Samani - Chang'ombe - Dar es Salaam ambacho hutengeneza samani za aina mbalimbali za Maofisini na Majumbani.

*73.* ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia Mradi wake wa Matrekta limeendelea kuagiza na kuuza matrekta, vipuri na zana zake kwa bei nafuu ili kumfanya mkulima kuweza kumudu kununua. Aidha, mradi umefanikiwa kuuza matrekta 67 kati ya matrekta 100 yaliyoagizwa mwaka 2018/19 na mradi unatarajia kuagiza matrekta mengine 100 kabla ya Juni, 2020. Mradi huu bado unaendelea kuifanyia kazi changamoto ya urejeshwaji wa madeni kwa wakati kutoka kwa wateja waliokopeshwa matrekta na zana zake ambapo hadi kufikia Machi, 2020 mradi ulikuwa unadai wateja wake kiasi cha **Shilingi 34,975,526,768.32** kutoka deni la **Shilingi 35,395,604,512.83**

mwezi Julai, 2019. Jitihada za kukusanya madeni kutoka kwa wateja wanaodaiwa wakiwemo Viongozi wa Serikali, Wabunge, Watumishi wa Umma na watu binafsi zinaendelea kufanyika.

*74.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 SUMAJKT kupitia shughuli zake mbalimbali limeweza kupata mapato ya **Shilingi 64,924,594,208.73.** Aidha, Shirika linaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali ili kuipunguzia Serikali gharama za uendeshji wa mafunzo ya vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/20

*75.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20 changamoto mbalimbali zimejitokeza zikiwemo upungufu wa rasilimali fedha na watu pamoja na Washitiri kutokulipa madeni. Kwa upande wa rasilimali fedha kiasi cha fedha za maendeleo na matumizi mengineyo kilichoidhinishwa ni pungufu ukilinganisha na kiasi kinachohitajika kutekeleza majukumu ya msingi ya Wizara.

*76.* ***Mheshimiwa Spika,*** upungufu huo umesababisha Wizara kutofikia malengo ya utekelezaji kwa baadhi ya maeneo hususan utafiti na uzalishaji wa mazao ya msingi katika viwanda vya Kijeshi, upimaji, uthamini na kulipa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, kuboresha makazi, kambi na ofisi, kuboresha Mawasiliano Salama Jeshini, kugharamia matengenezo na matunzo ya zana na vifaa, kugharamia likizo na uhamisho kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma, kutoa viwango vya fedha za chakula kulingana na mahitaji halisi na kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi waliotoa huduma mbalimbali.

77. ***Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa rasilimali watu, Mashirika ya MZINGA na TATC - NYUMBU yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa rasilimali watu iliyosababishwa na watumishi kustaafu. Aidha, SUMAJKT linakabiliwa na changamoto ya washitiri kutolipia huduma kwa wakati na kuzalisha madeni kwa Shirika ambayo yanakwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali na malengo ya Shirika.

**HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

*78.* ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha, kwa kuendelea kutumia vizuri fedha inayotolewa kutekeleza majukumu yake. Pia, Wizara imeendelea kukutana na wazabuni pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kupitia na kukubaliana utaratibu wa kulipa madeni husika. Aidha, majadiliano yanaendelea kati ya Wizara na Wizara ya Fedha na Mipango kuona uwezekano wa kuongeza wigo wa bajeti kulingana na majukumu na vipaumbele vya Wizara.

*79.* ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupata vibali vya ajira kuziba nafasi zilizo wazi ili kukabiliana na upungufu wa rasilimali watu katika Mashirika ya MZINGA na TATC - NYUMBU. Aidha, Mashirika yameandaa mipango ya maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu. Shirika la TATC - NYUMBU limeandaa Mpango wa Miaka Kumi (2019/20 – 2028/29) wa kuliimarisha ambao upo katika hatua za majadiliano ngazi ya Kamati ya Makatibu
Wakuu, ili hatimaye uwasilishwe kwenye Baraza la Mawaziri kupata ridhaa na kuweza kutekelezwa. Shirika la Mzinga limeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2017/18 – 2021/22). Vile vile, Wizara kupitia SUMAJKT imeendelea na juhudi mbalimbali za kukusanya madeni kwa kutumia kampuni ya ukusanyaji madeni na mnada ya SUMAJKT (SUMAJKT Auction Mart).

**MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI MWAKA WA FEDHA 2020/21**

*80.* ***Mheshimiwa Spika*****,** Mpango na Mwelekeo wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2020/21 ni kutekeleza majukumu yake kwa weledi kulingana na Dira na Dhima yake. Mwelekeo wa kazi zinazokusudiwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha 2020/21 utazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

(a) Kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano pamoja na rasilimali watu;

(b) Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa Wanajeshi ikiwemo mafunzo, matunzo ya zana na miundombinu, maslahi, huduma bora za afya, ofisi na makazi;

(c) Kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi kwa vijana wa Kitanzania;

(d) Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

(e) Kuendelea kuimarisha na kuratibu Jeshi la Akiba;

(f) Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kikanda na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi;

(g) Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika; na

(h) Kuendelea kupima, kuthamini na kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kutoka kwa wananchi kwa matumizi ya Jeshi.

**SHUKRANI**

*81.* ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wafuatao kwa michango yao katika maandalizi ya Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu: Katibu Mkuu **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi **Jenerali Venance Salvatory Mabeyo**, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi **Luteni Jenerali Yacoub Hassan Mohamed**, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa **Brigedia Jenerali Charles Mang'era Mbuge**, Wakuu wa Kamandi na Wakuu wa Mashirika.

*82.* ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wa Wizara kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika

kufanikisha majukumu ya Wizara. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii.

*83.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitakuwa mnyimi wa fadhila endapo sitawashukuru Wahisani mbalimbali waliotoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maendeleo ya Jeshi. Wahisani hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, India, Marekani Canada, Ufaransa, na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Falme za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Jamaica, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Morocco, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Maendeleo Kusini mwa Afrika.

*84.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha miaka mitano tangu wanichague kuwawakilisha hapa Bungeni. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

*85.* ***Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,*** mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu, na Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa ndani na nje ya Bunge wakati wote nikiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, nawatakia kila la kheri na fanaka kwenye Uchaguzi Mkuu ujao na ni matumaini yangu kuwa tutakutana tena hapa Bungeni katika kipindi kijacho.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### Makadirio ya Mapato

*86.* **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 85,103,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu kwa mchanganuo ufuatao:

**Jedwali Na 3: Makadirio ya Kukusanya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/21**

| Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2019/20 |
|---|---|
| 38 – NGOME | 22,000,000.00 |
| 39 – JKT | 61,903,000.00 |
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 |
| Jumla | 85,103,000.00 |

**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

*87.* **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,141,034,489,000.00** kwa mafungu yote matatu ambapo kati yake, **Shilingi 1,977,034,489,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 164,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na 4: Mchanganuo wa Bajeti kwa Fungu kwa Mwaka wa Fedha 2020/21**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (TZS) | Matumizi ya Maendeleo (TZS) | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|
| 38-NGOME | 1,607,164,984,000.00 | 10,000,000,000.00 | 1,617,164,984,000.00 |
| 39-JKT | 350,234,958,000.00 | 4,000,000,000.00 | 354,234,958,000.00 |
| 57-Wizara | 19,634,547,000.00 | 150,000,000,000.00 | 169,634,547,000.00 |
| **Jumla** | **1,977,034,489,000.00** | **164,000,000,000.00** | **2,141,034,489,000.00** |

**MWISHO**

*88.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.

**KIAMBATISHO NA.1**

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2015-2020 KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Serikali kupitia Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ya mwaka 2015-2020 pamoja na majukumu mengine ya Wizara. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Wizara imetekeleza Ilani ya uchaguzi ya CCM 2015 – 2020 kama ifuatavyo:

**Ibara 146 (i)** *Kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea raslimali watu na raslimali fedha kwa kadri uchumi utakavyoruhusu.*

**Utekelezaji:** Katika kipindi husika Serikali imetoa kibali cha ajira kilichowezesha kuandikisha Maafisa na Askari. Aidha, Wizara ilipatiwa Watumishi wa Umma katika kada ya Afya. Katika kutekeleza majukumu yake Mhe. Rais na Amiri Jeshi Mkuu amekuwa akitunuku Kamisheni kwa Maafisa wanaohitimu mafunzo katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli (TMA) na nje ya nchi.



*Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu akikagua gwaride la Maafisa wapya kundi la 67/19 kabla ya kuwatunuku Kamisheni katika viwanja vya Ikulu Dar es Salaam tarehe 08 Februari, 2020.*

Ili kuwajengea uwezo Maafisa na Askari wake kiutendaji katika ngazi mbalimbali, Serikali kwa kupitia Wizara imeendelea kuliimarisha Jeshi kwa kuwapatia mafunzo ya weledi Wanajeshi katika Shule na Vyuo vya Kijeshi ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya Wizara kila mwaka wa fedha kulingana na hali ya uchumi wa nchi yetu.

**Ibara 146 (ii)** *Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama*

**Utekelezaji:** Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi na Watumishi wa Umma kwa kuwapatia mishahara na posho mbalimbali kwa wakati. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha huduma za afya na tiba kwa Wanajeshi ikiwemo ununuzi wa dawa na vifaa tiba kukidhi mahitaji ya Hospitali za Jeshi ikiwa ni pamoja na utoaji huduma ya usafishaji wa figo baada ya kupata mashine za *dialysis.*

**Ibara 146 (iii)** *Kuendelea kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa Mujibu wa Sheria.*

**Utekelezaji:** Katika utekelezaji wa Ilani ya CCM, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kujenga uwezo kwa kuongeza kambi mpya. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2018/19 Jeshi la Kujenga Taifa limejenga kambi mpya ya Kikosi cha Jeshi 830 katika eneo la Mkupuka Wilaya ya Kibiti ambayo kwa sasa imeanza kuchukua vijana kwa Mujibu wa Sheria na wa kujitolea. Hata hivyo, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kujenga uwezo kwa Wakufunzi kupitia Chuo cha Uongozi cha Jeshi la Kujenga Taifa kilichopo Kimbiji na hivyo kuendelea kuweka mazingira mazuri ya mafunzo kwa vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.



*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipotembelea Mradi wa ujenzi wa bwalo kwenye Kikosi kipya cha Jeshi 830 – Kibiti, Mkoa wa Pwani tarehe 15 Machi, 2020.*

**Ibara 146 (iv)** *Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika shughuli za Ulinzi wa Amani kwenye nchi mbalimbali Duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.*

**Utekelezaji:** Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa, katika Operesheni za Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ili kuleta amani na usalama kwenye nchi zenye migogoro na machafuko. Kwa kuzingatia hayo, JWTZ limeendelea kupeleka Maafisa na Askari katika Operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi za Lebanon, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo – DRC, na Jamhuri ya Afrika ya Kati – CAR.

Aidha, Jeshi linao Maafisa Wanadhimu, Waangalizi wa Kijeshi, na Makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan, Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Vile vile, Jeshi limekuwa likishiriki katika vikao mbalimbali vya kikanda ikiwemo mikutano ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Nchi za Eneo la Maziwa Makuu.

Katika kuimarisha ushirikiano kwa Jumuiya za Kikanda na nchi rafiki, Jeshi limeshiriki mazoezi mbalimbali yafuatayo na nchi za kanda ya SADC, EAC na nchi nyingine ikiwemo:

a. **Shared Accord:** Zoezi hili lilifanyika nchini Rwanda mwezi Agosti, 2019;

b. **Ushirikiano Imara 2019:** Zoezi hili la Kituo cha Uamrishaji lilifanyika nchini Uganda Novemba, 2019; na

c. Maandalizi ya zoezi la **Beach Landing Operation**: yaliyofanyika Mapinga - Bagamoyo, kuanzia tarehe 22 Desemba, 2019 hadi 16 Januari, 2020.

Jeshi pia lilishirikiana na nchi rafiki katika masuala mbalimbali ya kiulinzi mfano katika Mwaka wa Fedha 2019/20 JWTZ lilipata msaada kutoka Serikali ya Ujerumani wa ujenzi wa Karakana ya matengenezo ya magari.

**Ibara 146 (vi)** *Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka (Cross Border Crimes) hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha haramu (money laundering), biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji wa binadamu.*

**Utekelezaji:** Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama nchini na Mataifa mengine katika kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uvuvi haramu, uharamia, biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu. Ushirikiano huu ambao umefanywa kupitia mafunzo na Operesheni mbalimbali umeliwezesha JWTZ kupata uzoefu na kujifunza mbinu mpya za kupambana na wahalifu wa makosa hayo.

**KIAMBATISHO NA.2**

**Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai 2019 Hadi Machi, 2020**

| Fungu | Matumizi Yaliyoidhinishwa | Bajeti ya Mwaka ya Fedha 2019/20 | Kiasi Kilichopokelewa hadi Machi, 2020 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 38 - NGOME | Mshahara | 1,102,392,157,000.00 | 847,622,973,405.20 | 76.89 |
| | Fedha za Chakula | 210,751,950,000.00 | 156,609,341,000.00 | 74.31 |
| | Matumizi Mengineyo | 31,503,201,000.00 | 66,954,844,374.68 | 212.53 |
| | Posho ya Msamaha wa Kodi | 62,079,600,000.00 | 46,599,700,000.00 | 75.06 |
| | Maendeleo | 6,000,000,000.00 | 2,515,468,293.00 | 41.92 |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,412,726,908,000.00** | **1,120,302,327,072.90** | **79.30** |
| | | | | |
| 39 - JKT | Mshahara | 189,923,371,000.00 | 153,604,697,996.00 | 80.00 |
| | Fedha za Chakula | 52,200,000,000.00 | 51,084,743,500.00 | 97.8 |
| | Matumizi Mengineyo | 30,419,054,000.00 | 21,535,071,497.16 | 63.0 |
| | Mafunzo ya Vijana kwa Mujibu wa Sheria | 16,000,000,000.00 | 16,000,000,000.00 | 100.0 |
| | Posho ya Msamaha wa kodi | 11,493,000,000.00 | 8,619,750,000.00 | 75.0 |
| | Maendeleo | 2,000,000,000.00 | 0 | 0.00 |
| | **Jumla ya Fungu** | **302,035,425,000.00** | **250,844,262,993.16** | **83.00** |
| | | | | |
| 57 - WIZARA | Mshahara (Wizara na Mashirika) | 10,170,965,000.00 | 6,743,468,500.00 | 66.3 |
| | Ruzuku (Mashirika na Majenerali) | 6,874,634,814.00 | 3,619,750,839.80 | 52.65 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,229,410,186.00 | 2,419,840,541.00 | 108.54 |
| | Maendeleo | 120,000,000,000.00 | 103,678,216,872.26 | 86.40 |
| | **Jumla ya Fungu** | **139,275,010,000.00** | **116,461,276,753.06** | **83.62** |
| | **JUMLA KUU** | **1,854,037,343,000.00** | **1,487,607,866,819.12** | **80.24** |

**SPIKA:** Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati wa Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama au Mjumbe kwa niaba yake, ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige nimekuona unaweza kuendelea na una dakika 20.

**MHE. ALMAS A. MAIGE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa pole za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, wewe Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwa msiba wa aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustino Mahiga, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kujadili bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Amiri Jeshi Mkuu kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi anavyowezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kibajeti Wizara hii ina jumla ya mafungu matatu yaani Fungu 38 la Ngome, Fungu 39 Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yaani Wizara. Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina bajeti ya mafungu yote matatu na matokeo ya uchambuzi yameonekana katika sehemu ya tatu na ya nne ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; kwanza ni matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, pili mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2020/2021, tatu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara

ya Mwaka wa fedha 2020/2021 na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa; Kamati ilikagua miradi mitatu inayohusu ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Kikombo Dodoma *(National Defence, Head Quarter (NDHQ),* ujenzi wa Hospitali ya Jeshi Dodoma chini ya Fungu 38 na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kikosi cha JKT Kibiti Mpuka chini ya Fungu 39. Sura halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2019/2020 imeainishwa katika ukurasa wa 4 hadi wa 7 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kamati ilijadili kwa kina taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi yote iliyokaguliwa na Kamati, katika ukaguzi huo changamoto kubwa iliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni ile ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara na vikosi vyake kuendelea kubuni mbinu mbadala za kukabiliana na changamoto hizo Kamati inaendelea kuishukuru Serikali kuendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ambayo ina tija kwa Taifa katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge wa kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 taarifa hiyo ilijumuisha maeneo makuu mawili ambayo ni mapitio ya utekelezaji wa mapato na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na uzingatiaji wa maoni ya ushauri wa kamati kuhusu bajeti hiyo kama inavyoelezwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020; uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa

mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo. Upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo yaani *other charges* fedha za mafunzo ya vijana kwa mujibu wa sheria kwa Fungu 39 yaani JKT na fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Naomba kuwasilisha mchanganuo huo kwa uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 81,104,000 kwa mafungu yote matatu. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 jumla ya shilingi 53,826,000 sawa na asilimia 66 ya makadirio yalikuwa yamekusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni pungufu ya shilingi milioni 6,293,557 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa kipindi kama hiki mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ilivyoonekana katika jedwali namba moja katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Bunge lako tukufu limekuwa likishauri Seikali kila mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Serikali. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 zimetolewa kiasi cha kuridhisha. Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 1,292,606,728,967 sawa na asilimia 69.72 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/

2020, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti ya mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu hayo, ulinganisho huo unaonekana katika Jedwali Namba 2 la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ulinganisho huo unaonekana kuwa Serikali ilizingatia ipasavyo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti kwa mfano Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 JKT ikiwa ni asilimia 16.29 ya bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na fungu hilo ni asilimia 17.43 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020. Kwa mwenendo huo Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa bajeti ya Ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na fedha zilizopatikana unaadhihirisha masuala mbalimbali kama yalivyoidhinishwa katika ukurasa wa 15 na 16 wa taarifa hii. Kutokana na uchambuzi huo Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hususan za maendeleo kwa Fungu 57 ambao tayari umepatikana asilimia 83.06 ya fedha za maendeleo hadi mwezi Februari, 2020 ni mzuri na unasaidia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa haraka fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni mbili zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 39 JKT ili kuimarisha uwezo wa jeshi hilo kuchukua vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; Kamati ilipopitia na kuchambua mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2019/2020 ilitoa ushauri katika maeneo 13 yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu bajeti hiyo. Utekelezaji wa ushauri ulitolewa na Kamati unapatikana katika ukurasa wa 17 hadi 20 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kiujumla katika utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati wa mwaka 2019/2020 Kamati inaipongeza Wizara kuwa pamoja na changamoto za kibajeti zilizojitokeza imeendelea kutumia kiwango kilichotengwa

kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa kufanywa na Wizara yanafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao bado unaendelea kutekelezwa na ule ambao haujazingatiwa ipasavyo unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021; uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu; 38, 39 na 57 inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 85,103,000. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 4.93 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mchanganuo wa lengo hilo na makusanyo na sura ya mchanganuo huo inaoneknana katika Jedwali Na. 3 na Chati Na. 3 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu lengo la kukusanya mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, Kamati inaishauri kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Kamati yalionesha kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa anayoomba kwa mafungu yote matatu ni shilingi 2,141,034,489,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,377,034,489,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 164,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(a) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeongezeka kwa shilingi 286,997,146,000 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 15.47. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake inavyovisimamia.

(b) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kimeongezeka kwa asilimia 28.13 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Fedha hizi zimezidi katika mafungu yote matatu kama inavyoonekana katika ukurasa wa 26. Kati ya shilingi bilioni 164 zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo, asilimia 6.10 ni kwa ajili ya Fungu 38 – Ngome, asilimia 2.44 ni kwa ajili ya Fungu 39 – JKT na asilimia 91.46 ni kwa ajili ya Fungu 57 la Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii na maoni yanayotolewa na Kamati yangu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kulinda mamlaka, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufatao:-

Mheshimiwa Spika, moja, Kamati inatambua juhidi kubwa za kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukusanya mapato. Kutokana na ufanisi huo wa ukusanyaji mapato, Serikali iongeze ukomo wa bajeti ya mafungu yote ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mbili, Serikali itoe fedha zinazohitajika katika ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi Kikombo, Dodoma ili ujenzi huo uendane na wakati na kuepuka kufidia bajeti gharama zitakazozidi.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iipatie fedha Wizara hii kwa ajili ya kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na yatakayotarajiwa kuchukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ione umuhimu wa kufanya ukarabati wa haraka wa nyumba za makazi ya wanajeshi kuanzia na zile ambazo zimechakaa.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali iongeze bajeti ya vijana wanaotakiwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na kuweka utaratibu utakaowezesha vijana hao kupata ujuzi na uzoefu wa kazi za kujitegemea unaotambulika baada ya mafunzo.

Mheshimiwa Spika, sita, pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali itoe kipaumbele kwa Wizara hii wakati wa kutoa fedha hizo kwenye mafungu husika.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali iyapatie fedha za kutosha Mashirika ya Nyumbu na Mzinga ili yaweze kuendeleza tafiti zake zinazoendelea na kuanzisha tafiti mpya zenye tija kwa nchi yetu kwani dalili njema zimeonekana kama vile utengenezaji wa magari ya kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya uwasilishaji wa taarifa hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi, Mbunge, kwa usirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Ramadhani Abdallah na Bi. Grace Bidia wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee taarifa hii na likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/ 2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kutoa pole za dhati kwa Mheshimiwa Rais, Dkt, John Joseph Pombe Magufuli, wewe Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwa msiba wa

aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na Mbunge mwenzetu Mhe. Balozi Dkt. Augustine Mahiga. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa leo ni Siku ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoliwezesha Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama Nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya pongezi hizo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Kudumu za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wizara ya Ulinzi na JKT ni mojawapo ya Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii nyingine zikiwa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimezipa Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia. Kufuatia jukumu hilo, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 26 Machi, 2020 ili kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa utaratibu wa Kibajeti, Wizara hii ina jumla ya Mafungu matatu (3) yafuatayo: -

i) Fungu 38- Ngome;
ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Wizara).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina Bajeti za Mafungu yote matatu na matokeo ya Uchambuzi yanaonekana katika sehemu ya Tatu na ya Nne ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne (4) zifuatazo: -

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**
**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii ikiwemo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia tarehe 12 hadi18 Machi, 2020, inayotekelezwa katika Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar.

Kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilikagua Miradi mitatu inayohusu Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – Kikombo, Dodoma (National Defence Headquarters

NDHQ), Ujenzi wa Hospitali ya Jeshi - Dodoma chini ya Fungu 38 na Mradi wa Ujenzi wa jengo la Kikosi kipya cha JKT, Kibiti – Mkupuka chini ya Fungu 39.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kupata sura halisi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, naomba kueleza utekelezaji huo kama ifuatavyo:-

**i) Mradi Na. 6103 wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi (National Defence Headquarters) – Kikombo, Dodoma**

Mradi huu ulipelekewa Shilingi **Bilioni 5** nje ya Bajeti kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu ya Makao Makuu ya Ulinzi katika eneo la Kikombo – Dodoma. Ujenzi huu kwa ujumla wake unatekelezwa na wataalam wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Hadi Kamati ilipotembelea mradi huo, maandalizi ya mambo muhimu yalikuwa yanaendelea na tayari Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeshalipa fidia jumla ya Shilingi **3,399,790,359.92** kwa wananchi 1526 waliopisha eneo kwa ajili ya kazi za ujenzi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii nzuri ya kuwalipa wananchi fidia kwa wakati na bila ya usumbufu. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kufanya hivyo kwa kila eneo lililochukuliwa na litakalochukuliwa kwa matumizi ya Umma.

**ii) Mradi Na. 6103 wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi – Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu maandalizi ya Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi, Jijini Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajenga Hospitali hiyo kwa Ushirikiano na Shirikisho la Serikali ya Ujerumani ambapo kwa sasa ipo katika hatua za maandalizi ya Ukaguzi wa eneo litakalofaa kwa ujenzi huo. Maeneo ambayo yanafanyiwa ukaguzi ni Ihumwa na Msalato.

**iii) Mradi Namba 6327 kuhusu Ujenzi wa Kikosi Kipya cha JKT 830 KJ- Mkupuka, Kibiti**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa kikosi kipya cha JKT 830 KJ – Mkupuka, Kibiti. Mradi huu unalenga kuongeza uwezo wa Serikali kuchukua vijana wengi zaidi wa kujiunga na JKT kwa mujibu wa Sheria na Kujitolea.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo Fungu 39- JKT lilipokea fedha zote jumla ya Shilingi Bilioni 6 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 661,639,679.00** kwa ajili ya ujenzi wa miondombinu mbalimbali kuwezesha uchukuaji wa vijana wengi zaidi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya mradi huu na kuwezesha kuwa na kikosi katika eneo hilo lililokuwa na changamoto za kiusalama.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Katika mwaka wa Fedha 2019/2020 Fungu 39- JKT halikupelekewa fedha zozote za maendeleo. Fedha hizo jumla ya Shilingi bilioni mbili (2) zinajumuisha Shilingi Milioni 160 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo ili kukamilisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

**Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Miradi yote iliyokaguliwa na Kamati. Katika ukaguzi huo changamoto kubwa zaidi iliyobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni ile ya ufinyu wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Wizara na Vikosi vyake kuendelea kubuni mbinu mbadala za kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali

kuendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ambayo ina tija kwa Taifa katika sekta hii.

## UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Taarifa hiyo ilijumuisha maeneo Makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti hiyo kama inavyoelezwa katika taarifa hii.

### Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha za Mafunzo ya Vijana kwa Mujibu wa Sheria kwa Fungu 39-JKT na fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Oktoba, 2019 na Januari 2020 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ilikadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi **81,104,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3) kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani,

mifugo na mazao ya shamba na kodi ya pango. Makadirio haya yalikuwa ni ongezeko la asilimia 7.54 ikilinganishwa na Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ya Shilingi **75,420,100.00**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2020, jumla ya Shilingi **53,826,000.00** sawa na asilimia 66 ya makadirio yalikuwa yamekusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni pungufu ya Shilingi **6,293,557.00** sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa kipindi kama hiki Mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa upungufu huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na Fungu 57 – Wizara, ambayo haijakusanya maduhuli kwa kipindi husika kutokana na kufungwa kwa mgahawa ambao ulikuwa ndio chanzo cha mapato ya maduhuli hayo baada ya Watumishi waliokuwa wanapata huduma katika mgahawa huo kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 hapa chini.


Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato

| FUNGU | MAKADIRIO | %YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | %YA JUMLA YA MAKUSANYO | %YA LENGO LA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| - Ngome | 20,001,000.00 | 24.66 | 11,500,000.00 | 21.37 | 57 |
| - JKT | 59,903,000.00 | 73.86 | 42,325,000.00 | 78.63 | 71 |
| - Wizara | 1,200,000.00 | 1.48 | 0 | 0 | 0 |
| **MLA** | **81,104,000.00** | **100.0** | **53,826,000.00** | **100.00** | **66** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi zaidi, Kamati ililinganisha mchango wa kila Fungu katika makadirio na kuoanisha na mchango wa kila Fungu katika makusanyo kama inavyoonekana katika chati Na. 1 hapa chini.

**Chati Na. 01:** Ulinganisho wa mchango wa kila Fungu katika Makadirio na Makusanyo ya Mapato




**Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha kuwa: -

i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 24.66 lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa asilimia 21.37 ya kiasi kilichokusanywa.

ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 73.86, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa asimia 78.63. Katika mchango wa Makusanyo, JKT imekuwa mbele katika mchango ikilinganishwa na lengo la mchango wake katika makusanyo ya mapato ya Wizara kutoka asilimia 73.86 hadi asilimia 78.63.

iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia kwa asilimia 1.48 kwenye mapato yote ya Wizara, lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 57 halikuweza kuchangia kutokana na sababu zilizoelezwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, uliisukuma Kamati kutaka kupata sababu za mwenendo huo wa makusanyo. Kamati ilibaini kuwa chanzo kikuu cha Mapato kwa Fungu 38- Ngome ni mauzo ya nyaraka za zabuni na JWTZ kuwa wakala wa ukusanyaji wa makato ya Bima zinazokatwa na Wanajeshi kutoka Kampuni mbalimbali za Bima.

Vyanzo hivyo vimepungua katika Fungu 38- Ngome na kusababisha kupungua kwa ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Aidha, Fungu 39-JKT linategemea makusanyo yanayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na mauzo ya mazao ya bustani, mifugo na mashamba yanayozalishwa na Jeshi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile, Fungu 57- Wizara linategemea mapato yatokanayo na Kodi ya pango ya Kantini kwa mtoa huduma za chakula, hata hivyo fungu hilo halikuchangia chochote kutokana na maelezo yaliyotolewa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Fungu 57 halikuweza kukusanya mapato yoyote kama ilivyoainishwa hapo juu, Kamati inapongeza juhudi za Wizara kwa kuweza kukusanya asilimia 66 ya jumla ya makadirio yaliyowekwa kwa mafugu yote matatu. Kamati ina imani kuwa kutokana na mwenendo huo, lengo la makusanyo litakuwa limefikiwa kwa kiwango kikubwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020.

### Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu limekuwa likiishauri Serikali kila Mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Serikali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa


Mwaka wa Fedha 2019/2020 zimetolewa kwa kiasi cha kuridhisha. Kamati ilibaini kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari, 2020, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi 1,292,606,728,967.11 sawa na asilimia 69.72 ya Bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa Fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 02.

Chanzo: **Randama ya Wizara 2020/2021**

Kamati ilitumia Jedwali hilo, kupata Chati Na. 02 iliyotumika miongoni mwa nyenzo za uchambuzi kama inavyoonekana hapa chini.

**Chati Na. 02: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinisha na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**




**[illegible]a ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiw[illegible]a**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia i[illegible]yo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha [illegible]i. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 - [illegible]wa ni asilimia 16.29 ya Bajeti ya Wizara na fedha zilizo[illegible]ewa na Fungu hilo ni asilimia 17.43 ya fedha zote zilizop[illegible]va na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi k[illegible]mwezi Febuari, 2020. Kwa mwenendo huu, Kamati inai[illegible]eza Serikali kutoa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome, Je[illegible]Kujenga Taifa na Wizara.

**[illegible]pika**, ulinganisho wa kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na Fedha zilizopatikana unadhihirisha masuala yafuatayo: -

i) Hadi kufikia Mwezi Febuari, 2020 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea Shilingi **1,292,606,728,967.11** sawa na asilimia 69.72 ya fedha

zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **1,189,815,508,917.11** sawa na asilimia 92.05 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **102,291,220,050.00** sawa na asilimia 7.95 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu ya asilimia 2.95 ikilinganishwa na Fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

iii) Fungu 39 - JKT halijapokea Fedha zozote za Miradi ya Maendeleo kati ya Shilingi **Bilioni 2** zilizotengwa.

iv) Fungu 38 Ngome limepokea Shilingi **2,515,468,293.00** sawa na asilimia 41.90 kati Fedha zote zilizotengwa **shilingi Bilioni 6**.

v) Fungu 57 - Wizara limepokea Shilingi **110,539,182,776.90** sawa na asilimia 79.34 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

vi) Kati ya Shilingi **102,291,220,050.00** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 97.44 ya Fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57 - Wizara na asilimia 2.56 ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome.

vii) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu, Fungu 57- Wizara lilipokea asilimia 79.34, Fungu 39- JKT lilipokea asilimia 74.59 na Fungu 38 Ngome lilipokea asilimia 67.70.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa Fedha hususan za Maendeleo kwa Fungu 57 ambalo tayari limepatiwa asilimia 83.06 ya Fedha za Maendeleo hadi Mwezi Febuari, 2020 ni mzuri na unasaidia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kamati inampongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuendelea kuimarisha vyombo vyetu vya Ulinzi na usalama.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kwa haraka Fedha za Miradi ya Maendeleo

Shilingi Bilioni Mbili (2) zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 39 – JKT ili kuimarisha uwezo wa Jeshi hilo kuchukua vijana wengi zaidi.

**Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipopitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2019/2020, ilitoa ushauri katika maeneo kumi na tatu (13) yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo.

Masuala hayo yalihusu mambo mbalimbali yakiwemo yafuatayo: -

i) Serikali kuongeza Ukomo wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kulingana na mahitaji halisi;

ii) Serikali kuona umuhimu wa kuongeza kasi ya ulipaji madeni ili itenge fedha nyingi zaidi za Miradi ya Maendeleo kwa Wizara hii;

iii) Serikali kutoa Fedha zote zilizotengwa katika Fungu 38 kwa ajili ya kugharamia mafunzo ya usalama na utambuzi;

iv) Serikali itoe fedha ziizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuboresha mfumo wa Mawasiliano salama Jeshini;

v) Serikali itoe Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Programu za Utafiti katika Mashirika ya Nyumbu na Mzinga;

vi) Serikali iendelee kutoa Fedha kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi;

vii) Serikali iongeze juhudi za kukamilisha mchakato wa Sera ya Ulinzi na;

viii) Serikali kuchukua hatua za kuhakikisha kwa wale wote waliokopa matrekta ya SUMAJKT wanalipa deni lao lote wanalodaiwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika masuala yaliyotolewa ushauri, masuala sita (6) yamezingatiwa kikamilifu, masuala matano (5) yanaendelea na hatua za utekelezaji na masuala mengine mawili (2) bado hayajazingatiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni ule wa kuongeza ukomo wa Bajeti ambapo kwa mwaka ujao wa Fedha wa 2020/2021, Serikali imeongeza Bajeti ya Wizara hii kwa asilimia 15.4 ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2019/2020. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huu na inaiomba kuendelea na utaratibu huu kwa bajeti za Wizara hii katika siku za usoni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati vile vile inaipongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dk. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutekeleza ushauri wa Kamati wa kuyachukua Madeni yaliyopo kwenye Mafungu ya Wizara hii ili yaweze kulipwa na Hazina moja kwa moja baada ya kuhakikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi Wizara ilipokuwa inawasilisha Taarifa yake kwa Kamati, Serikali ilikuwa imeshalipa Shilingi **37,434,045,727.56** ikiwa ni deni lililohakikiwa kwa Mwaka 2017/2018. Aidha Serikali iko katika mchakato wa kuhakiki madeni ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 kabla ya kufikia mwisho wa Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya ushauri unaoendelea kuzingatiwa ni ule wa kulipa fidia kwa maeneo yanayotwaliwa na Jeshi baada ya kufanyiwa tathmini, ambapo maeneo ya Ras Mshindo (Kilwa), Kilima cha Losirwai – Tanganyika Packers (Arusha), Kilima cha Ilemela (Mwanza), Makoko (Musoma), Kakonko (Kigoma) na Kikombo (Dodoma) tayari yamekwisha lipiwa fidia inayostahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendelea kulipia fidia maeneo mengine yote iliyoyatwaa kwa haraka

iwezekanavyo ili kuondoa changamoto zinazoendelea kujitokeza kwa kuchelewa kulipa fidia hizo.

**Mheshimiwa Spika, vilevile** Wizara iliiarifu Kamati kuwa inaendelea na utekelezaji wa kuboresha makaazi ya Wanajeshi lakini kwa kiwango kidogo sana kutokana na ufinyu wa bajeti. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kubuni utaratibu mzuri zaidi utakaowezesha kuboresha makaazi hayo ili kuwaondoshea Wanajeshi changamoto zinazowakabili kutokana na kuishi kwenye nyumba zisizoridhisha au nje ya Kambi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya ushauri ambao haujazingatiwa ipasavyo ni ule wa Serikali kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa Mashirika ya MZINGA na NYUMBU kwa ajili ya Program za Utafiti. Kamati iliarifiwa kuwa Kwa Mwaka 2018/2019 Serikali ilitoa asilimia 13.33 kwa Shirika la MZINGA na asilimia 8.0 kwa Shirika la NYUMBU ya Bajeti zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyapa kipaumbele mashirika hayo katika kuyapatia fedha ili yaendelee kujiimarisha na kazi zake za utafiti hususan kutokana na mwelekeo wa dunia ya sayansi na teknolojia unavyokwenda.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla, katika utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2019/2020, Kamati inaipongeza Wizara kuwa, pamoja na Changamoto za kibajeti zilizojitokeza, imeendelea kutumia kiwango kilichotengwa kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao bado unaendelea kutekelezwa na ule ambao haujazingatiwa ipasavyo unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

## UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili, 2016 na kuoanisha na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza majukumu ya msingi manne yaliyoainishwa katika Hati Idhini, Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kulingana na Dira na Dhima kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu matano likiwemo la kuendeleza utafiti na Teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu ya Wizara hii pamoja na kuwapatia Vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, Stadi za Kazi na kuwajengea Uzalendo na Umoja wa Kitaifa.


**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

4.93 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 03. Na Chati Na. 03 hapa chini: - **Shilingi 85,103,000.00.** Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 4.93 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 03. Na Chati Na. 03 hapa chini: -

**Jedwali Na. 03: Mchanganuo wa mapato**

**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**

**Chati Na.03: Sura ya mchanganuo wa lengo la makusanyo**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa asilimia 4.93 ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

ii) Fungu 38 – Ngome linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 25.85 ambapo Mwaka 2019/2020 lilitegemewa kwa asilimia 24.66

iii) Fungu 39 – JKT linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 72.74 ambapo Mwaka 2019/2020 lilitegemewa kwa asilimia 73.86

iv) Fungu 57 linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1.41 wakati Mwaka 2019/2020 lilitegemewa kwa asilimia 1.48. Hata hivyo, kiasi hicho cha Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa Mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya.

**Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Kamati yalionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni Shilingi **2,141,034,489,000.00.** Kati ya Fedha hizo, Shilingi **1,977,034,489,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **164,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020.

Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imeongezeka kwa **Shilingi 286,997,146,000** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 15.47. Kamati inaipongeza Serikali kwa

kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

b) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa asilimia 28.13 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Fedha hizi zimezidi katika Mafungu yote matatu kama ifuatavyo: -

i) Fungu 38- Ziada ni Shilingi 4,000,000,000 sawa na asilimia 66.67;

ii) Fungu 39- Ziada ni Shilingi 2,000,000,000 sawa na asilimia 100; na

iii) Fungu 57- Ziada ni Shilingi 30,000,000,000 sawa na asilimia 25.

c) Kati ya Shilingi **164,000,000,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, asilimia 6.10 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, asilimia 2.44 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 91.46 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia Randama za Mafungu matatu ya Wizara na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii na Maoni yaliyotolewa na Kamati yangu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka

wa Fedha 2020/2021 ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya kulinda Mamlaka, Maslahi na Mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa Maoni na Ushauri ufuatao: -

i) Kamati inatambua juhudi kubwa na kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Tano katika ukusanyaji wa Mapato. Kutokana na ufanisi huo wa ukusanyaji wa Mapato Serikali iongeza Ukomo wa Bajeti kwa Mafungu yote ya Wizara hii kwa kiwango cha kuweza kukabiliana na changamoto zenye umuhimu zaidi kutatuliwa katika Wizara hii.

ii) Serikali itoe fedha zinazohitajika katika Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi – Kikombo, Dodoma ili ujenzi huo uendane na wakati na kuepukana na kufidia Bajeti ya gharama zitakazozidi.

iii) Serikali iipatie Fedha Wizara hii kwa ajili ya kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na yanayotarajiwa kuchukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

iv) Serikali ione umuhimu wa kufanya ukarabati wa haraka wa nyumba za makaazi ya wanajeshi kwa kuanzia na zile ambazo zipo katika hali isiyoridhisha ili kuepuka gharama kubwa inayoweza kujitokeza ya kuzijenga upya.

v) Serikali iongeze bajeti ya vijana wanaotakiwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na Kuweka utaratibu utakaowawezesha vijana hao kupata ujuzi na uzoefu wa kazi za kujitegemea unaotambulika baada ya mafunzo yao.

vi) Pamoja na kuongezeka kwa bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Serikali itoe kipaumbele kwa Wizara hii wakati wa kutoa fedha hizo kwenye mafungu husika.

vii) Serikali iyapatie fedha za kutosha mashirika ya Nyumbu na Mzinga ili yaweze kuendeleza tafiti zake zinazoendelea na kuanzisha tafiti mpya zenye tija kwa nchi yetu kwani dalili

njema zimeanza kuonekana kama vile utengenezaji wa magari ya zimamoto.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
4. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
5. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
6. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
8. Mhe. Bonnah L. Kamoli, Mb
9. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
10. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
11. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
12. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
13. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
14. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
15. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
16. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
17. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
18. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
19. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
20. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
21. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
22. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
23. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
24. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
25. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT

Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Salum Mwinyi Rehani**, Mb**
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,**
**ULINZI NA USALAMA**
Mei, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige kwa kutupitisha katika taarifa ya Kamati vizuri kabisa. Tunawashukuru sana Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji, naomba niwatambue wageni wetu ambao

wamehudhuria hapa katika uwasilishaji wa hotuba ya Wizara hii ya Ulinzi na JKT ambapo ninao viongozi wa Jeshi wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Faraji Mnyepe, ahsante sana, karibu sana Katibu Mkuu, tunafarijika sana kuwa nawe miongoni mwetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunaye Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, ahsante sana Mkuu wa Jeshi, tunakushukuru sana kufika na kuwa na sisi leo. Hakika unapokuwa nasi tunafarijika sana, karibu sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunaye Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Yacoub Mohamed, ahsante sana Mnadhimu Mkuu wa Jeshi. *(Makofi)*

Tunaye pia Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Brigedia Jenerali Charles Mbuge, ahsante sana Ndugu Mbuge, tunakushukuru sana na karibu sana hapa mjengoni. *(Makofi)*

Pia tunaye Kamishna wa Sera na Mipango Bwana Egbert Ndauka, karibu sana Kamishna, tunakushukuru sana, karibu sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana na kwa mara nyingine niwakaribishe sana wageni wetu wote. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea na uchangiaji, na hebu atuanzie Mheshimiwa Masoud Abdallah, tuanze na *CUF* leo na wachangiaji wengine wajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* kuwa mchangiaji wa kwanza leo katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, leo tuko kumi la pili, *maghfirah,* kumi ambalo ni la kuomba kufutiwa dhambi na *Allah Subhanahu-Wataala.* Niwaombe wote walio katika kufunga basi wazidishe bidii ya kumtaja Mwenyezi Mungu atusamehe dhambi ambazo binadamu tumezitenda na ni imani kwamba *Inshallah* tutaongeza bidii, tuamke usiku tuendelee na kasi.

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu hii ni Kamati yangu na kwangu ni kuboresha tu na mambo yote ambayo yameelezwa na Msemaji wa Taarifa yetu ya Kamati ni mambo muhimu sana na kikawaida sisi hatuna mambo mengi katika mambo ya ulinzi, ni kuona kwamba hali yetu ya ulinzi na usalama inakwenda vizuri, Taifa liko salama mipaka iko salama, sisi kwa jumla yake yote.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache tu ya kuboresha boresha hapa na pale ambalo moja ilikuwa ni suala zima la Sera yetu ya Ulinzi wa Taifa. Sisi kama Kamati tumesema mara nyingi sana kwamba sera ni ya zamani, tangu mwaka 1966, karibu miaka 54 sasa na lengo letu kubwa lilikuwa ni kuboresha, kupatikana kwa sheria ambayo itajenga taswira ya jeshi sasa kubwa au dogo la kisasa na kuendana na mazingira ya dunia mabadiliko ya sayansi na teknolojia, ndiyo lengo letu, ilikuwa ndiyo lengo letu kubwa tu katika Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la Sera ya Ulinzi wa Taifa ni jambo muhimu sana. Duniani kuna mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, ni vyema sasa tuone kwamba suala hili Serikali inaweza kulifanyia kazi, inawezekana. Mchakato tangu mwaka 2006, mimi nilikuwa ndio Waziri Kivuli katika Waziri Kivuli aliyekaa muda mrefu katika Uwaziri Kivuli mimi *alhamdulillah,* nimekaa miaka kumi Waziri Kivuli, kwa hiyo ni kivuli cha muda mrefu. Nimekuwa suala hili nikilizungumza sana tu lakini bado inaonekana halijakaa vizuri. Hilo lilikuwa ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala zima la Corona, ikiwa jeshini na maeneo mengine yote ya ulinzi na usalama lazima tuzungumzie habari ya Corona. Wananchi ambao wana familia zao zenye kulinda amani kwenye misheni za kimataifa; DRC Congo na maeneo mengine, Lebanon, wanataka kufahamu hali ya wapendwa wao, familia zao huko zikoje? Maana Corona imeenea dunia nzima, wangependa kufahamu na sisi ndiyo midomo yao, ndiyo sauti zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa hebu awatoe hofu Watanzania ambao wana familia zao, ambao wako

nje ya nchi wanalinda amani, hali ya Corona kwenye jeshi lao ikoje. Tuwape taarifa ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala ambalo tumekuwa tukilizungumza sana kwenye Kamati, suala la upimzaji, kutathmini na kulipa fidia maeneo ambayo yamechukuliwa na Jeshi au kwa lugha nyingine yametwaliwa na Jeshi, maeneo ya wananchi. Ukienda kwenye Fungu 57 - Wizara, mwaka 2019/2020 tulitenga shilingi bilioni 120; ukienda kwenye Fungu 57 mwaka 2020/2021 kuna shilingi bilioni 150 lakini kwenye mwaka 2019/2020 kwenye shilingi bilioni 120 fedha karibu shilingi bilioni mia moja naa zimetolewa na hapa ndipo penye fidia, penye kupima, kutathmini na kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali tena sana kwamba fedha hizi zitolewe wananchi hawa wengine maeneo yao yalichukuliwa zamani miaka na miaka, muda mrefu umepita wanalalamika, wengine wamekufa wameacha watoto wao, watoto wao hawajui pa kuanzia. Niombe sana hizi fedha za kulipa fidia kwa maeneo ambayo yamechukuliwa au yametwaliwa na Jeshi wapewe wenyewe wananchi, hizo ndiyo sauti zao, muda umekuwa ni mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumejaribu mara hii *alhamdullilah* kule Kilwa tumepeleka fedha angalau wamebahatika, Singino - Kilwa, lakini maeneo mengi bado baadhi ya maeneo ambayo hizi fedha zimetolewa lakini naona kuna ukakasi fulani. Naomba tuongeze kasi kwa Serikali, fedha hizi wapelekewe wananchi wenyewe maeneo yaliyochukuliwa na muda umekuwa ni mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala zima la SUMA JKT. Kwenye taarifa hii wananchi wamekuwa wakifarijika sana na suala zima la SUMA JKT na hasa kile Kitengo cha Ujenzi, lakini Mheshimiwa Waziri utakapokuja kidogo tu, watu wanataka kupata faraja ni kwa kiasi gani ubora aliyonao SUMA JKT na kazi ambazo amefanya na alivyojenga nyumba nyingi wameingiza fedha kiasi gani? Hiyo wananchi wanapenda sana kwa sababu ni kama tangazo

kwamba nyumba wanazojenga SUMA JKT ni nzuri, ni safi, ni bora. Kwa hiyo ni kiasi gani cha fedha ambacho kimeingizwa hadi sasa? Wangependa kujua.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna *SUMA JKT Guard,* wale walinzi; napo vilevile ni kiasi gani ile kampuni ya ulinzi imeandika fedha kiasi gani katika shughuli zetu. Lakini kuna malalamiko hapo yametoka hapohapo kwamba kiwango cha fedha wanacholipwa wale walinzi wetu wa *SUMA JKT Guard* ambao wanafanya kazi kwenye taasisi mbalimbali, kiwango hicho bado ni kidogo, wanalipwa shilingi 190,000, hazitoshi, waongezwe, wanalalamika wale walinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila kona wanapokwenda katika maeneo mbalimbali *SUMA JKT Guard* wanalalamika, Waheshimiwa tupigieni kelele. Kwa hiyo ningeomba sana kwa sababu hii taasisi shughuli inaendelea kuwa vizuri zaidi, basi naomba tuongeze kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la mwisho, suala zima la Jeshi wakati wa uchaguzi. Sisi kwetu wakati wa uchaguzi Jeshi wanaleta masanduku ya kura baada ya kura kumalizika wanachukua masanduku. Lakini kuna kitu ningeomba msiruhusu na nashukuru sana Mkuu wa Majeshi hapa *Major General* Mabeyo upo na mwenzako yule wa JKT yupo, msiruhusu kabla ya wiki mbili au tatu ikawa kuna vifaru vinatembeatembea katika maeneo mbalimbali, wananchi wanatishika. Wananchi hawafurahi, wanajiuliza kuna nini zaidi, kwa nini kuna uchaguzi wa kiraia, lakini kunakuwa na magari au vifaru vinapita barabarani na magari yale ya *deraya* yanapita. Sasa hii mnatia hofu wananchi kwa sababu uchaguzi ni wa kiraia, hakuna vita. Waacheni wananchi, msiwatie hofu waende kwenye uchaguzi wachague wanayemtaka na kama umefanya mazuri utachaguliwa tu. Kwa hiyo mimi nafikiri nasema hili Mkuu wa Majeshi yupo.

Mheshimiwa Spika, na niseme waziwazi kwamba hili jambo msiruhusu hata kidogo kuacha magari yale yakatembea siku tano, wiki moja kabla ya uchaguzi. Si jambo jema kidogo tafsiri inakuwa ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Masoud. Lakini si mazoezi ya kawaida tu ya askari wanapitapita kidogo, wanayoosha misuli, ahsante sana Mheshimiwa Masoud. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Maryam Msabaha yupo? Ahsante, karibu uchangie na utafuatiwa na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha nikiwa mzima wa afya, si kwa ujanja wangu ila ni kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu na tuko kwenye kumi la pli, kumi la *maghfira,* Mwenyezi Mungu atufanyie wepesi kila penye uzito, na wewe pia na Bunge lako lote Mungu atuondoshee maradhi kwa sababu kuna watu wanatuombea maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, niwaombee ndugu zangu, viongozi wenzangu ambao tulikuwa nao humu Bungeni lakini Mwenyezi Mungu amewapenda, wametangulia mbele ya haki, akawaswame waliyoyafanya kwa siri kwa kwa dhahiri na akawape pepo pamoja na viongozi wote waliotangulia kwa maradhi mbalimbali. Siyo kila mgonjwa anayekufa anakufa kwa Corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niipongeze pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kudhibiti maradhi ya Corona, tumeona jitihada za Serikali na Serikali ya Muungano pia nao wanahangaika wanadhibiti haya maradhi ya Corona na namna wananchi wanavyopewa elimu, na hizi elimu pia wazingatie namna ya kujikinga na haya maradhi ya Corona.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwanza na Kamati pia nimeona wameeleza vizuri sana na niwapongeze Kamati ya Ulinzi, wameeleza mambo muhimu sana. Kulikuwa

na hili suala la Nyumbu na hii Nyumbu kwa kweli ni sehemu ya viwanda ambavyo ni nyeti na kuna vitu vinatengenezwa vya muhimu sana katika Nyumbu, lakini sasa fedha zinakuwa hazipelekwi kwa wakati. Sasa niombe Serikali pale pesa zinavyotengwa kwenye Wizara hii zipelekwe kwa wakati ili zile changamoto ambazo zimo kule ndani ya hivi viwanda vya kutengeneza kwa sababu kule pia kuna maghala ya silaha ambayo wanakuwa wanatengeza silaha na wao sasa wapate malighafi ya kutengenezea hivi vitu wanavyovihitaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu makazi ya wanajeshi. Tumeona mvua zilivyonyesha, kwa sababu makazi mengi ya wanajeshi yalikuwa ni ya tangu enzi za mkoloni, kwa hiyo, mvua kama kwa mfano yale makazi ya Keko pia unaweza kuyashuhudia pale si rafiki sana sambamba na eneo langu ninalotoka la Migombani, mvua hizi zimenyesha kwa kweli, hali sio rafiki sana. Niombe basi Serikali iangalie makazi ya wanajeshi angalau watenge sasa hiyo bajeti na ikipitishwa kwenye Wizara ya Fedha iangaliwe na haya makazi pia yanaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, lingine kulikuwa na yale maduka ambayo yalikuwa yanasaidia wanajeshi yaliondoshwa, tukaambiwa kama maduka yale vile vifaa ambavyo labda walikuwa wanapata kwa bei ya punguzo fedha zile wangeweza kurejeshewa wakapata angalau kujikimu na kufanya mahitaji mengine, lakini sasa fedha hizi hazitoki kwa wakati na zimekuwa pia wanapata mtihani kidogo kwa sababu, wao si watu wa kugoma ni watu wa kufanya kazi. Sasa kama ni watu wa kufanya kazi wao hawajui kulalamika, kwa hiyo, nalo Serikali pia iwe inaangalia mahitaji yao kwa umuhimu sana ili zipelekwe kwa wakati muafaka kama ni kitu wameahidiwa basi kilepelekwe kwa sababu yale maduka ambayo walikuwa wanapata angalau kwenda kujikimu kununua vitu vidogo vidogo na punguzo kidogo hayapo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia pia bado kuna vimitindo viko huko mitaani kwa watu ambao sio waadilifu, bado kuna wengine wanatumia sare za wanajeshi kuvaa na

wengine kufanya mambo ya uhalifu. Kwa hiyo, niombe kitengo husika kifanye uhakiki hawa ambao wanajihusisha kuvaa nguo ambazo na wakati mwingine kutumia kama nembo ya wanajeshi kwenda kufanya mambo ya uhalifu nao wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, ukija pia kuna wanawake ambao kwa kweli ni wazuri sana na ni watendaji wazuri sana katika Jeshi la Jamhuri ya Muungano, Jeshi la Kujenga Taifa, Maafisa wa Jeshi. Sasa hawa wanawake nao pia waongezwe madaraja wapandishwe madaraja, tusiwe tunaona tu wanaume na wanawake pia nao wale wanaofanya vizuri. Hata kwenye Sherehe za Mapinduzi uliona wanawake namna gani walifanya vizuri sana pale, kwa hiyo, tuangalie namna gani hawa wanawake nao kama ni wa kupandishwa vyeo nao wapandishwe vyeo kwa sababu sasa hivi sio wanaume tu ambao wako Jeshini pia na wanawake nao wanafanya vizuri sana Jeshini.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya wastaafu; wastaafu wanavyostaafu kwa kweli kuna kitu ambacho sasa hivi wanasema wastaafu wengi wa Jeshi wamekuwa waganga wa kienyeji. Hapana, niiombe Serikali kwa kweli wastaafu hawa waangalie *pension* zao wazipeleke kwa wakati na zile stahiki zao pia wawalipe kwa wakati ili nao wapate kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, na lingine nilikuwa naomba pia wanajeshi wanavyokuwa kazini Serikali pia iangalie sasa namna gani ya kumkopesha kila mwanajeshi angalao apate nyumba uraiani wanavyotoka makambini wasiende tena kukaa kwenye nyumba za kupanga, ili warudi sasa nao wakae na makazi yao na familia zao, kwa sababu sio vizuri wanajeshi wakishastaafu wakirudi kule mitaani kwenda tena kuhangaikahangaika kwenye masuala ya kukodi vinyumba, haipendezi kwa kweli. Sasa Serikali iangalie ni namna gani kuweka mikakati maalum kwa ajili ya kuwakopesha wanajeshi, kila mwanajeshi apate nyumba na hata angalau apate na chombo chake cha usafiri ili kwa sababu mazingira

anayorudi mtaani alikuwa kwenye mazingira ya kambini asije akapata matatizo kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu hawa vijana. Vijana wengi wanavyokwenda huko JKT wanategemea kama Serikali iwaajiri, lakini niwaombe vijana wengi wanavyokwenda JKT wakirudi basi wajiajiri wenyewe na Serikali iangalie namna gani ya kuajiri hawa vijana wasingoje ajira Serikalini kwa sababu wanavyokwenda kule wanaenda sio wote, tuseme tena wote watapata ajira, lakini wale sasa ambao watakaopata kule na yale mafunzo wanayopata kule na Serikali nayo iangalie namnba gani ya kusaidia hawa vijana ambao watabaki mitaani ili wasiingie kwenye masuala ya uhalifu ili nao wapate kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tuna suala la uchaguzi; niombe Serikali iangalie kwa makini sana wanajeshi, hasa ambao wako mipakani kwa sababu sasa hivi ndio maadui wanapata kujipenyesha na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Maryam, kengele ya pili.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakupongeza sana Mheshimiwa Maryam kwa kuendelea kufanya kazi zako na majukumu yako ya Kibunge. Tuko pamoja tunakutia moyo sana.

Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani. Mheshimiwa Nahodha tafadhali.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, dunia inapita katika kipindi kigumu sana. Sisi Watanzania tunapaswa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujalia Amiri Jeshi Mkuu jasiri hasa katika kipindi hiki

tulichonacho. Mtakumbuka mwaka 1978 wakati Taifa letu lilipokuwa linajiandaa kupambana na nduli Idd Amin, Baba wa Taifa alisema maneno yafuatayo na ni vizuri tukayatafakari; “Nia ya kumpiga tunayo, uwezo wa kumpiga tunao na sababu ya kumpiga tunayo.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia inatuonesha kwamba viongozi wote walioshinda vita vigumu ni wale wenye sifa tatu, ya kwanza maono - uwezo wa kuona mambo ambayo watu wa kawaida hawayaoni; ujasiri - uwezo wa kusema ukweli juu ya hatari iliyoko mbele yetu, lakini bila ya kuwakatisha watu tamaa na tatu kutoa matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnapokuwa kwenye vita kama tulivyo sisi hivi sasa kazi ya kiongozi si kuwatia watu hofu, bali kazi ya kiongozi kuwapa watu matumaini. Baba wa Taifa alifanya hivyo, Rais Magufuli anafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Rais wa Marekani wa 32 Marehemu Franklin Rosevelt aliwahi kusema maneno yafuatayo, nanukuu; “Taifa letu kubwa litashinda kama lilivyoshinda kwenye mapambano huko nyuma. Jambo tunalopaswa kuliogopa zaidi ni hofu.” Narudia, “Jambo tunalopaswa kuliogopa zaidi ni hofu.”

Mheshimiwa Spika, Rais wetu kila anapopata nafasi ya kuzungumza na Wananchi juu ya janga lililoko mbele yetu amekuwa akitueleza kwamba, ni kweli ugonjwa wa corona ni hatari, unauwa, lakini tunapaswa kuchukua tahadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tukabiliane vyema na vita hii ya corona napenda kushauri mambo mawili yafuatayo kwa Serikali; la kwanza, tulipatie Jeshi la Wananchi wa Tanzania fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya utafiti wa maradhi makubwa ya binadamu pamoja na maradhi haya ya Corona. Ninasema hivyo kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba mataifa makubwa yenye uwezo yanatumia majeshi yao kama ni kitovu cha kufanya utafiti mkubwa na sisi haitakuwa dhambi tukilifanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania linatakiwa kufanya utafiti maalum kuhusiana na masuala mbalimbali ya *micro biology.* Ukisikiliza kwa makini mjadala na malumbano yanayoendelea kati ya mataifa makubwa utabaini kuna jambo ambalo limefanywa, lakini hatulifahamu vizuri juu ya nini hasa chanzo cha maradhi ya Corona. Kama siku za nyuma mataifa makubwa yaliwahi kutumia silaha za kemikali kuangamiza watu, haitashangaza siku zijazo mataifa makubwa yakatumia silaha za kibaiolojia ndio maana ninasema Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania lifanye utafiti juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho; ugonjwa wa corona unatupa tafakari juu ya mambo mawili makubwa, la kwanza linatupa nafasi ya kutafakari juu ya ukuu na uwezo wa Mwenyezi Mungu, linalomshinda binadamu kwa Mwenyezi Mungu inawezekana. Nakubaliana sana na kauli ya Mheshimiwa Rais wetu tumtangulize Mungu katika kila jambo. Nasema hivi kwa sababu hata hao wanasayansi tunaowategemea sana tunasahau tu kwamba na wao wameumbwa na Mwenyezi Mungu na huo uwezo unatokana na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa namna Rais wetu anavyosimamia juu ya suala hili la Corona inatudhihirishia ulimwengu kwamba Waafrika wana uwezo mkubwa sana wa kufikiri na wa kutenda. Sasa Waafrika tuitumie nafasi hii kufanya mambo makubwa na ninafikiri tunaweza. Nalisema hili kwa sababu ukiwa na kiongozi sahihi anayefanya maamuzi sahihi kwa wakati sahihi kama anavyofanya Rais wetu, bila ya shaka makubwa yatakuwa madogo, bila ya shaka tunamuomba Mwenyezi Mungu tushinde vita hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. Ahsante sana kwa mchango wako mzuri.

Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwanza kupata na mimi nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini nilitaka kuchukua fursa hii vilevile kukushukuru wewe kwa kuniamini na kunikabidhi kijiti cha kuiongoza Wizara hii ambayo mwanzoni nilidhani kwamba sitaweza kusimamia na kuiongoza Wizara hii ya Ulinzi kwa sababu, sikutokea kwenye fani hizo, lakini nikushukuru sana ushauri, miongozo na maelekezo na ushirikiano ambao nimeupata kwa kiasi kikubwa nimemudu kuweza kuisimamia Wizara hii na nimefikisha lengo ambalo nimelikusudia na leo hii tumefikia kuwasilisha bajeti hii ya mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana Waziri wa Wizara, Katibu Mkuu na Makamanda mbalimbali akiwemo Kamanda Mkuu wa Majeshi kwa ushirikiano vilevile na maelekezo katika shughuli mbalimbali za kijeshi, lakini hata kunisaidia sasa kuniongoza jinsi ya kupokea zile saluti za kijeshi, sasa hivi nimekuwa naweza vizuri sana kuzipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Wizara na Serikali mambo matatu muhimu katika eneo hili; la kwanza, katika Fungu lile la Ngome na Nyumbu pana fursa kubwa ya Jeshi kuweza kuzalisha na kuiongezea kipato nchi hii kama tutaweza kutumia rasilimali ya mawazo na utaalamu waliokuwanao wanajeshi wetu katika eneo lile. Si tu katika eneo la ulinzi peke yake, lakini eneo lile ni sehemu mojawapo ambapo tunaweza kuanzisha vyanzo vya viwanda mbalimbali kwa uwezo, lakini na muelekeo waliokuwanao.

Mheshimiwa Spika, suala kwamba kupanga ni kuchagua, kati ya mambo ambayo wanayapanga pale Wizarani tunataka tuione sasa Nyumbu inafanya tafiti za kuweza kutumia rasilimali ya chuma tulichonacho Tanzania, badala ya kukiuza kikiwa *raw* tuuze *products.* Na Nyumbu ni eneo ambalo tunaweza tukafanya uhandisi huo, zikatengenezwa aina mbalimbali za mashine au chuma

kilichokuwa kimeshagandishwa sasa kwa ajili ya kuzalisha mashine, mitambo na vitu mbalimbali na ni sehemu moja ambayo sisi wenyewe tutakuwa tunaweza kuchimba yale madini, lakini tukaweza kuyatumia sasa kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali zinazotokana na chuma kile.

Mheshimiwa Spika, la pili; eneo hilo hilo limeonesha muelekeo mzuri sasa wa kuweza kukarabati, lakini na kutengeneza magari. Kumekuwa na ubunifu mwingi na wameonesha uwezo sasa wa kuweza kuzalisha magari ambayo hayana tofauti na yale ambayo tunayaagiza China au Marekani au sehemu nyingine. Kinachohitajika ni kujengewa uwezo, lakini na uthubutu sasa wa kusema na sisi tunaanzisha viwanda vya aina kama hiyo ili kuweza kupunguza sasa mzigo wa kuagiza bidhaa, lakini na sisi tuweze kupata fursa ya kuuza bidhaa zetu katika maeneo mbalimbali haya ya *SADC* na kwingineko duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu tujenge nguvu kwenye tafiti za bidhaa mbalimbali ambazo tutaweza kuzifanya pale katika maeneo ya Ngome na Nyumbu ambapo kwa kweli baada ya kuona shughuli na uwezo wa wale watu waliokuweko pale zile rasilimali bado hatujazitumia ipasavyo. Wana uwezo mkubwa na wako tayari kuweza kuonesha kile walichonacho kichwani kwa ajili ya kuitenga Tanzania hii kiviwanda zaidi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili Wizara kupitia Serikali imelipa fidia eneo la Kilwa ambapo Jeshi lina maono ya kuwa na bandari pale, *navigation* gati. Ushauri wangu, ile bandari ni muhimu sana. Muhimu kwa sababu kwanza hatujawa na bandari maalum kama *navigation* gati, lakini sehemu mojawapo ya kuanzisha karakana kwa ajili ya ukarabati wa meli mbalimbali katika eneo lile na tatu, pale mahali tunaweza tukapatumia kwa sababu ndiyo penye *depths* kubwa Tanzania ya maji. Tukaweza kupatumia kwa ajili ya ufungaji gati wa meli kubwa ambazo zinashindwa wakati mwingine kufunga gati katika maeneo yetu mbalimbali na kufaulisha kwenye meli nyingine.

Kwa hiyo fursa iliyokuweko pale kiuchumi ni kubwa sana, lakini hata lile wazo la meli za uvuvi pale ndiyo mahali ambapo tunaweza kufanya *inspection* na kuweza kupakia mabaharia wakaweza kwenda kuvua katika eneo letu la uvuvi wa Bahari Kuu, mi mahali muhimu. Niombe sasa tusiishie tu kulipa fidia pale, sasa tuanze mkakati wa kupatumia sasa pale kwa kupajenga miundombinu ambayo itaweza kuzalisha kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la tatu wenzetu hapa wametoa mawazo mbalimbali juu ya vijana wetu wa Jeshi ambao wanakwenda kujitolea lakini tumeanza kushauri vile vile hata kwenye Kamati. Tunahitaji kuona sasa mchango wa vijana wale wanaokwenda kujitolea, tupate ile *outcome* na sio kwamba Serikali inakwenda kule baada ya kujitolea wale wanachangiwa wao. Tuliomba Wizara iandae mpango mkakati wa uzalishaji kwa vijana ambao wanakwenda JKT na wakitoka pale sasa watoke na *certificate* za uzalishaji bidhaa mbalimbali zikiwemo za kilimo ili kuondoa ile dhana ya kwamba nakwenda JKT ili niweze kupata kazi. Imeshaelezwa hapa, JKT si sehemu sahihi ya kusema kwamba mimi nakwenda kule lazima niwe mwanajeshi, unaweza kuwa mtu mwingine yeyote na ukawa na fani kubwa zaidi kuliko wale ambao walikuwa wamekwenda kusoma katika vyuo vingine.

Kwa hiyo, tunachotaka sasa hivi, tuone kwamba JKT inafanya *restructuring* ya uendeshaji wake na kujenga muelekeo sasa wa kuona kwamba inaleta matunda na wale watu wakienda pale kila aliyetoka anakuwa na nyenzo ya kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine tuliliomba kwamba ndani ya JKT kuweko na kifungu maalum ambacho kitawawezesha baadhi ya wale vijana waliotoka pale mwenye ufundi aondoke pale na *tool* ambayo ataweza kwenda kufanyia kazi katika shughuli zake. Lakini mwenye kupata fani nyingine zozote zile awe na nyenzo akiondoka pale basi aende akaanze kujitegemea na ni sehemu ambayo itaweza kusaidia kujenga uzalendo thabiti zaidi ambapo kila

mmoja akiondoka pale JKT anakuwa ana kitu ambacho anakitegemea kuliko kusema nilishaondoka JKT nikatafute ajira katika sehemu nyingine.

Kwa hiyo niombe kwamba JKT ijifanyie *restructuring* kubwa kwenye suala la utaalam wa kilimo na mifugo, kwenye suala la uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za viwandani ili kuweza kufanya vijana wetu waweze kuwa na sura sasa ya kujitegemea wenyewe zaidi kuliko sura ya kutegemea kwamba lazima aajiriwe kwa sababu Serikali ndiyo inajukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nikushukuru sana na mimi naunga mkono hoja asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mwenyekiti wa Kamati. Tunakushukuru sana kwa kuongoza Kamati hii nyeti kwa kipindi chote ambacho imekuwa chini ya uongozi wako. Ubarikiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli nimeshakutaja na Mheshimiwa Munde Tambwe kama yupo atafuatia.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai mpaka dakika hii, tunasema ahsante sana. Kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna alivyowaondoa hofu wananchi na kuhakikisha kwamba wananchi wasiweze baadaye pengine kuweza kupata shida au vifo kutokana na hofu kwa sababu kama walivyoeleza wenzangu kwamba hofu inaua zaidi kuliko ugonjwa wenyewe. Kwa hiyo, nampongeza sana, amefanya jambo la maana sana na wananchi wamepata imani. Tuwaombe waendelee kufuata taratibu zake kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais namna ya

kujikinga na corona kama wanavyoeleza Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili tuweze kuondokana na janga hili la Corona katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimepongeze sana Waziri wa Ulinzi kwa namna anavyofanya kazi yake, amekuwa ni Waziri ambaye ni mnyenyekevu na tumekuwa tukishirikiana vizuri sana kwenye Kamati, kwa hiyo, kwa kweli ni Waziri wa kuigwa mfano, Kamati ikitoa maelekezo amekuwa akiyafanyia kazi vizuri sana na Mheshimiwa Waziri huyu hajawahi kosa kwenye ziara tulizopita kukagua miradi, tumekuwa naye akipokea ushauri mbalimbali na kuhakikisha kwamba yale tuliyoshauri yanaweza kutekelezwa. Kwa hiyo, ni Waziri wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Katibu Mkuu aliyestaafu na huyu aliyeingia. Nimpongeze Mkuu wa Majeshi kwa namna wanavyofanya kazi nzuri sana. Sisi wananchi tunalala, lakini wao usiku na mchana wanafanya kazi za kuhakikisha kwamba nchi inabaki kuwa salama na ndiyo maana imeendelea kuwa nchi ya amani, lakini nchi pia yenye utulivu mkubwa. Tunawashukuru sana wapiganaji wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoshauriwa na wenzangu waliotangulia kuhusu mambo yanayohusu fidia, ni kweli kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa sana huko nyuma ulipaji wa fidia. Lakini tunaipongeza Serikali kuanzia awamu hii imeweza kuendelea kulipa fidia kwenye maeneo ambayo Jeshi lilikuwa limetwaa kama walivyoeleza kwenye maeneo kama ya Kilwa na maeneo mengine limeweza kutoa fidia. Sasa kuna maeneo mengi yametolewa kwa mfano hapa Dodoma kwa sasa hivi, tuiombe sana Serikali ilipe fidia mapema maana ukichelewa kulipa fidia watu wanaweza wakaanza kuvamia, lakini sio tu kulipa fidia, tuiombe Serikali iweze kupima haya maeneo yote, yawe na hatimiliki ili baadae kutokana na ongezeko la watu hapa Dodoma na maeneo mengine ili wasiweze kuvamia haya majeshi na wakaingia mgogoro na Jeshi kama inavyotokea maeneo mengine. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yetu ya Chama cha

Mapinduzi iweze kulipa fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa ili mwisho wake tuondoe migogoro kati ya wananchi na Jeshi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wameeleza wenzangu vizuri sana kuhusu mashirika haya Nyumbu na Mzinga. Hili shirika linafanya kazi kubwa sana za utafiti, lakini katika taarifa imeelezwa kwamba pia wamefanya utafiti wa kuwa na gari la zimamoto, kwa hiyo ni jambo zuri sana. Sasa tuliwezeshe, Serikali itoe fedha za kutosha kuweza kuyawezesha haya mashirika mawili, Mzinga na Nyumbu ili yaweze sasa kufanya tafiti kubwa zaidi na baadaye kutoka kwenye tafiti sasa tuweze kuhama kwenda kwenye uzalishaji maana yake tufanye utafiti lakini baadaye tuanze kuzalisha bidhaa za magari, mbalimbali na kadhalika ili sasa tuweze kuwa na uwezo wa kujitegemea badala ya kutegemea kuagiza hizo bidhaa kama magari, silaha pengine kuagiza nchi za nje na sisi tufike siku moja tuwe na uwezo wa kutengeneza silaha hapa hapa nchini, tuweze kutengeneza vifaru, bunduki, na bidhaa nyingine ili tusitegemee nchi nyingine, maana unapotegemea nchi nyingine kwa silaha maana yake huwezi kujua, mtu anaweza akakupatia silaha ambayo uwezo wake ni mdogo, lakini inavyotokea pengine vita, hatuombei Tanzania itokee vita, kwa hiyo unaweza ukakuta adui akakushinda kwa sababu hujui teknolojia ya hiyo silaha ambayo imetengenezwa. Lakini tukitengeneza wenyewe itakuwa vizuri zaidi na usiri unakuwa mkubwa wa silaha zetu ambazo tumetengeneza na hatimae tutakuwa tunaweza kujiamini pale inapotokea shida.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumeeleza kwenye Kamati juu ya vijana hawa wanaoingia JKT. Tuiombe Serikali iongeze bajeti kwenye upande wa vijana wanaoingia JKT ili vijana wengi waweze kupata mafunzo ya JKT kwa sababu mafunzo haya yanaendana pia na kuwafundisha vijana wawe wazalendo. Tunaona sasa hivi dunia au nchi yetu vijana wengi wanakosa uzalendo, lakini kumbe wengi wakipita kwenye JKT basi watapata uzalendo. Lakini pamoja na hiyo pia watapata mafunzo/ujuzi mbalimbali kama ilivyoeleza watapata ujuzi wa kilimo, ufugaji na ufundi umeme. Basi wakirudi kwenye maeneo yao waweze kutumia huu ujuzi

na hatimaye waweze kuwa na kipato kwa sababu ilivyo sasa hivi wanaporudi kwa mfano wale vijana wanaomaliza *form four* wengi wanakuwa hawajaiva vizuri. Kwa hiyo, tukawawezesha lakini pia wanakosa mitaji. Tukiwawezesha kama ilivyoelezwa kwamba tukiwawezesha wakapata ujuzi lakini pia wakapata chochote cha kuweza kwenda kuanzia kama mtaji, kitawawezesha hawa vijana wetu waweze kujitegemea kuliko kutegemea ajira zile za Serikalini.

Kwa hiyo niiombe sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, iwawezeshe hawa vijana waweze kurudi wakiwa na ujuzi na hatimae basi waweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hongoli, tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Munde Tambwe, kama hayupo, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuweza kufika katika siku hii ya leo tukiwa katika hali ya uzima na afya zetu zikiwa zinaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nikupongeze wewe mwenyewe kwa usimamizi mzuri, mwanana katika kuliongoza Bunge lako tukufu. Mimi muislamu, kwa mujibu wa sheria ya dini ya kiislamu, kiongozi ni mtu ambaye anaonesha njia, ndiyo kiongozi na sifa bora za kiongozi, miongoni mwao ili uwe kiongozi bora basi *confidence.*

Kwa hiyo, wewe unaliongoza vyema Bunge lako hili tukufu, Mwenyezi Mungu aendelee kukuongoza hivyo hivyo. Kama nilivyosema, kiongozi anaonesha njia, tuko katika kipindi kigumu sana na kiongozi bora unamjua pale ambapo mnapata tatizo. Leo hii kuna mtu anasema watu wasiingie

Bungeni, maana yake huyo sio kiongozi bora na hafai hata kuchaguliwa kipindi kinachofuata! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunazungumzia Wizara ya Ulinzi, sheria za Jeshi, askari akikimbia vita wanampiga risasi! Maana yake huyo hafai! Leo hii tuko katika vita hii ya Corona *at the same time* wananchi wanalilia wanataka maji, afya, hizo bajeti tutazipitishaje kama tuseme tu tuondoke hapa Bungeni? Sikupongezi kwa unafiki, ninakupongeza kutoka ndani ya nafsi yangu na kama wana-CCM na wananchi wako wangekuwa wannaielewa mimi ningewaombea wakuache tu na hapa Bungeni Uspika ujao uachwe bila kupingwa wewe ni kiongozi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais. Nimesema kiongozi mzuri unamjua wakati ule mnapopata matatizo. Dunia leo ukimuangalia Rais wa Ufaransa, analia hadharani kabisa. Leo Trump na vile alivyo, Trump mwenyewe amefikia *stage* analia, Trump mwenyewe! Leo hii Mheshimiwa Magufuli ndiyo maana nasema ili uwe kiongozi bora miongoni mwa sifa hizo ni *confidence,* uwezo wa kutoa maamuzi. Mheshimiwa Rais ameliongoza vyema Taifa letu, ametoa mwanga, ameonesha njia, ameonesha muelekeo. Tunaendelea kumuombea na mimi niliwahi kusema hata pale Arusha, ili mimi nikukubali uwe kiongozi katika nchi hii, *confidence.* Hii ni muhimu sana, sio kila kiongozi ana uwezo, ana *confidence* ya kuweza kutoa maamuzi kama haya.

Kwa hiyo, niseme nampongeza sana Dkt. Ali Mohammed Shein na Balozi Seif Ali Iddi kwa pamoja kwa namna ambavyo wanaliongoza Taifa letu. Kwa namna ambavyo wote kwa pamoja, Dkt. Shein, Mheshimiwa Magufuli, Balozi Seif na Mheshimiwa Waziri Mkuu, namna ambavyo wanaliongoza Taifa lakini pia namna wanavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii anayetoka nje kuja Tanzania akifika Ubungo anapotea, leo hii! Mimi nilishawahi kupotea

pale kwangu Mbezi pale. Nilitoka tu Bungeni hapa miezi miwili nilikuwa sijaenda nikapotea, badala ya kushuka pale Mbezi kwa Msuguri, nikaenda mbele zaidi, mabadiliko yaliyokuweko ndani ya Tanzania, maendeleo yaliyokuweko ndani ya Tanzania. Ukienda Zanzibar hali kadhalika ndiyo hivyo hivyo Zanzibar na huku Bara kunatofautiana kidogo. Huku Mheshimiwa Rais uzuri wake hasa anayeharibu, anamtumbua! Wenzangu hili Zanzibar halifanyiki sana, nampongeza sana Dkt. Shein kwa kutumbua hata yule Waziri wa Fedha ambaye aliharibu pale.

Kwa hiyo, Rais ajaye wa Zanzibar kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu aweze kufanya hili, wezi Zanzibar wapo, mafisadi wapo na tunawafahamu. Kwa hiyo, nimetoa sifa hizo lakini *weakness,* maana sisi ni binadamu, kila mmoja ana mapungufu! Kwa hiyo, hili Rais ajaye aweze kulirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika Wizara ya Ulinzi, ninampongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, kwa kweli ukimuangalia Dkt. Hussein ni mtu ambaye ana *vision* na *mission,* ni mtu ambaye unajua Mheshimiwa Waziri ukiiangalia Wizara ya Ulinzi, uendeshwaji wake unahitaji mtu wa namna gani kwa *nature* ya Wizara yenyewe, inahitaji mtu mtulivu, mtu mwenye hekima na busara, vinginevyo Wizara ile Mkuu wa Majeshi angepigana ngumi na Waziri wa Ulinzi. Ninawaambia ukweli.

Kwa hiyo, Dkt. Hussein ameiongoza vyema, ametulia na kwa ukweli Jeshi wanafanya kazi vizuri sana, hongereni sana. Maana mimi kama ingekuwa kuna uwezo wa kusema kwamba wapewe vyeo Jeshi, basi ningesema vyote wote! Wanafanya kazi nzuri sana. Hongereni sana Mkuu wa Majeshi wa Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ukifuatiwa na makamanda wako. *Realist* wanasema wataalam hao, nchi yoyote ile, kitu muhimu ni *power!* Bila ya *power* huwezi kufanya chochote, bila ya kuwa na *power,* huwezi hata ku-*protect* hizo *interest of the state* maana *interest of the state* ni *peace and security.* *(Makofi)*

Sasa niwaombe Wizara ya Fedha tuwape fedha kwa wakati na za kutosha Jeshi la Ulinzi la Wannachi wa Tanzania. Mkifanya hivyo na mnafanya, lakini mkifanya hivyo basi ile *power* ninayoizungumza itaimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu leo ina amani, mipaka yetu iko salama. Niwaombe wenzangu wa Wizara ya Fedha kama nilivyowaambia, hakikisheni fedha zinakwenda kwa wakati ili wapate kununua vifaa vya kutosha kwa mfano, *radar. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda hapa kikosi cha *radar* hiki hapa nazungumza kwa sababu mimi mwenyewe nimetokea jeshini.Kikosi cha *Radar* hiki hapa wana upungufu wa vifaa, kwa hiyo nimeona niseme sitazungumza sana lakini najua *in and out* ndani ya jeshi kwa sababu familia yangu yote imo ndani ya Jeshi. Kwa hiyo, niwaombe sana wenzangu tufanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza JKT wanafanya kazi vizuri, sasa niwaombe JKT wawasaidie JKU, waimarishe uchumi wa Zanzibar. Wataimarishaje? Isiwe kama vile wanavyokwenda, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakishirikiana JKT na JKU hata kuwapatia mashamba huku, vifaa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafute watalima wataimarisha uchumi na kufikia *stage* ya hata askari wao kuwalipa wao wenyewe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa malizia sasa.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema katika kipindi changu cha miaka kumi nimejifunza mengi ndani ya Bunge hili. Ninakushukuru sana kwa busara zako, kunilea mpaka hapa nilipofikia, tutaonana *Inshallah* miaka mingine kwa wale watakaokuja Zanzibar inawezekana tukakutana Zanzibar maana sisi wengine

hatutagombea tena, inawezekana tusigombee tena kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sadifa, tulikuongezea dakika kwa sababu wewe mwenyewe askari, lakini umenifurahisha kusema familia karibu yote ipo jeshini, hufanani na wale Wanyamwezi wale watani zangu wengine unakuta ukoo mzima hata sungusungu hakuna hata mmoja. *(Kicheko)*

Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi. Mheshimiwa Masele tafadhali, Mbunge wa Mbogwe.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote duniani ambayo imefanikiwa kiuchumi, kisiasa na kijamii ni lazima iwe na jeshi lenye nguvu. Nazungumza haya nikiwa nina uhakika kabisa ya kwamba kila mmoja wetu anajua hakika kuwa kwamba mataifa yenye nguvu kama Marekani yana uchumi imara, viangalie na vyombo vyake vya ulinzi na usalama vilivyo na nguvu. Iangalie Urusi ambayo hapo zamani ilikuwa *Soviet Union* iangalie Uchina na jeshi lake la *People's Liberation Army,* majeshi yake ya anga, ardhini na majini utajua hakika ya kwamba vyombo hivi ni vya msingi sana katika Taifa lolote.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yetu hii ambayo sasa tunaijenga ni Tanzania mpya ambayo inakwenda kuwa na uchumi wa kati na uchumi ulioendelea na kwa maana hiyo tunahitaji kuwa na jeshi imara na lenye uwezo wa kuweza kuyalinda haya mafanikio ambayo tunayatekeleza. Nchi yetu imejiingiza katika utaratibu wa kujenga uchumi wa kisasa,

tuna reli ya kisasa, Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo litaendelea kuzalisha umeme ambao utakuja kuitengeneza Tanzania kuwa ni nchi ya viwanda na kwa ajili hiyo ninaomba Serikali pia iwekeze kikamilifu katika jeshi. Jeshi letu hili liwe na uwezo wa kuweza kuanzisha au kukaribisha makampuni kutoka nchi rafiki yaje hapa nchini yaweze kuwekeza katika nyanja zote za Jeshi la Ardhini, Jeshi la Majini na hata Jeshi la Anga.

Mheshimiwa Spika, nitolee tu mfano, Taifa la Uturuki ambalo kimsingi makampuni yake ndiyo yanafanya kazi ya kutujengea *SGR* hapa, yapo pia makampuni ya Serikali na ya watu binafsi yanayojishughulisha katika uzalishaji wa zana za kijeshi. Mitandao ni shahidi na ukweli upo, mashirika kama *FNSS* na *SSB* pamoja na Octane lile ambalo ni la Serikali yanatengeneza zana za kijeshi na kwa maana hiyo, dunia hii imefanana, ukiangalia miundo ya ndege za kijeshi zinazotengenezwa Marekani, Urusi na Uchina muundo wake unafanana.

Mheshimiwa Spika, na kwa maana hiyo, mimi nina imani kwamba jeshi letu nalo tukiliwezesha na hasa na mimi nilikuwa napendekeza kwako ikiwezekana tuanzishe mamlaka ambayo itahusika na mambo ya utafiti pamoja na maendeleo ya zana za kijeshi kwa maana kwamba tuwe na *National Defense Research and Development Agency* ambayo itakuwa inafanya kazi ya kufanya tafiti mbalimbali na kutembelea mataifa mengine kuona wanaendeleaje huko na hatimaye waweze kuzileta tafiti mbalimbali ambazo wanaweza kuzipata huko na kukaribisha mataifa mbalimbali yaje kuwekeza hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini ya kwamba Taifa letu linazo rasilimali nyingi, tunayo madini, maliasili na vitu mbalimbali ambavyo vinaweza vikatusaidia kuwa ni sehemu ya kuvutia wawekezaji mbalimbali kuja kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwa mfano, Taifa la Iran wamefanya Mapinduzi mwaka 1979 wakati sisi ndiyo

tunapigana na adui Idd Amin. Leo hii Iran tarehe 22 Aprili wamepandisha *satellite* ya kijeshi angani, kwa maana hiyo watu hawa wamewekeza na ukiangalia kimsingi ni kwamba teknolojia hii wamepata Korea Kaskazini, wamesaidiwa na Wachina na Warusi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata sisi nina imani kwamba jeshi letu likiwekeza vizuri katika mataifa rafiki na tukawa na sisi kama Serikali ikaweka nguvu zake kwa kuwekeza pesa katika mfuko wa Utafiti pamoja na Maendeleo Jeshini, nina aminimakampuni yetu ya Nyumbu na Mzinga yatakuwa na uwezo wa kuweza kutengeneza hizi zana.

Mheshimiwa Spika, upo uwezekano kabisa wa Taifa letu kuweza kutengeneza vifaru, magari ya delaya na hata meli pamoja na ndege za kijeshi kwa sababu uchumi wetu unaruhusu, mbele ya safari huko tutaweza. Kama Iran waliweza kuwakaribisha Warusi wakawatengenezea *nuclear reactor* kwa ajili ya matumizi ya kiraia kutengeneza umeme na sisi madini ya *uranium* yapo na kwa maana hiyo jeshi letu na lenyewe linaweza likaingia katika utaratibu huo wa kuweza kuwekeza katika matumizi rafiki ya madini haya ya *uranium.*

Mheshimiwa Spika, ninasema kwa dhati kabisa kwamba Taifa letu limefanya kazi kubwa ya kuweza kuyakomboa mataifa mengine na wakati huu sasa tunapokwenda kupigana tena vita hivi vya kiuchumi, ninaamini kabisa kwamba Jeshi letu la Ulinzi pamoja na JKT watakuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inawezekana na Tanzania ambayo ina ulinzi wa uhakika na yenyewe inakwenda kuzaliwa upya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, naunga mkono hoja, asante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele kwa mchango wako mzuri sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi na

atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi. Mheshimiwa Masaburi.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa ridhaa ya kuweza kusimama katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye yeye ndiyo amenipa kibali cha kuwa Mbunge katika Bunge hili kwa awamu hii ya uongozi wa awamu ya tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii adhimu kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye aliguswa na Mwenyezi Mungu na kuweza kuniteua na mimi kuwa Mbunge katika Bunge hili, nasema ahsante sana tena sana kwa kuniamini na Roho Mtakatifu aliyemtumia wakati ule uliokuwa tarehe 21 Oktoba, 2017 nasema sitamsahau. Mwenyezi Mungu aendelee kumlinda na kumtunza, malaika wake wamlinde siku zote za maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru wewe na kukupongeza kwa uongozi wako bora kwa kuweza kulisimamia Bunge letu na kama walivyosema Wabunge wenzangu, umekuwa Spika mwenye msimamo thabiti, nakupongeza sana na vilevile nakuombea urudi tena kwenye kiti chako hicho na wananchi wa Kongwa waweze kukurudisha tena upite bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa ujumla wake, kuanzia Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote na watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa umoja wao wamefanikisha nchi hii imetoka mahali fulani na imepiga hatua ya maendeleo katika mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa mawazo yao mazuri pia wameshiriki kujenga nchi hii. Waheshimiwa Wabunge hongereni sana

nawaombea kwa Mwenyezi Mungu muweze kurudi tena katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikimuangalia Mheshimiwa Rais wetu ninamfananisha na wale Manabii wa Mungu, ninamfananisha na Nabii Musa ambaye aliwavusha wana wa Israel katika Bahari ya Shamu kufikia katika nchi ya Ahadi, ninamfananisha na Manabii tofauti ambao walitumika na Mungu wakati ule. Kuna Nabii ambaye alitengeza safina, kuna Nabii ambaye alitumika katika lile eneo la Mnara wa Babeli, kuna Manabii tofauti walitumika kwa nyakati tofauti pale watu walipomuasi Mungu, Mungu aliwatumia Manabii na Manabii wale waliwaelekeza watu lakini kuna watu walikuwa na mioyo migumu.

Mheshimiwa Spika, Nabii wetu wa sasa wa karne hii Dkt. John Pombe Magufuli ametumia muda wake wa kipindi kifupi sana katika kufanya maono ambayo sasa hivi ndiyo tafsiri yake inaonekana. Kwa mfano, amejenga hospitali, ameongeza bajeti ya dawa, ameimarisha miundombinu katika sekta nzima ya afya, lakini ameimairisha huduma ya maji. Katika maeneo haya yote na ujio huu wa gonjwa la Corona, najiuliza kama si maono ya Dkt. Magufuli hivi hawa watu ambao wanaugua wangepata huduma ipi, maana yake huduma zingekuwa chache.

Mheshimiwa Spika, maji Mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa ni tatizo, lakini sasa hivi maji ni historia katika Mkoa wa Dar es Salaam. Ndiyo yanayotumika kwa watu kunawa mikono ili kujikinga na ugonjwa wa Corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kuliangalia na kutafakari kwa kina huyu mtu si mtu wa kawaida. Ni Mwenyezi Mungu amemshusha kwetu Watanzania na sisi Watanzania tunapaswa kumuenzi na kumthamini na tuzidi kumuombea kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu si kitu cha kawaida. Hata ukiangalia hotuba yake ya juzi aliyotoa imekuwa gumzo duniani kote, Mataifa mbalimbali wanaomba ile *speech* katika lugha zao duniani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninawaomba wataalam wa lugha hapa nchini wasaidie ile *speech* iweze kufika katika lugha tofauti huko duniani, waweze kumsikia Nabii wetu anayetoka Bara la Afrika, aliyezaliwa Tanzania na wazazi wake kule Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namuona wa Chato ameshtuka, hongereni sana wana wa Chato kwa kumlea na kumtunza Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mafanikio yamesaidia sana katika mapambano ya ugonjwa wa Corona maana hii miundombinu ndiyo imesaidia watu kuwa watulivu wakati wakipatiwa huduma. Niliona katika *clip* moja ilikuwa inaonesha kwamba kuna nchi fulani walikuwa sasa hivi wanageuza shule na ma-*godown* kuwa wodi za wagonjwa wa Corona, lakini sisi Mungu ametupendelea hospitali zipo. Watu wetu wanapata huduma wakiwa kwenye hospitali nzuri sana za kisasa, tunataka nini Watanzania? Mungu atupe nini kama si zawadi Mungu aliyotupa Rais wetu wa aina hii.

Mheshimiwa Spika, askari yeyote duniani tunasema hakimbii vita na Mwenyezi Mungu katika makundi ambayo amewasamehe tunaamini amewasamehe dhambi ni askari ambao wanasaini kufa au kupona. Ni kama askari wa Jeshi la Wananchi au askari yeyote duniani wenye nia njema katika kulinda nchi yao, lakini kuna askari ambao ni kama madaktari ambao wanaokoa roho za watu/wanadamu walioumbwa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, makundi haya yamesamehewa dhambi, lakini naomba kundi hili la wanajeshi/madaktari tunaomba Serikali iongeze bajeti ya kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge walivyopendekeza kwa upande wa Jeshi la Wananchi wapewe fungu la kuweza kufanya utafiti katika masuala ya afya, lakini na masuala mbalimbali ambayo yanaweza kuwa suluhu ya matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme nawaomba Watanzania tuache kumuasi Mungu. Matatizo haya ya Corona tunaweza kuiangalia kwa kufikiria kidogo kidogo, lakini na matatizo haya ni uasi ambao tumemkosea Mwenyezi Mungu. Ndoa za jinsia moja si jambo la ajabu, mwanaume na mwanaume wanaoana, wanawake kwa wanawake wanaoana, lakini hata wanaume ambao wapo kwenye ndoa na wake zao wanawageuzi wanawake zao kinyume cha maumbile.

Mheshimiwa Spika, pia hata madada/mabinti zetu wanarubuniwa na wanaume kwa kisingizo cha kuhongwa magari na kujengewa majumba wanaharibu kizazi chetu, lakini tumesikia kuna taasisi za kijamii zinapita kwenye shule kuwarubuni watoto/wanafunzi katika mambo ya ushoga, haya mambo lazima tuseme. Kizazi kinaharibika, Tanzania hatutaki huu uchafu katika nchi yetu, hatutaki ushoga na wakome kuja kuwarubuni watoto wetu wadogo kwa kisingizo cha kuwapa vihela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba wanawake majumbani wawatunze watoto, nawaomba walimu wawafatilie wanafunzi, hii tabia imeenea, watu hatusemi, lakini ni wajibu wetu lazima tuseme, hii tabia ya ushoga nadhani ndiyo chukizo la Mwenyezi Mungu. Mwanasayansi namba moja aliyeumba mbingu na dunia ndiyo amekasirika maana yake tutasema sayansi inasema, lakini mtu *creator,* mwanasayansi ni Mungu mwenyewe aliyosema anga na iwe na ikawa, bahari na iwe ikawa huyo ndiyo mwanasayansi aliyotoa maarifa kwa wanasanyansi wa duniani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili tatizo la Corona tulifatilie kwa umakini, twende tukawahamasishe wananchi wetu wafate masharti yanayotolewa na Wizara ya Afya, tuvae barakoa, wote tuvae barakoa, tuamue nchi nzima tuvae barakoa kwa lazima. Nimeenda hapo sokoni hapo Dodoma watu akinamama hawavai barakoa na wako karibu karibu, tunaomba mapambano haya twende kwa pamoja bila ushirikiano wa pamoja hatuwezi kumshinda adui.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme Mwenyezi Mungu ana upendeleo ametupendelea sisi Watanzania mpaka kufikia leo hii ni kudra za Mungu na Mungu mkono wake uko juu yetu, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa viongozi wenye maono, Mungu endelea kuwalinda viongozi wetu, Mungu akulinde Spika wetu, Mungu awalinde Wabunge wote, Mungu awapokee kwenye nuru ya uso wake wale waliotangulia mbele za haki akawapumzishe kwa amani, ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, sasa nimuite Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi na Mheshimiwa Alhaj Almas Maige atafuatia. Mheshimiwa Kapufi tafadhali.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote na mimi naunga mkono hoja, lakini utaona karibu kila mzungumzaji anayezungumza anaanza na neno la pongezi, na pongezi kwa tabia yake ina tabia ya kumtia mtu moyo kwa sura hiyo hiyo na mimi naomba niwapongeze wote nikupongeze Spika, lakini nimpongeze Waziri, niliwahi kusema huko nyuma nikatumia neno Rahim, pia Waziri huyu ni mtu Rahim huko kwenye Kamati tumeona jinsi alivyo mtu Rahim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa hali ya mipaka yetu ni shwari, ushwari siyo jambo linakuja lenyewe, ukiona vinaelea vimeundwa, kwa hiyo, huu ushwari tunaouona wa mipaka yetu ni kutokana na kuwa na Jeshi imara. Sasa Jeshi imara ili liendelee kuwa imara zile changamoto zinazojitokeza najua mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kazi iliyoko mbele yetu ni matokeo ya sisi kama Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa hiyo, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo nikiamini hayo mengine tayari tulikwisha yajadili katika ngazi ya Kamati na kwenda kuongezea minofu kidogo kwenye hiyo kazi nzuri ambayo Kamati imeifanya.

Mheshimiwa Spika, hili la mipaka nimesema japo tuna changamoto ya uharibifu wa alama za mipakani, tumelisema

hilo ili lifanyiwe kazi maana yake kama alama hizi tutaacha zinaendelea kuharibiwa kesho, kesho kutwa itakuwa ni chanzo cha vurugu maana yake mwingine atasema hapa pangu hapa pangu. Lakini hizo alama tukiendelea kuzifanyia kazi itakuwa ni jambo lenye tija.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia ni kweli limeongelewa na mimi niendelee kumpongeza, najua Rasi Mshindo, Kilwa lakini maeneo ya Kikombo hapa Dodoma na mimi niendelee kusema changamoto zinazojitokeza katika maeneo yote yanayogusa fidia ukienda kule Katavi kuna suala la kampuni na watu wa jeshi kama kuna changamoto zozote hapo nilikuwa naomba ziendelee kufanyiwa kazi, kwa sababu Jeshi letu na mimi nampongeza sana Hayati Baba wa Taifa alipolibatiza jina kuwa Jeshi la Wananchi unaiona kabisa sura ya wao kuwa wa kwetu kwa maana Jeshi la Wananchi na hapa tusiache, nakumbuka wakati tukijadiliana katika Kamati kuna suala la kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura inapohitajika.

Kwa hiyo, mimi niliombe jeshi katika eneo hili dharura zipo nyingi, majanga yako mengi, mafuriko, iwe ni Corona, iwe ni vitu vingine, lakini ili waweze kukabiliana na majanga ni kulifanya liwe na vifaa, ni kulifanya liwe na fedha changamoto ya rasilimali fedha, Jeshi letu tukiendelea kuliwezesha kwa maana hiyo mimi nasema litaendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na changamoto mbalimbali zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, JKT 830KJ Mkupuka - Kibiti, tulipita kule, Kibiti huko nyuma ilikuwa ndiyo gumzo la kila siku, lakini leo hii kuko shwari. Ushwari umekujaje kwasababu kwanza hii JKT imewekwa kimkakati na sehemu kubwa ni suala la usalama. Kwa hiyo, ili tusirudi kule Kibiti ile ya wakati ule miundombinu ile ambayo ni korofi pale hapa mara ya mwisho watu hawa hawakupatiwa fedha ya maendeleo. Niombe sana ili kuweza kuifanya miundombinu iwe salama na maeneo yale yaendelee kuwa salama tukirejea kwenye kusudio la awali la kufanya maeneo yale ili watu wetu wawe salama na nchi iwe salama kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, hili la ufinyu wa bajeti tumekwisha kuliongelea lakini kuna suala la madeni niendelee kuomba ili kutoa nafasi zaidi ya miradi ya maendeleo ni pamoja na kuyaangalia madeni, kwa hiyo madeni yanayogusa watu mbalimbali ambao wamefanya shughuli na jeshi letu tuendelee kuyaangalia. Najua kuna ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi kwa maana ya Dodoma.

Changamoto zinazojitokeza duniani ni kweli kuna mzungumzaji wa mwanzo hapa ameongelea hata habari ya virusi na silaha za kibaiolojia wakati tunakwenda kufikiria ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Jeshi, Dodoma ni jambo jema, lakini tusiache haya yote pamoja na tafiti hizi ambazo wazungumzaji wote wa awali wameendelea kuzisema, kwa sababu Jeshi kwa nidhamu yake ni watu wanautii, lakini ni watu wanatakiwa waende mbele zaidi.

Sasa hili suala la utafiti ambalo tumekuwa tukiendelea kulizungumza litawezekana tu najua tunazungumzia habari za Nyumbu, lakini tunazungumzia habari za Mzinga, hawa wote ili waende huko tunakotamani kuwaona wakifanya shughuli za kitafiti changamoto ni hiyo tu rasilimali fedha, kwa hiyo nilikuwa naliomba sana hilo ili tuone kwamba Jeshi letu linaendelea kuwa la kisasa, lakini linalokabiliana na changamoto zilizopo duniani.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapo awali mimi ni Mjumbe wa Kamati ambayo imewasilisha suala hili kwa mchango huu nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi kwa mchango wako mzuri kabisa. Sasa nilikwishasema namuita Mheshimiwa Alhaj Almas Maige na atafatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King. Mheshimiwa Maige tafadhali.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, na mimi pia naomba nikushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kweli siwezi kuzungumza bajeti ya majeshi bila kwanza kumtaja kwa unyenyekevu mkubwa Amiri Jeshi Mkuu wa

Majeshi ya Ulinzi na Usalama Dkt John Joseph Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kumkamata mkono, kumshika mkono Mheshimiwa huyu Amiri Jeshi Mkuu na nimpongeze kwa kazi kubwa ya kuiweka Tanzania katika njia yake kuu ya zamani ya kutoyumba na kuwa na misimamo ya kitaifa na kizalendo. Zile kauli za zamani kwamba Tanzania imesema naziona zinarejea, enzi zile za Mheshimiwa Marehemu Baba wa Taifa tulikuwa tukisema Tanzania watu wanasikiliza.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni hotuba ya Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu juzi imekuwa gumzo kila mahali duniani lakini pia maamuzi yake imara ya kutoifunga nchi hii kitu kinachoitwa *lockdown* yamekuwa mfano mkubwa na wale ambao walikuwa wamefunga sasa wanafungua, lakini wamepata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Amiri Jeshi Mkuu katika kusimamia suala hili la Corona inaonyesha jinsi gani ana misimamo ya kizalendo na hasa hasa ya Kitanzania ambayo kwa kweli italipeleka Taifa hili mbele, kwa hili mimi nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naona upande wa pili kule wenzetu watani zetu wale hawapo lakini mimi sishangai hili wala siyo geni kwa upande ule, nilikuwepo Bunge la Katiba walitoka ilipokaribia kupatikana Katiba Inayopendekezwa, lakini baadae wanaitaka Katiba hiyo na wao lakini walitoka. Lakini pia mara ya pili walitoka kwa kumuogopa Naibu Spika muda mrefu mpaka walipopewa chai Ikulu, wakarudi tena na sasa wametoka wanaogopa Corona.

Sasa sijajua, mimi sijaamini kwamba madaktari nao wataogopa kwenda kwenye wodi za karantini wakimbie Corona, sisi tuko hapa kwa kazi kama vita, tuko ndani ya ukumbi huu huu ambapo wenzetu wametoka wakatangulia mbele za haki, lakini sisi tumo kwa sababu tuna kazi ya

kutengeneza bajeti ya kupitisha bajeti ya Wizara zote na baadae Serikali ikafanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni bajeti maalum na muhimu kabisa kwa sababu ya majukumu na dhima ya Wizara hii ya kulinda mamlaka maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu mara kwa mara imeshauri kuongeza kwa ukomo wa bajeti kwa mafungu yote 38, 39 na 57 ili Wizara itekeleze majukumu yake kikamilifu, lakini lipo suala la utafiti wataalam wanasema *research and development,* majeshi yetu yanataka kufanya utafiti na Serikali inalo fungu la fedha la utafiti, lakini limewekwa kwenye taasisi ya kiraia na jeshi haliwezi kupeleka tafiti zake kwenye taasisi hii ya kiraia, *COSTECH* nafikiri ili waweze kuwapa wasome andiko la jeshi ni nini halafu waruhusu hela hii, haiwezekani kwa watu wote wenye busara suala hili haliwezekani.

Kwa hiyo, Jeshi limekuwa linafurukuta lenyewe kutafuta hela na pale kufanya tafiti, lakini utafiti ni kazi kubwa sana na ni ghali sana na bila utafiti jeshi letu litadumaa, lazima Serikali itoe hela inayowapeleka kwenye taasisi ya kiraia ya tafiti ya kiraia iwe peke yake na hela za utafiti wa kijeshi uwe peke yake ili jeshi liweze kufanya *research and development* au inaitwa *R&D* kitaalamu hii itatusaidia sana kuweza kuwa na jeshi la kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nashauri sana Serikali ipeleke hela kwenye mashirika yetu ya Nyumbu na Mzinga hasa zitumike kwa ajili ya utafiti. Lipo suala la ukosefu wa hela kidogo zinazopelekwa kwenye taasisi za kijeshi Mzinga na Nyumbu, Kamati yangu imeona mapungufu haya na naunga mkono ushauri kuwa Serikali inyooshe mkono au ifungue mkono iwapelekee hela ili waweze kuendeleza tafiti ambazo zipo au zile ambazo wanataka kuzifanya na kwa maslahi makubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimetaja kidogo mambo ya SUMA JKT na *SUMA Guard* naomba ni *declare* kwamba mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Makampuni ya Ulinzi Tanzania, na *SUMA Guard* ni moja ya makampuni ya ulinzi yanayofanyakazi vizuri sana yanahitaji kupongezwa sana, lakini mishahara kwa sasa hivi imepangwa na Serikali kwa pamoja na sekta binafsi *(private sector)* kupitia *LESCO* na mishahara iko ya aina mbili tu kwa sekta ya ulinzi, mishahara ya makampuni ya nje na mishahara ya makampuni ya ndani, kima cha chini ya mishahara kwa makampuni ya ndani ni shilingi 100,000 kwa mwezi. JKT au *SUMA Guard* wanalipa shilingi 190,000 wako juu ya kima cha chini cha mishahara ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kinachokosekana hapa kama kuna upungufu wa mishahara ni kasoro hiyo ya kutokuwepo na Sheria ya Ulinzi ambayo itapanga mishahara na *grade,* sasa hivi hakuna madaraja katika sekta ya ulinzi daraja la kwanza, la pili na la tatu hakuna kwahiyo inakuwa vigumu kufikiria mshahara gani ulipwe wapi pengine kampuni ya *SUMA Guard* ingekuwa daraja la kwanza au daraja la pili, kwa hiyo viwango vyake vingejulikana. Sasa hivi makampuni yote yana madaraja mawili tu; makampuni ya nje au makampuni ya ndani makampuni ya ndani shilingi 100,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nilisoma mimi hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mengi nimeyasema wakati nasoma hotuba ile naomba niishie hapa, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie Wizara hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Alhaj Almas Maige. Nilishakutaja Mheshimiwa Ali Hassan King na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae. Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru sana kupata nafasi hii awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na kutujaalia kuwa wazima na lingine nikushukuru wewe kwa jinsi hili Bunge letu bado linaendelea na tunashukuru kwamba uhai tunao, hatuja kufa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpe neno la faraja pale dada yangu Mheshimiwa Maryam Msabaha ambaye alisema kwamba wanatuombea mabaya kwamba yatukute mabaya. Sifa ya Maryam ni mkazi wa Jang'ombe, lakini yeye ndiye mwenye ofisi nzuri kabisa ya CHADEMA katika Tanzania hii katika Jimbo la Mpendae pale amejenga ofisi moja kubwa sana. *(Makofi)*

Sasa dada yangu Maryam nikupe faraja moja, anavyotaka mtu siyo anavyotaka Mungu, anavyotaka Mungu ndiyo yanayokuwa mtu yeye atafanya tu mambo yake mengine na wale waliosema kwamba wanakimbia kifo kwa kukimbia kwenye Bunge, si kweli wanajidanganya tu, Mungu anasema *ainamatakun yudirikum lmauti walaukuntum fiburujimushayad* (mtakapokuwa nyie mauti yatakufikeni tu hata mkiwa katika ngome madhubuti) na kingine wanaambiwa kwamba; *kulli innalmauta ladhi tafiruna minhu fainnahum lakiku* (hayo mauti mnayoyakimbia yatakukuteni tu); lakini kingine; *wamatadhir nafsu madhatas kibu ghadhan* (nafsi haielewi kesho itachuma nini); *walaa tadir nafsu biayyi ardhi ntamutu* (wala nafsi haijui itakufa katika pahala gani), haijui kabisa.

Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi umauti ni wake Mungu kwahiyo wao wanasema wanakimbia hapa Corona, lakini wako mnadani huko wanaenda mnadani Jumamosi tumewakuta mnadani huko, sasa wanakimbia Corona hiyo kule mnadani na hapa Bungeni wapi inapatikana kirahisi. Ndiyo maana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam atawakamata huko, kwa hiyo, sisi wala siyo kitu cha kusema hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna kisa kimoja enzi za mitume kilitokea alikwenda mtu mmoja kwa Mtume Suleiman, yule mtu akamkuta mtu mwingine kwa Mtume Suleiman, kwa hiyo yule mtu akawa anamtizama sana yule mtu aliyekaa na Nabii Suleiman, yule mtu akapata hofu, akamuuliza Nabii Suleiman huyu ni nani? Akamwambia huyu ni malaika anayetoa roho, kwa hiyo, pale yule mtu akamwambia Nabii Suleiman una uwezo wa kunihamisha nchi hii? Nabii Suleiman alikuwa na

uwezo wa kuamrisha upepo, akauambia upepo mchukue huyu mpeleke China, kwa sababu amemuogopa amesikia pale pana Israeli pale, kwa hiyo akachukuliwa pale akapelekwa China anafika China tu anatua tu anamkuta yule aliyeambiwa huyu ndiyo malaika anayetoa roho, anamuuliza dah nilishangaa sana nilipokuwa nakukuta kule wakati niliambiwa nije nikutoe roho huku China, wewe wakati huo uko kule Jerusalem. Sasa kwamba kumbe mauti hayakimbiliki, kwa hiyo tusijidanganye hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii ya Wizara wa Ulinzi na Jeshi ya Kujenga Jeshi la Kujenga Taifa ni lazima tunzungumize mambo ambao yana husiana na kiongozi wetu juu majeshi yetu haya. Kuna kiongozi mmoja wa chama cha upinzani, nimesikia katika chombo cha habari akisema kwamba kwa nini Rais ameviita vyombo vya ulinzi na usalama badala kuwaita watu wa afya? Hivi haweze kujua kwamba pengine kama kuna *biological weapon* kama siyo Jeshi la Wananchi na nani anausika na mambo hayo? Angeusika nani? Lakini ingelikuwa kama Corona ni janga ni jeshi gani linahusika majanga kama siyo Jeshi la kuzima moto na majanga? Kama katika Corona kuna mambo ya *criminal* yanafanyika na wengine wanapanga kufanya mambo ya *criminal* kama tunavyosikia ni nani anayehusika na *criminal* kuliko Jeshi la Polisi?

Mheshimiwa Spika, lakini kama Corona inapitia mipakani au kwamba inaweza ikatoka kwa kupitia mipakani, kama siyo Jeshi la Uhamiaji ni nani mwingine anaweza akahusika na kuzuia na kuingia watu katika mipaka yetu? Sasa ni lazima tutazame kwamba Rais wetu ameona mbali katika kuviita vyombo hivi vya ulinzi na usalama, katika kuwaambia jambo hili na ukienda katika *TISS* au Usalama wa Taifa hao ndio wamenzunguka na mambo yote hayo wanayo na yote hayo wanayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini kumbe nilivyoangalia nikakuta kwamba kumbe kuna baadhi ya viongozi wanaweza wakawa wakubwa katika taasisi, lakini wakaosa

hekima. Hekima ni hiki ni kitu ambacho ni kizuri sana kukitumia katika kuamua jambo na unapotaka kufanya jambo lolote ni lazima uliamue na ulifanye kwa hekima na hekima si lazima kwamba awe nayo mkubwa, inawezakana hekima hiyo anaweza akawa nayo mdogo. Ndiyo maana unapotaka kuamua jambo uwashikirikishe wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingekuwa hekima ni uwasho wa pilipili, basi tunasema kwamba inapatikana kwenye pilipili kichaa kuliko kwenye pilipili mboga. Kwa maana hiyo pilipili kichaa ni ndogo lakini ina uwasho mkubwa, lakini pilipili mboga kubwa hilo lakini chapwaa, halina uwasho wowote. Lakini sijakusudia kusema kwamba kiongozi wa chama cha upinzani hicho kwamba ni pilipili mboga. Sijakusudia, *chija chema* hivyo Wamakonde wanasema hivyo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije nichangie katika *SUMA JKT Construction Company Limited,* jeshi letu hili tumeliona kwamba linafanya kazi nyingi sana nzuri na mimi nilikuwa naomba kwamba liendelee vizuri sana. Lakini nilikuwa naomba wawe *proactive,* mara nyingi jeshi letu linafanya kazi ambazo linapewa na Serikali. Lakini hapa ukitazama hili jina limeandikwa *SUMA JKT Construction Company Limited,* ina maana lipo chini ya Msajili wa Hazina. Nilikuwa napendelea zaidi kwa *potential* ambayo wananayo, wangekuwa wao wenyewe wanaweza kutafuta fedha kupitia Msajili wa Hazina na nalizungumza hapa mbele Waziri wa Fedha wakaanzisha kwa mfano Rais amejenga pale *Magomeni quarters* amefanya ujenzi mmoja mkubwa sana. Lakini pia Serikali ilikuwa ina nyumba zake ambazo zikisimamiwa na taasisi nyingine pale Magereza Ukonga. Lakini kwa nini kama wao wasiseme labda sisi tunaenda tunajenga mji wa Tandale. Wakaazisha wao wenyewe kwa kupitia/kutafuta fedha vyanzo kwa kupatia vyanzo vya fedha ambavyo vipo kwa hiyo wakaendelea wakafanya hilo jambo likawa kubwa, wakaenda pengine mpaka Kongwa wakasema tunajenga mji wa kisasa wa Kongwa ambao utakaliwa na wananchi, kuliko kuja kuchukua kazi ambayo labda ilimshinda mtu fulani halafu wao wakaenda, wana uwezo wa kutafuta fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, nchi kama ya China iliendelea kwa sababu ilikuwa wanafanya kazi zao katika *brigades* na *brigades* zile ziliwekwa na zilikuwa zinafanya kazi katika sehemu tofauti tofauti. Kwa hiyo, na sisi tumeona ule uweza ambao upo katika hili jeshi, kwa hiyo upo uweze wa ku-*capture* hiyo *opportunity* kupitia jeshi hilo na si ajabu kama tutasema kwamba jeshi hili litakuwa linaendesha katika mfumo huo wa kuchukua fedha katika masoko yetu ya mtaji litakubalika tu. Kwa sababu chema chajiuza, watu wote wanakubali kwamba JKT wanao uweze wa kujenga na kuendeleza mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ambacho kinzungumzwa na watu wengi kuhusiana na masuala ya *Research and Development.* Ukitazama Mzinga na Nyumbu walieleza katika ukurasa wa 77 katika hotuba ya Waziri *paragraph* ya 77 katika hotuba ya Waziri, walisema wana tatizo au changamoto ya rasilimali watu. Mimi nilikuwa nishauri kitu kimoja mara nyingi sana mitaani ukitizama *television* zetu wanatoka wabunifu tofauti tofauti ambao wanatoka mikoani, vijiji wanaanzisha vitu tofauti tofauti, kwa nini hawa wasiwe sehemu ya watu ambao wanaweza labda wakawekwa kule? Na kingine kwa nini katika sehemu hii ya Mzinga na Nyumbu wasipatiwe fungu zuri la kufanyia *research* ambao pengine wanaweza wakafumbua mambo tofauti kama nchi nyingine wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi mchango wangu leo niliona ni-*base* katika masuala haya mawili; moja *SUMA JKT* kutokana na muundo wake ulivyo kwa kupitia Msajili wa Hazina wawe wabunifu zaidi, wawe wanachukua kazi sio kutarajia fedha ambazo zinazotoka Serikalini, wawe wanauweza na mfumo wa kuanzisha fedha. Kwa sababu katika changamoto walizosema ni rasilimali fedha, kwa hiyo, wao wana uwezo kupitia kwa Msajili wa Hazina wanaweza wakafanya *structure* ya mambo yao kule wakapata hizo fedha. Lakini katika rasilimali watu katika Nyumbu na Mzinga pia upo uwezo huo wa kupata hawa watu na serikali ijaribu kuwaangalia hawa Nyumbu na Mzinga ili waweze kufanya ubunifu katika kikosi chao cha *Research* and *Development.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan Omar King tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma nilishakutaja na badala yako Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel atafuata. Mheshimiwa Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema leo tupo kwenye mjadala wa Wizara ambayo kwa mtazamo wangu ni mboni ya jicho la Taifa, ndiyo sehemu pekee tukitazama kama mboni yetu tunaweza tukakusanya bongo zote kubwa za Taifa hili, zikakusanywa kule na kutengenezewa mazingira mazuri sana ili wabaki na kazi moja tu ya kutafakari na kuweza kuyaona yale mambo ambayo hayawezi kuonekana kwa macho ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nichangie kwenye eneo la malengo ya wizara kipengele “c” kujenga uwezo katika tatifi mbalimbali uwailishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na raia. Lakini ningetamani sana kwenye eneo hili kama Katibu Mkuu sijui kama ni mimi sijaelewa vizuri sana kama ikiwezekana akaongeza tafiti na ugunduzi.

Mheshimiwa Spika, ulitutuma mwaka 2017 kule Ujerumani, wakati huo nilikuwepo kule upande wa kina kaka zangu watoro. Wakati ulitutuma Ujerumani tukapokelewa na Spika wa Bunge la Ujerumani, akatutembeza maeneo mbalimbali akatupeleka kwenye jengo ambalo linaongonzwa na Mwanasayansi Mkuu wa nchi hiyo. Alikuwa ni Muisrael mrefu mnene sana lakini kuwa na ubishi kwa sababu mle kulikuwa na ule mjusi ambayo anasemekana ametoke Tanzania. Lakini kwenye ile maabara kulikuwa na mafuvu ya vichwa mbalimbali wamekusanya wakati wakitawala sehemu dunia wamechukua mafuvu ya watu mbalimbali na viumbe mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tuliokwenda nao nilikuwepo na akina Kafumu,

Mama Chatanda na wengine, wakawa wanapendekeza kwa nini mjusi wetu asirudi. Baadae sijui kwa nini yule jamaa akaniambia hebu twende ofisi kwangu, nikaenda ofisi kwake nilipovyo-*check* ni kama mwanajeshi yule. Lakini alichoniambia alisema haya mafuvu unayoyaona humu sisi hatutumii kukusanya fedha za utalii kama watu wengine wanavyo fikiri. Akasema tunatumia haya mafuvu na mfupa huu wa mjusi anayetoka kwenye Tanzania kumuingia Mungu alifikiria nini miaka milioni mbili iliyopita? Na kutazama Mungu anawaza nini miaka milioni mbili ijayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumuingia Mungu kwa namna hiyo tunakuja na sayansi na teknolojia na tunaitawala dunia. Hayo ndiyo nilikuwa nayapendekeza juzi nikichangia Wizara ya Afya hasa pale niliposema ambao namshukuru Mheshimiwa Nahodha ameilezea vizuri, nikisema tuwe na Chuo Kikuu cha Jeshi cha Utafiti na Ugunduzi ambao tutakuwa kwenye pori ambapo tutakusanya na ukiangia huko nyuma *Tabora school*, *Tabora school* ilikuwa ni shule ya mchepuo ya ulizi na uongozi.

Mheshimiwa Spika, wakati huo kila Wilaya ilikuwa inachukua wale watoto wenye uwezo mkubwa sana wanawekwa pale Tabora. Wanafundishwa mambo mbalimbali pamoja na uzalendo na vitu vingine, lakini nafikiri ilikuwa lengo ni kujua *brain* za nchi ziko wapi? Mimi nafikiri na ninakumbuka, ukiangalia Nyerere amesoma pale, ukienda Mzee Sitta alisoma pale, huku Bungeni kuna Shangazi alisoma hapa, lakini hata Lipumba ndiyo maana tabia yake sio mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunafikiri tuanze kutengeneza mfumo wa jeshi pamoja na Usalama wa Taifa wa kutambua zile *brain* za nchi na wale watoto wenye akili sana na wakati mwingine kuwatambua watoto wenye akili sana, sio sana ni kufaulu tu, una weza ukatambua kwa njia wanavyofaulu darasani, lakini kuna wengine hawafaulu sana darasani, lakini wana akili sana. Maana yake ukimuangalia Eusten alikuwa anafaeli darasani lakini mwisho wa siku ndiye aliyeizungusha hii dunia.

Mheshimiwa Spika, leo tuna teknolojia na *5G,* swali la kwanza kujiuliza sisi Watanzania, wakati wenzetu wako kwenye *5G.* Je, sisi tupo hata kwenye *1G?* na *repercussion* yake kama wenzetu wanagomba kama Marekani na China kuhusu *5G* kwenye ulinzi na na usalama na mambo mengine maana yake hata wenzetu wanaotugaia karatasi sasa tukifika kwenye *5G* ina maana wataondoka humu itakuwa una roboti moja hivi inatuletea hivi kila kitu kinakuwa *contolled* hatuhitaji, Je, sisi kwenye tasinia zetu zote tunajipangaje?

Mheshimiwa Spika, sehemu pekee ukilinganisha na *discipline* ya jeshi letu na jeshi letu lilivyojipanga na lilivyotuonesha kwa wakati wowote ule walivyokuwa tayari kufanya, watu hao wenye akili tukiwaweka kwenye ndani ya jeshi na usalama wetu wa Taifa tukawapa *resource* za kutosha wataweza kufikiria vizuri sana na kutusaidia na sisi tukimbizane na dunia inayokimbia.

Mheshimiwa Spika, leo ukimwangalia wenzetu waliokimbia kule juu tofauti na Amiri Jeshi Mheshimiwa Dkt. Rais John Pombe Magufuli na baadhi ya viongozi waliokimbia kule, ukimwangilia Mheshimiwa Dkt. Rais John Pombe Magufuli kabla hajawa Rais hata Mbunge, utamkuta yupo shuleni na watoto ana-*titrate,* anangalia *chemisty,* anachanga madawa anaangalia *color* zinavyobadika nakufundisha watu.

Mheshimiwa Spika, lakini viongozi waliopita kule ukiwaangalia kule nyumba utakuta hata wengine wamekamatwa na polisi wanavusha bia za magendo kutoka Tanzania kutoka Kenya. Unaweza ukawaangalia wengine ukakuta wapo *club* na mabaunsa kuhakikisha kuweka mambo ya *club* sana wanapofika humu Bungeni wanafikiri uendeshaji wa nchi na Taifa na Bunge unaenda kama uendeshaji wa mtaani.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana leo mimi nafikiri kuna umuhimu wa sisi kukaa chini kuhakikisha tunatengeneza mfumo wa kinchi wa kuanza kujua *brain* za Taifa hii. Moja, zitusaidie kuchunguza siri za maumbile ya uumbaji wa Mungu.

Lakini pili, tuhakikishe kwenye kuja viongozi humu ndani waweze kuja watu wenye akili sana.

Nikueleze wakati wa Uyunani dunia iliharibika sana, hata vitabu vya Mungu viliharibiwa. Lakini akatokea mwanasayansi mmoja anaitwa Pilato huyo jamaa alikuwa anatembea kwa kuangalia jua. Anaangalia jua halafu mahesabu yanamijia kichwani wakati huu alipoanza kuja na hayo mahesabu, wanafalsafa wote walikusanyika duniani ndio wakaanzisha chuo kikuu cha kwanza Ulaya ambacho walivyokusanyika ndipo waliosoma hicho Chuo Kikuu wakatoka ndio maana Ulaya ikanyanyuka. Aliamini nini, aliamini ukifaulu hesabu na sayansi unakua kiroho na kimwili.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku walipotoka wale watu waliosoma hesabu na sayansi ambao wamekua kiroho na kimwili na ndio maana Rais wetu anajua sayansi haiwezekani bila Mungu. Dini haziamini *definition* ukienda kwenye kamusi za sayansi.

Mheshimiwa Spika, *genius* ni mtu mwenye uwezo wa kuyaona siri za maumbile, siri za Mungu kwa kutumia nguvu za Roho Mtakatifu akazileta duniani, akazibadilisha zikawa sayansi. Ndio *genius* na ndio maana tunapofika mahali tupo kwenye gonjwa kubwa kama Corona, Rais wetu anaposema twendeni tukaombe anajua tukiomba katika ulimwengu wa kiroho akili za binadamu zitapasuka na *solutions* zitaonekana kwa kupitia nguvu za kiroho na zikija zikiletwa katika ulimwengu wa dunia namna hiyo tunaweza tukapata uvumbuzi wa tatizo kama la Corona.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio mambo yanayofanyika na watu wenye akili kubwa. Ndio maana mimi narudi nasema kwamba Rais wetu tuna *opportunity* kubwa ya kufanya haya mambo ambayo katika akili ya kawaida ninavyozungumza hivyo, kwanza wengi wanaweza wasinielewe nasema nini. Lakini katika akili ya kawaida inawezekana ionekane isiwezekane kufanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini tukiwa na Rais, Waziri Mkuu, Spika kama wewe ambayo dunia nzima inaelekea upande huu, ninyi mnathubutu kwenda upande huu bila kuogopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukishakuwa na viongozi wakuu wanaothubutu kufanya hayo. Nataka kukuhakikishia leo, tukisema tunataka kwenda kuzitumia *brain* za Taifa hili tukaamua tukajenga Taasisi za kitafiti kubwa katika Taifa hili, tutaweza kufanya hivyo kwa sababu tuna miradi mikubwa sana tumethubutu ambayo hakuna mtu yoyote ambaye angeweza kuifanya.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema mimi nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niishukuru Serikali, nimeipokea Wilaya ya Siha wakiwa wanapambana kwa zaidi ya miaka 15 kuhitaji lami. Leo ndani ya Wilaya ya Siha kuna lami iliyojengwa kwa thamani ya shilingi bilioni 52.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Siha tumeipokea haina Hospitali ya Wilaya, leo Wilaya ya Siha imepata shilingi bilioni 1.75 imejengwa Hospitali ya Wilaya na tumeipokea Wilaya ya Siha ikiwa inapata fungu la dawa shilingi milioni 32. Leo tunapata shilingi milioni 256. Leo pale Siha kuna ghorofa tatu zinajengwa kwa shilingi bilioni tisa kwenye Hospitali ya Kibongoto, inajengwa maabara ya kisasa ya magonjwa yanayoambukiza ikiwepo Corona na kuweka vifaa inajengwa maabara ya namna hiyo kwa shilingi bilioni tisa ambayo itatumika kwa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumza hivi Wilaya ya Siha, mkandarasi yupo mwingine upande mwingine yupo na shilingi bilioni 1.6 anaweka maji. Upande mwingine shilingi bilioni 1.75; kule Donyomoro shilingi milioni 752; Kashashi shilingi milioni 452, Levishi shilingi milioni 380 hayo ni maji na kila dola moja unayoingiza kwenye maji unapunguza dola nne kwenye Wizara ya Afya. Maana yake ukiwekeza kwenye maji hata matumizi kwenye Wizara ya Afya yanapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme wewe umetusaidia, dunia iliyopo zamani watu walikuwa wanaogopa mabumu ya *nuclear*. Walikuwa wanafikiri na *nuclear detunes* nyingi na bajeti nyingi zimetumika kwa ajili ya kujiweka vizuri kwenye silaha za *nuclear* na nyingine tuwe salama.

Mheshimiwa Spika, dunia inayokuja hatari kubwa tutakayokutana nayo ni *virus*. Ndio maana tukisema twendeni tukawekeze kwenye utafiti wa magonjwa ya binadamu na mambo mengine na hizi *virus* na tutafute sehemu ya kuweka maabara ambayo iko katikati porini huko na tuwe na Jeshi lenye nidhamu kuweza kushikilia vitu vya hatari, tunamaanisha na tutafute bajeti ya kutosha tunamaanisha ni njia sahihi ya kuweza kupambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu Jeshi letu wakati wote liko tayari kwa ajili ya kupambana na majanga tukiweza kuwapa *helicopter* za *ambulance*, ndege za *ambulance* ikitokea janga lolote kwa tabia ya Jeshi letu na jinsi ambayo imetuonesha wakiwa na vifaa hivyo na wakiwa na wanasayansi waliobobea, chochote kitakachotokea kuwapata Taifa letu, tutakuwa vizuri sana na watatoka watapambana kwa wakati, na tutapiga na tutakuwa na Taifa linaloheshimika.

Mheshimiwa Spika, ninatamani Tanzania leo ugonjwa wa UKIMWI ukipatikana dawa, akatokea ni Mtanzania amegundua ni zaidi ya *gold* ambayo tunaichimba sasa. Tunatamani Tanzania na sisi tuwe sehemu ya *brain* za dunia. Sisi tukikaa kule Jeshini, Wanajeshi wetu wanaweza wakatikisa kiberiti hivi dunia ikatikisika hawa jamaa wamejenga nini na dunia wakaanza kufikiri Tanzania kinaendelea nini.

Mheshimiwa Spika, hii inawezekana tukitumia fursa ya kuwa na Rais mzuri kama Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ahsante sana nakushukuru sana. *(Makofi/ Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oloyce Godwin Mollel kwa hotuba nzuri kabisa, tunakushukuru sana na

tunakupongeza sana jinsi ambavyo umewapigania watu wa Hai, hakika unarudi ukiwa kifua mbele kabisa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imetekeleza kwa ufanisi miradi mingi ya ujenzi na pia kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi wa askari wetu. Jeshi letu limeendelea kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu na hata ushiriki wa ulinzi katika nchi zingine zenye changamoto ya amani. Napenda kuipongeza Wizara kwa mafunzo ya vijana wetu wa Jeshi la Kujenga Taifa na kuwezesha kuzalisha ajira kwa majeshi yetu na taasis zingine.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuendelea kutoa motisha kwa majeshi yetu kutokana na kazi nzuri na pia kuhakikisha wanakuwa na vifaa pamoja na weledi unaoendana na wakati na mazingira ya sasa. Pia napendekeza wastaafu wa majeshi yetu walipwe mafao yao bila ucheleweshaji na pia kuboresha pensheni yao kulingana na gharama ya maisha ya sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya katika Wizara hii, natambua umuhimu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwenye nafasi za kujiunga na JKT, natambua kuwa nafasi hizi ni chache lakini mgawanyo hauendi sawa kwenye mikoa. Hivyo niombe mgawanyo kuzingatiwa hasa kwenye mikoa ya mpakani ili vijana wanapomaliza vijiji vinakuwa na uhakika wa kuwa na vijana wengi wakakamavu na wenye nidhamu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili Mkoa wa Kigoma unapakana na nchi za Burundi na DRC Congo hivyo ni dhahiri kuwa matukio ya uvamizi kwa wananchi wanaojishughulisha na uvuvi wa Ziwa Tanganyika yalikuwa mengi huko nyuma, lakini sasa hivi kidogo yamepungua lakini doria za mara kwa mara ni muhimu sana.

Kwa kuwa tunazo kambi za jeshi kama vile Kambi ya Jeshi Sibwesa/Lufubu na Kambi ya Jeshi Sigunga, Kambi ya Jeshi Kirando. Kambi zote hizo zipo na zinafanya kazi nzuri tu ya kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto kubwa wanazokumbana nazo ni ukosefu wa makazi ya kudumu, ukosefu wa vitendea kazi kama magari na pikipiki na ukosefu wa boti za kufanya doria kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Waziri alijionea mwenyewe umbali wa kutoka Kijiji cha Sibwesa hadi Kijiji cha Sigunga kwenye kambi ya pili ni kilometa 180; unaweza kuona ni jinsi gani wanajeshi wetu wanavyopata adha ya usafiri na kwenda Kigoma Mjini kwenye huduma za kijamii kama benki na hospitali ni kilometa 250.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Wizara ni kununua boti za mashine angalau mbili za doria, kununua pikipiki angalau sita kwa ajili ya kuwapatia kila kambi pikipiki mbili.

Mheshimiwa Spika, binafsi ushauri wangu kwa leo ni huo niendelee kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi nzuri anayoifanya na nizidi kumuombea Mungu amsimamie katika majukumu yake, Amina.

**MHE. ZUBERI M.KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uhai na kuniwezesha na mimi leo kuchangia Wizara hii. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuongoza vyema majeshi yetu na kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu. Uongozi wake mahiri amelifanya jeshi letu kuwa imara na la kisasa, linalojijengea sifa ndani na nje ya mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza jeshi letu kwa weledi mkubwa na kuliletea sifa na heshima kubwa jeshi letu. Hakika utumishi wake katika nchi yetu ni wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa leo naomba nianze na bima ya afya kwa wanajeshi. Bima ya afya kwa maasikari wetu imekuwa ni changamoto kubwa kwa maaskari pamoja na familia zao. Ukizingatia kuwa sio maaskari wote wanakaa kwenye makambi ya jeshi ambako kuna huduma za afya, lakini pia sio kambi zote zina hospitali bora zenye miundombinu iliyokamilika, ikiwemo na wataalam wa kutosha. Hivyo familia nyingi za maaskari wetu zimekuwa zikiathirika sana na changamoto hii ya kiafya. Hivyo naiomba Serikali kuharakisha mchakato wa bima kwa maaskari wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya JKT kwa vijana; kumekuwepo na mafunzo ya JKT kwa muda mrefu nchini, mafunzo haya hapo awali yalikuwa ni ya kipindi cha mwaka mmoja, lakini kutokana na gharama za uendeshaji muda huo umepunguzwa kati ya miezi sita hadi miezi mitatu kwa vijana wa kujitolea na wale wa kwa mujibu wa sheria. Je, hivi ni kweli kambi hizi za vijana zimeshindwa kujiendesha kiasi cha kuifanya Serikali kufupisha muda wa mafunzo kwa

vijana wetu? Ni yapi basi hayo mafunzo wanayopata vijana hadi washindwe kujitegemea?

Mheshimiwa Spika, lengo la kuwaweka vijana hawa makambini ni kuwafundisha mambo ya ulinzi wa nchi yetu, lakini pia kuwapatia stadi za kazi katika fani za kilimo, ufugaji, ufundi stadi na kadhalika. Naishauri Serikali kuhakikisha kambi hizi kwa kiasi kikubwa zinajiendesha ili kukidhi matakwa ya kuanzishwa kwake na muda wa mafunzo urudishwe ule wa mwanzo wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya mipaka; kumekuwa na migogoro ya ardhi katika sehemu mbalimbali nchini kati ya makambi ya jeshi na wanajamii. Kwa kiasi kikubwa migogoro hii imechangiwa na maeneo ya jeshi kutokupimwa na kukosa hatimiliki. Hivyo naishauri Serikali kupima maeneo yote ya makambi ya majeshi yetu kote nchini. Sambamba na hili ni pamoja na uwekaji wa alama za kudumu zenye kuonekana na watu wa kawaida na pale wanapoonekana raia kuingia kwenye eneo la jeshi basi hatua za haraka za kiustaarabu zichukuliwe kuhamisha raia hawa mapema kabla hawajajenga majengo au mashamba ya kudumu ambayo baadaye huzusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vyeo vya askari; wako maaskari wamekuwa wakihudhuria mafunzo katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuongeza ujuzi, elimu na stadi mbalimbali katika mafunzo ya kijeshi. Lakini bado kuna ucheleweshaji mkubwa kwa baadhi ya maaskari kupata shahada na vyeo vyao vipya kulingana na mafunzo yao. Kuchelewa kuwapa hivi vyeti na vyeo vyao kunaambatana na kuchelewa kwa kupandishwa mishahara yao. Hivyo naiomba Serikali kuangalia jambo hili kwa jicho la ziada ili kuinua mori kwa maaskari wetu na kupunguza manung’uniko miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo hapo juu naomba kuunga mkono hoja 100%.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na wasaidizi wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha kwa utaalam wa hali ya juu katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara kubwa sana yenye maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia Wizara hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na kushirikisha wananchi katika jeshi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu ni jeshi lenye sehemu nyingi sana za uzalishaji na utaalamu ambao mpaka sasa haujawafaidisha wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi ni jeshi ambalo lina vitengo vingi vya uzalishaji mali, kwa mfano uvuvi na kulima. Jeshi hili lina ujuzi mkubwa katika maeneo haya. Lakini bado utaalamu huu haushushwi kwa wananchi. Bado wakulima na wavuvi wa nchi hii wanahitaji ujuzi huu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suali hili ni kwamba wapeleke ujuzi huu ambao jeshi hili linao wa hali ya juu na wa kutosha kwa wananchi, wakulima na wavuvi ili wananchi nao wafaidike na hatimaye kujua hasa kuwa jeshi hili ni lao, Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo Naishauri pia Serikali iboreshe nyumba za askari wetu maana nyingi miundombinu yake imechakaa ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa raia ambao wanapenda kuvaa nguo za jeshi wachukuliwe hatua za kisheria, maana kuna baadhi wanatumia mavazi ya jeshi kufanya uhalifu. Pia naishauri Serikali iwakopeshe askari wetu fedha ili waweze kujenga nyumba zao ili wanapostaafu na kurudi uraiani waweze kuishi katika nyumba zao, maana wengi wanaishi katika makambi. Naishauri Serikali pindi askari akistaafu alipwe pensheni yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali askari wa kike wenye sifa wapandishwe vyeo.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa leo hii kuwezesha kuchangia.

Mheshimiwa Spika, mimi najielekeza zaidi katika mambo matatu na la kwanza Jeshi lisijihusishe kabisa na kazi za kisiasa, kazi yao ni ulinzi wa mipaka yetu na pale panapohitajika tu, hii itasaidia kuleta na kulinda amani ya Taifa hili. Nasema hivi kwa sababu kila panapotokea uchaguzi basi vifaa vya jeshi vinaonekana uraiani, si jambo jema kuleta hofu ndani ya jamii, ni vizuri wahusika wahakikishe jambo hili halitokei hasa kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, la pili, ulinzi wa pamoja, nchi hii itabaki kuwa salama kama tu kutakuwa na ulinzi wa pamoja, mfano wananchi wapewe mafunzo ya kujitetea ili ikitokea jambo la kuathiri maisha mwanachi kujitetea aweze kujitetea yeye mwenyewe na kulisaidia Taifa pale itapobidi. Hali kadhalika mwananchi aweze angalau kutumia silaha inapobidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, la tatu, jeshi la kisayansi na teknolojia; dunia sasa imebadilika sana na teknolojia, pia imebadilika sana kwa kila sekta hasa sekta ya ulinzi, bado jeshi letu liko duni sana kisayansi ya kivita, ni vizuri Wizara kutoa kipaumbele kwa kuwa na vifaa vya kisasa vya kivuta ili ikitokea kulinda Taifa hili lilindwe kwa hali itakavyokuwa, adui akirusha ndege, basi na sisi turushe ndege , akirusha kombora basi na sisi turushe kombora.

Mheshimiwa Spika, tusibweteke na utulivu uliopo, anaweza kutokea muhuni akatujaribu, ni vizuri tujitegemee kwa mambo mbalimbali, kujenga viwanda vya kutengenezea silaha mbalimbali, lakini pia tuwe na uwezo wa kutengeneza zana za kivita.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mungu kwa kuwezesha nchi yetu kumpata Rais Dkt. J. P. Magufuli mwenye maono ya mbele ya tunakokwenda. Mungu ampe maisha marefu na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na makamanda wote kwa kazi nzuri waifanyayo ya kumuunga mkono Jemadari wetu wa nchi, kwa ulinzi wa nchi na kudumisha amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wanajeshi wastaafu kupatiwa viwanja vya kujenga nyumba zao nje na maeneo ya Jeshi ambayo wanatumia wakiwa wanapakana na wananchi wetu, kwani wanaleta mgogoro kutokana na maeneo mengi kutokuwa na upimwaji wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa zoezi linaloendelea la kupima maeneo ya Jeshi, bali tunaomba kasi ya utekelezaji kuongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maamuzi ya Jeshi kuwa na utaratibu wa kujipanga kuwa na chakula cha

kutosha, hivyo nashauri Serikali kushirikiana na Wizara hii kujenga ghala kuu la uhifadhi chakula ambacho kitawasaidia maaskari wa aina yote pindi ikitokea mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ndugu zetu wa Hazina kwa maana ya Wizara ya Fedha kutoa bajeti iliyokamili ili wakamilishe miundombinu ya aina yote husika katika kuliimarisha Jeshi letu na kwenda na sayansi ibadilikayo ndani ya ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kwa ngazi mbalimbali kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa baraka, ulinzi, usalama na mapendo makuu kwetu sote na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sisi Watanzania tuwe na imani thabiti kumwomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliondoshe janga la Corona duniani kote. Aidha, sisi viongozi wa kuchaguliwa na watendaji mbalimbali kila mmoja kwa nafasi zetu kuendelea kuelimisha na kutafsiri maelekezo ya Serikali kuhusu kupambana na janga hili la Corona. Tuendelee kuwaombea ndugu zetu waliotangulia mbele za haki kwa Mwenyezi Mungu ili awapokee katika ufalme wake.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini natoa salaam za pongezi kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, kwako Mheshimiwa Spika, viongozi na waandamizi wote wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya CCM. Hongera sana Serikali ya awamu ya tano.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu wa kuishauri Serikali kupitia Wizara hii. Kwanza ninaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga makao makuu ya Wizara ya Ulinzi Kikombo, Dodoma, hivyo basi

Serikali itoe fedha za mradi huu ulio muhimu kwa ajili ya Taifa letu.

Pili, kwa kuwa kupitia taarifa ya Kamati baadhi ya maeneo ya wananchi yaliyotwaliwa na jeshi nchini bado hayajalipiwa fidia hali inayoleta mahusiano yasiyo mazuri kwa majeshi yetu na wazawa, kwa hiyo, Serikali itoe fedha zilizoombwa katika bajeti hii kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa vijana wengi wanaojiunga na JKT nchini wana mawazo ya kuajiriwa jeshini. Serikali iandae mazingira ya ajira za ulinzi kwa wahitimu hao katika mashirika ya umma, binafsi, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa. Kwa mfano ni nafasi za ulinzi ni ofisi za Idara za Halmashauri, shule za sekondari, msingi na mamlaka mbalimbali. Hali hii itadhibiti uhalifu na kuimarisha ulinzi kwani kwa sasa wanaolinda ni vibarua wasio na taaluma nchini.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ifanye utafiti wa fursa zilizoko katika mikoa mbalimbali za kuanzisha matawi ya Shirika la SUMA JKT kwa ajili ya kuanzisha matawi hali itakayochochea fursa za ajira kwa wahitimu wa JKT. Kuhusu uzalishaji wa bidhaa kutoka SUMA JKT, Mzinga na Nyumbu uendane na ubora wenye ushindani wa soko la ndani na nje ya nchi. Pia naipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa jinsi wanavyolinda mipaka ya nchi yetu ukilinganisha na nchi zinazotuzunguka katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua nafasi hii kukupongeza sana kwa jinsi uliyotuongoza kwa miaka mitano hii, busara na hekima zako zimetufikisha hapa tulipo Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana ya kuongoza nchi hii na kuwa Jemadari Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana naendelea kuzitoa kwa Waziri wa Ulinzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi nzuri, usikivu wake na busara za kuongoza Wizara hii nyeti mno. Nimpongeze Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie yafuatayo na nikianza na mafunzo ya JKT kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa kurudisha haya mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na pia kuwafanya vijana wanaohitimu kidato cha sita pia kuhudhuria mafunzo haya. Kwa kweli yamewajengea ujasiri vijana wetu pia mafunzo haya yamekomesha hata mifumo vyuoni.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu kwanza vijana hawa wafundishwe mafunzo ya ufundi wa vyuo vya *VETA* ili wakihitimu waweze kuajiriwa katika viwanda vyetu sababu Tanzania tunajenga uchumi wetu kwa kutegemea viwanda vidogo vidogo na vya kati, lakini mafundi mchundo wanahitajika sana katika viwanda vyetu. Pia itawasadia sana vijana wetu kujiajiri na kuweza kuajiri hata wengine wakiwezeshwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitoe pongeze kwa SUMA JKT, wamekuwa wakitoa ajira mbalimbali kwa vijana wanaohitimu mafunzo haya ya JKT. Hongera sana na wamekuwa wakifanya kazi zao vizuri sana na kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu vijana hawa walipwe mshahara mzuri na stahiki zao ili SUMA JKT iwe kisima cha ajira kwa vijana wetu. Nimeona sasa hivi hawa vijana wakiwafuata Wabunge au kuwaaandikia *message* tuwasaidie walipwe vizuri. Niombe viongozi wanaohusika na jeshi hili basi washughulikie hili jambo ili Tanzania iwe nchi ya kuigwa na mataifa mengine katika kuwajenga vijana. Nimechangia yote haya sababu na mini ni mmoja wa Wabunge waliopata bahati ya kuhudhuria mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za askari wetu; niipongeze Serikali kwa ujenzi mzuri mno wa makazi ya askari kwa mikoa yote nchini. Ushauri wangu wanajeshi hawa kutokana na kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya, uwepo utaratibu wa kupatiwa mikopo ya nyumba wakikaribia kustaafu ili wakistaafu waishi maisha mazuri na heshima ya kutumikia jeshi letu kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze wanajeshi wetu kwa kazi nzuri wanazozifanya wananapopatiwa nafisi za uteuzi na hakika Mheshimiwa Rais uongozi wako unapewa maono makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pia hata miradi mingi uliyolipatia jeshi letu limefanya vizuri kama ujenzi wa uzio wa Mererani, Arusha na miradi mingine mingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja 100%.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri na timu yake yote ya Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza vijana wetu waliofanya kazi kubwa sana kujenga ukuta wa Mererani ili kulinda madini yetu na pia wanajenga ukuta wa Ikulu hapa Dodma. Mheshimiwa Rais alitoa agizo vijana wote walioshiriki kujenga kuta hizi mbili wote wapate ajira ya Serikali.

Hata hivyo vijana wengi walifanya kazi hii nzuri hadi kusaidiwa na Rais na kuwaaahidi ajira, wengi wameondolewa jeshini na kurejeshwa majumbani kwa visingizio kwamba wanaumwa wakati wamekuwa na jeshi zaidi ya miaka mitano na wametumwa mara kadhaa hawakukutwa na ugonjwa. Ila baada ya Rais kuagiza waajiriwe wameonekana wanaumwa na wameingizwa wengine. Huu ni uonevu, ni ubaguzi wa hali ya juu. Kwa nini wenye mamlaka wamepuuza agizo la Rais na badala yake kuwarejesha majumbani kwao?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi limeanzisha Kampuni ya Ulinzi na anachukua *tender* ya kulinda maeneo mbalimbali na wanafanya kazi nzuri. Jambo la kusikitisha hawa vijana walioajiriwa na SUMA JKT kwa ajili ya kulinda, wanakesha kwenye malindo usiku kucha lakini mshahara wao ni kidogo sana haulingani na kazi kubwa wanaofanya kwenye mazingira magumu sana. Kwa nini SUMA JKT hawalipi vijana hawa jirani unaolingana na kazi wanaofanya?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na migogoro mingi ya ardhi kwenye maeneo ya Jeshi na Wananchi wanaoishi jirani na jeshi, maeneo mengi hapa nchini. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo yote ya jeshi yanapimwa na kuwekwa alama za kudumu ili kuondoa migogoro ya kila siku ya ardhi kwenye maeneo ya jeshi?

Mheshimiwa Spika, JKT wamekuwa wanaatengeneza samani *(furniture)* nzuri za ndani ambazo ni chanzo cha mapato kwa JKT. Serikali ina mikakati gani kuwezesha SUMA JKT kuongeza mtaji ili waweze kutengeneza samani kwa wingi na kusambaza nchi nzima na kununua samani dhaifu kutoka China?

**SPIKA:** Sasa tunaanza na upande wa Waheshimiwa Mawaziri na tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo na atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende sana kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uhai tumeweza kudiriki katika kushiriki katika kikao hiki cha Bunge na miaka mitano sasa ndiyo inaisha na hakika Mwenyezi Mungu ametufanyia mambo makubwa sana, tuna kila sababu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa wema wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuko ndani ya Bunge, binafsi naomba sana, wewe umekuwa kiongozi wa aina yake

na nadhini kwa sababu umepikika muda mrefu sana. Mheshimiwa Spika wetu nadhani ni miongoni mwa Maspika saa nyingine wachache waliopita katika mkokotoo wa aina mbalimbali ndiyo maana umekuwa mahiri na unatuweza kutuvusha hata wakati mwingine hata upepo ukivuma vipi, lakini Bunge lako limekuta *stable,* hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Rais, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopitia vyombo vya habari kuanzia juzi, jana na leo kuna habari nyingi zinazungumzwa duniani na hii yote ni kwamba mimi naamini ni Rais wa chaguo la Watanzania ambaye Mungu ametupa kwa kipindi hiki. Kwa kweli binafsi tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajumbe wamezungumza hapa wa Bunge lako hili kujadili maoni ya Mheshimiwa Rais na maono yake, amekuwa Rais wa kipekee kwa kweli, naomba nizungumze ukweli na ndiyo maana nilikuwa na Wakuu wa Mikoa siku moja tulipokuwa tunakagua *Standard Gauge* nikasema hata Rais ajae ana changamoto kubwa sana wa miaka hiyo atakayokuja kuvaa atatoka na swaga la aina gani, yote mkubwa huyu amemaliza. Kwa kweli tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupa Rais huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mwinyi na Wizara yake, kwa kweli kwa kazi kubwa anayofanya na jeshi lake kwa ujumla wake ni Wizara imetulia sana na hakika leo hii tukitimiza mwaka huu wa tano Wizara hii ni muhimu sana na hasa kutokana na kazi kubwa aliyofanya Rais wetu. Maana ukiipima Tanzania ndani ya miaka mitano kuna mambo yanapaswa kulindwa na hasa jeshi letu lazima liwe jeshi madhubuti na ndiyo maana nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi kubwa anayofanya.

Mheshimiwa Spika, leo hii Watanzania wanashuhudia hakuna sehemu iliyoachwa katika Taifa letu hili. Ukizungumzia suala zima la umeme kwa ndugu yangu, kaka yangu

Mheshimiwa Kalemani pale, kazi kubwa iliyofanyika ya ujenzi wa miundombinu hii lazima ilindwe katika usalama wa nchi yetu. Siyo wote watakaotamani, suala zima la uwekezaji katika suala zima la umeme wa pale Rufiji siyo wote watakaotamani. Wengine wanataka jambo lile liharibike katika *fraction of second,* siyo wote watakaotamani, watu wa ukanda wa kati hapa Mheshimiwa Kalemani amepambana ujenzi wa msongo wa umeme wa *KV* karibuni 400 umejengwa, wengine wanatamani miundombinu ile iharibike watu wapate *frustration. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kule hali yao ilikuwa tia maji tia maji hata umeme hawana wanatumia majenereta, leo hii nchi yote imekuwa *connected* siyo wote wanaotamani, lazima jeshi liweze kusimama vizuri. Nchi yetu tunaishuhudia jinsi gani ujenzi wa reli hii, tutazame ndugu zetu wa jirani hapa miundombinu yao ya *Standard Gauge* iliyojengwe halafu *compare* na sisi. Fedha za walipa kodi wa Tanzania, jeuri ya Watanzania kupitia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, reli ya mfano inayojengwa *Standard Gauge* ambayo wengine wanatamani jambo lile liharibike, siyo wote wanaotamani, lazima vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, jeshi letu liwe imara. Lakini ukiangalia katika upande mwingine nchi yetu imekuwa na kadhia kubwa sana. Ajenda ya ndugu yangu hapa Mheshimiwa Dkt. Biteko suala la madini jinsi gani nchi yetu ilikuwa inapoteza rasilimali madini, lakini nchi ya Tanzania sasa hivi inaanza kiigizo kizuri kwa ajili uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaweza wakapatikana watu wabaya kuharibu mifumo hii yote tuliyokuwa nayo, lazima tuwe na jeshi imara la ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda katika nyanja mbalimbali leo hii watu wote wanashuhudia jinsi gani uwekezaji katika sekta ya afya tumezungumza sana humu

ndani. Nchi yetu ilikuwa inataabika, nakumbuka wakati ule Mheshimiwa Kigwangala na Mheshimiwa Ummy Mwalimu wanahangaika pale ukiangali pale Hospitali yetu ya Muhimbili. Lakini kazi kubwa iliyoshushwa mpaka huku chini leo hii kila mahali ambapo jambo halionekani lilikuwa linaonekana siyo jambo la kuwezekana leo hii kila ukienda mpaka vijijini kule uwekezaji mkubwa umefanyika, siyo wote wanaotamani. Tunaweza tukapata waharibifu wachache wakataka kuiharibu nchi hii lazima tuwe na jeshi imara katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi kubwa anayofanya katika taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulishuhudia leo hii watani zangu Wanyamwezi wa Tabora na Sikonge kule, uwekezaji ambao Mheshimiwa Dkt. Mpango anahangaika pale na ofisi yake na dada yangu Mheshimiwa Kijaji. Leo hii maji yanakuja yanakwenda Tabora watu wanaona kazi inayofanyika na siyo mradi huo peke yake isipokuwa nchi nzima kazi inayofanyika, hivi ni kweli watu wote watatupenda? Wengine kutoka ndani na wengine kutoka nje watatamani mambo hayo yaharibike.

Kwa hiyo, lazima tuwe na jeshi imara litakaloweza kulinda nchi yetu katika vipindi vyote. Kwa hiyo, binafsi naomba kuunga mkono bajeti hii kwa nguvu zote, lakini kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa *leadership* yake anayotuongoza katika taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa letu leo hii kama ninavyofahamu siyo kisiwa, dunia nzima imekumbwa na tatizo la ugonjwa wa Corona, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa *leadership* yake. Mara nyingi tunaambiwa *be yourself* katika uongozi, kuwa kama ni wewe.

Mheshimiwa Spika, Rais Magufuli ameamua kuwa yeye kama yeye kuliongoza Taifa letu hili kipindi hiki, tunampongeza sana na naomba Watanzania wote tuungane wote na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niwapongeze Watanzania na hasa kutekeleza ile siku ya nyungu, wiki ya nyungu niwapongeze sana Watanzania, leo hii ndiyo tunakamilisha siku ya sita katika ile wiki yetu ya nyungu. Niwapongeze Watanzania wote, wasanii, viongozi, wanakijiji, kila mtu katika eneo lake tumefanya kweli kweli, hii vita haichagui silaha. Wewe piga nyungu yako vizuri, kunywa *juice* yako ya tangawizi, kula matunda yako na bahati nzuri kuna habari nilizozipata katika *message* wanasema bwana tumejaribu nyungu inaonekana kwamba siyo ugonjwa huu peke yake, isipokuwa inarekebisha na mambo mengine. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, watu wamesema kabisa kijasho kikitoka, kikitoka na kule basi shughuli inakuwa pevu kweli kweli, ninashukuru sana ndugu zangu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama Taifa na kweli tuna kila sababu ya kujivunia katika eneo hilo lakini ndugu Watanzania tufanye maombi sana. Katika maombi mara nyingi sana tunaambiwa tuigize kipindi cha baba yetu wa imani Ibrahim. Na mimi namuomba sana Mungu atunusuru katika janga hili, Mungu wakati Ibrahim wa kipindi kile anaingizwa katika moto au Abraham basi nikasema ewe moto kuwa salama na amani kwa Ibrahim. Tuendelee kuomba Mungu hivi virusi vya Corona viwe salama na amani kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Jafo maarufu Mzee wa Nyungu. *(Makofi/Kicheko)*

Ushauri wako umepokelewa kona zote za nchi yetu, kwa kweli tunakushukuru sana hata waliokuwa hawajui kufukiza ni nini sasa wanaelewa wamekuwa mabingwa na wameelewa kuna tofauti ya sufuria na nyungu, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango sijakupangia muda, atafuata mtoa hoja, ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi nianze pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kuchangia kwenye bajeti hii muhimu sana. Naomba nianze kwa kweli na mimi kuungana na wenzangu kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, yaani ni chuma kweli kweli, upeo wake hauna mfano, tulimhitaji sana kiongozi huyu na Mungu akatupatia. Mungu amlinde sana kiongozi wetu, ailinde na familia yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Ulinzi, wote wamesema hapa ni Waziri mtulivu sana, msikivu kweli kweli na ndiyo maana hatuoni shida sana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze *CDF* na wasaidizi wake wote wanafanya kazi nzuri sana, mchango wa jeshi letu ni mkubwa sana katika Taifa, sana ndiyo maana tunalala usingizi. Lakini mnaona jeshi letu kila mahali kwenye majanga lipo, wananchi wetu wote wanafaidi sana huduma za jeshi kwenye hospitali za kijeshi, lakini pia ujenzi wa nyumba za askari. Vilevile siyo tu hivyo hata kwangu kule kwenye mapato jeshi limekuwa ni la msaada mkubwa sana ikiwa ni pamoja na ujenzi ule ukuta kulinda ile mali yetu pale Mererani. Kwa hiyo, kwa kweli niseme naunga mkono hoja na kuwapongeza sana kwa kazi hii nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nilitaka tu nisisitize kwamba kwa upande wa Wizara ya Fedha tunajitahidi sana kutoa kipaumbele cha juu kibajeti kwa Wizara hii nyeti na ndiyo maana mpaka kufikia mwezi Machi Jeshi la Wananchi wa Tanzania - Fungu 38 mpaka kufikia Machi tumekwisha kuwapatia asilimia 79.2 ya bajeti yao. Lakini pia upande wa JKT - Fungu 39 tumekwisha kuwapatia bajeti asilimia 86.8 ya bajeti yao na kwa upande wa Wizara yenyewe Fungu 57 tumekwisha kuwapatia asilimia 83.2 ya bajeti yao. Kwa hiyo, ukizijumlisha zote tuna wastani wa asilimia 80.77 ya bajeti ya Wizara hii tumezitoa na hii ni kuthibitisha tu kwamba kwa kweli

tunazingatia umuhimu wa Wizara hii kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningetaka kulisemea ni suala la fidia, niseme tena kwamba tunatoa kipaumbele cha juu kabisa kuhakikisha kwamba tunalipa fidia kwenye maeneo ambayo yametwaliwa na jeshi kwa matumizi ya kijeshi na niseme tu kwa mfano, kwa upande wa mwezi Mei peke yake, *exchequer* ya mwezi Mei tunatoa shilingi bilioni 8.18 kwa ajili ya kulipa fidia maeneo mbalimbali yaliyotwaliwa na Jeshi. Lakini siyo tu hivyo, tunatoa pia shilingi bilioni 2.11 kwa ajili ya kulipa hati za madai za wakandarasi kwenye miradi ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pengine kwa taarifa upande wa eneo lile la jeshi pale Ilemela kwa mwezi Mei tunatoa, wao walileta maombi ya shilingi bilioni 6.195 tulipofanya uhakiki tukakuta yanayostahili kulipwa ni shilingi bilioni 6.165 na haya nikuahidi na Bunge lako kwamba tutayalipa kabla ya tarehe 30 Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa *exchequer* ya mwezi wa tano kwa ajili ya Ilemela peke yake tutatoa shilingi bilioni 3.53; upande wa Arushi Jiji na *DC* tunatoa pia shilingi bilioni 3.53 na upande wa *Musoma Municipal Council* tunatoa shilingi bilioni 1.11. Nasema hizi tu kama mfano kuthibitisha kwamba tunatoa kipaumbele cha juu sana kuhakikisha kwamba maeneo yanayotwaliwa na jeshi basi tunaondokana kabisa na madai ya wananchi wetu wambao wanapisha kazi za jeshi kufanyika katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nyumbu pengine sitakuwa na takwimu lakini niseme kwamba mimi na wenzangu pale Wizara ya Fedha tunaamini kabisa kwamba taasisi ile ni ndoto ya Baba wa Taifa letu Hayati Mwalimu Nyerere na kwa hiyo tutafanya kila liwezalo kuhakikisha kwamba tunaipelekea fedha taasisi ile kadri mapato yanavyoturuhusu, kwa hiyo, tunazingatia ushauri ambao tumeusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maduka ya wanajeshi ilisemwa hapa kwamba fedha hazitoki kwa wakati. Niseme kwa kweli tunafanya jitihada kubwa sana kulipa hizi posho za fidia kwa wale waliokuwa wanatumia yale maduka ambayo kama tulivyosema nyuma yalikuwa yanafaidia watu wachache na askari wengi hasa wale *rank unfilled* walikuwa hawafaidiki na kumbe tunawalipa posho zao moja kwa moja kwenye akaunti zao ili kuhakikisha kwamba kweli kila mwanajeshi ananufaika. Kama kuna ucheleweshaji kwa kweli tunakuwa tumebanwa, lakini kila baada ya miezi mitatu tunahakikisha kwamba posho zao zimelipwa.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika kwa upande wa wastaafu wa jeshi masuala ya *pension,* nisisitize tena kwamba kama Serikali tunatambua sana mchango mkubwa wa askari wetu ambao sasa wamestaafu. Kwa hiyo, tunafanya jitihada kuhakikisha kwamba wanapata stahili zao na *pension* zao ili waweze kupumzika baada ya kulitumikia taifa vizuri.

Mheshimiwa Spika, leo kwa kweli nimefurahi sana, mjadala ambao mmeusimamia ni mjadala mzuri sana na mimi ningetamani kwamba Wabunge wenzangu wahakikishe kila mtu anapata *Hansard* ya majadiliano haya. Ushauri uliotolewa ni mzuri sana kuhusu jeshi kupewa fedha za kutosha kufanya utafiti mbalimbali wa magonjwa, lakini pia mambo mbalimbali *including* masuala ya *micro-biology.* Na mimi nipende kusema kwamba sijui kama nipata *privilege* tena ya kupata Uwaziri mezani lakini katika *handing over notes* zangu nitasisitiza mambo haya yapewe msukumo na atakayekuwa msaidizi wangu kibajeti. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme neno lingine pengine la mwisho kuhusu tafiti za jeshi. Ni kweli kabisa haziwezi kupelewa *COSTECH.* Kwa hiyo, tunapokea ushauri na sana sana ni kusisitiza tu kwamba Wizara yangu itaendelea kuelekeza fedha kwenye utafiti ndani ya jeshi lenyewe na hasa kwenye vyombo vyake ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaendelea kubaki salama kama taifa na tunasonga mbele, lakini jeshi likiwa pia ndiyo chachu au *centre* ya *excellence* ya tafita ambazo zitahakikisha kwamba tunaendelea kuwa

salama katika ulimwengu ambao unatawaliwa na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono haja na nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha ahsante sana kwa hotuba nzuri sana yenye *analysis* zinazowatia moyo Waheshimiwa Wabunge ikiwa ni pamoja na masuala ya fidia na mengine yote uliyoyaainisha tunakushukuru sana sana sana.

Sasa mtoa hoja nakukaribisha, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU - K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nianze na mimi kwa kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha mjadala huu wa hotuba ya bajeti ya Wizara hii kwa viwango vya hali ya juu kama ilivyo kawaida yako, hongera sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa michango yao iliyotolewa hapa Bungeni wameungana na hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri zenye mfano wa kuigwa ndani ya Bara la Afrika. Lakini tunasema kwamba hata katika mataifa mengine nje ya Bara la Afrika Rais wetu amekuwa ni kinara na amekuwa ni kioo cha viongozi waliochipukia katika karne hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu naweza nikasea kwamba tunamuhitaji Dkt. Magufuli Rais wetu leo kuliko tulivyomuhitaji jana na tutamuhitaji zaidi kesho kuliko hata tunavyomuhitaji leo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu

kwa zawadi ya kiongozi huyu mahiri, shupavu, mchamungu ambaye analipeleka taifa hili kwa maono makubwa ya mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo ni kwa sababu tunapozungumzia ulinzi na usalama wa mipaka ya Taifa letu, ulinzi wa Taifa hili pamoja na kazi nzuri inayosimamiwa na Dkt. Mwinyi, lakini na majeshi yetu yakiongozwa na *CDF* na viongozi wengine ndani ya Jeshi, lakini kiongozi namba moja ni Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye ametufikisha mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaungana na Watanzania wote wale wenye nia na mapenzi mema ya nchi yetu ambao wanampa moyo na kum-*support* Rais wetu asonge mbele na aendelee kuwa kuwa imara kwa ajili ya Taifa hili na kwa kweli watanzania hao wanafanya jambo jema sana.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kwa niaba ya Mheshimwia Dkt. Mwinyi kuwashukuru kwanza Kamati iliyochambua bajeti hii kwa maoni na ushauri wao mzuri ambao tumeupokea na ninaomba kukuhakikishia kwa maelekezo niliyoyapa kwenye Dkt. Mwinyi majibu ya hoja zote yataandikwa pia kwa maandishi na Wabunge watapatiwa majibu ya hoja hizo zote kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitakwenda kujibu baadhi ya hoja na baadae utaniruhusu niweze kuliomba Bunge lako lilidhie Jeshi letu lakini na Wizara hii iweze kupokea mapendekezo ya fedha kama nilivyoyasoma kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, ukiutizama mjadala wa leo kwanza unalipongeza Jeshi letu kwa asilimia 100 kwamba ni Jeshi imara na linafanya kazi kubwa sana, lakini mjadala huu ukiuweka kwa mafupisho yake umedhihirisha kabisa kwamba Watanzania wana imani ya mabadiliko makubwa ya kisayansi, kitafiti na kiteknolojia kupitia Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. Lakini ukiangalia pia mchango huu katika

mawanda yake umedhihirisha kwamba Jeshi letu limefanya kazi kubwa ndani ya nchi yetu na nje ya nchi ya Tanzania na kujipambanua kuwa ni miongoni mwa majeshi machache yanayofanya vizuri ndani ya Afrika na nje ya Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Spika, lakini michango hii yote ukiitazama imeonesha ni kwa kiasi gani Jeshi letu limekuwa ni kimbilio la wananchi na ndiyo maana ni Jeshi la Wananchi na hasa ukipata mifano halisi wakati wa majanga mbalimbali Jeshi hili limekuwa mstari wa mbele kushirikiana na Watanzania na kuonesha dhahiri, shahiri kwamba Jeshi letu ni Jeshi la Watanzania ni jeshi la wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mukutadha wa mawanda na maudhui hayo niliyoyasema, ninaomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba jeshi hili litaendelea kufanya kazi kwa weledi na kwa utii mkubwa kwa Amiri Jeshi Kuu kwa kuzingatia taratibu na misingi ya Sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likiongozwa na *CDF* mwenyewe, makamanda wengine, lakini likisimamiwa na Amiri Jeshi Mkuu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikipitia hoja ambazo ziliibuliwa hapa ya kwanza ilikuwa ni kiu ya Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba baada ya Serikali kuhamia Dodoma basi ujenzi wa Makau Makuu ya Jeshi la Ulinzi kule Kikombo kila mtu ilikuwa ni kiu yake kuona ujenzi huo unaanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Amiri Jeshi Mkuu na Rais wetu kwa kufanya maamuzi ya kuhamishia Serikali Dodoma kwanza na wote ni mashahidi Serikali imekwishakuhamia Dodoma. Sasa hajaishia hapo tu tayari Wizara ya Fedha imeshatoa fedha za kitanzania takribani shilingi bilioni 10 na tumekwisha kuanza kujenga Makao Makuu ya Jeshi hapa Dodoma eneo la Kikombo na mkakati wa Serikali ni kutumia miaka miwili ujenzi umeanza mwezi Machi, 2020 tunatarajia utakamilika mwezi Machi, 2022. Kwa

hiyo, Waheshimwia Wabunge na Wajumbe wa Kamati jambo hili limefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Wabunge na ushauri wa Kamati kwamba kuna hata ya kujenga hospitali kubwa ya Kanda ya Jeshi hapa Dodoma na yuko mfadhili ambaye alikuwa amejitoa kutusaidia kujenga mradi huo, lakini Kamati imetushauri kwamba tupokee fedha, lakini ujenzi ufanywe na Jeshi lenyewe, tunapokea ushauri huo na utafanyiwa kazi ndani ya Serikali na utafanyiwa kazi ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, lakini tumepongezwa hapa Wizara ya Fedha, lakini Amiri Jeshi Mkuu Rais wetu kwa kujali bajeti ya Wizara hii na kuweza kuitoa katika kiwango kikubwa tunapokea sana pongezi hizo na Waziri wa Fedha amezungumza hapa vizuri na kuonyesha nia njema ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 bajeti hii imeongoeza mpaka kuwa shilingi trilioni 2.1 toka shilingi trilioni 1.8 kwa mwaka 2019/2020.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hiyo ni nia njema tunaonyesha dhahili kwamba Serikali kwa kweli tunajali Wizara hii kwa sababu kwa kweli ni msingi wa maendeleo, amani, utulivu umoja, ulinzi wa Taifa ndiyo msingi wa maendeleo endelevu ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameonesha iko haja na kiu kubwa ya kuona kwamba JKT inaongeza vijana wengi na hasa wale wanaoenda ili kwenda kujitolea, kwa sababu ni eneo pekee tutakalojenga uzalendo kwa vijana wetu wa Tanzania, waitambue nchi yao vizuri, wawe tayari kulitumikia Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, kwa kwa hiyo tumekubaliana na ushauri huo kwa mwaka 2021 Jeshi limejipanga, linatarajia kuchukua vijana kwa mujibu sheria takribani kama 21,000, vijana wa kujitolea 12,000 itachukua jumla ya vijana 33,000 na hiyo yote ni kwa miongozo ambayo inatolewa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini mmetuambia tuwe na mkakati wa ziada kwenye mapambano haya dhidi ya Corona, tumekubali hapa kwamba kwa kweli tunahitaji kwenda kutafakari ndani ya Serikali Waziri wa Fedha ameiweka vizuri sana, lakini tutasaidiana na Jeshi letu, tunasema tunaliamini Jeshi letu kama kitivo cha utafiti kinafanya vizuri tumekuwa mashuhuda Nyumbu na Mzinga wamefanya vizuri sana sana katika ubunifu wa teknolojia ya hali ya juu, hawataweza kushindwa kufanya utafiti na ubunifu katika vita hizi za kibailojia ambazo zinakuja kwenye ulimwengu wa sasa.

Mimi nadhani tuwape nafasi na kwa kuwa wako hapa wanatusikia nina uhakika kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano na aina ya Jeshi tulilonalo watafanya miujiza mikubwa ndani ya Taifa na ulimwengu mzima.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunakubaliana na ninyi Waheshimiwa na ninamshukuru Mheshimwia Waziri wa Fedha amechomeka hapa kama atarudi, asiporudi kwenye Wizara hiyo amesema ataacha ajenda hiyo mezani kwake kuhakikisha kwamba tunawezesha mashirika haya yanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge niwape tu *comfort* kwamba kwa mwaka huu wa fedha za maendeleo kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 tuna shilingi bilioni kama 150. Kwa hiyo, ndani ya Serikali na ndani ya Wizara tumeamua shilingi bilioni 11.5 hizo zianze moja kwenye utafiti katika mashirika haya mawili.*(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha kukurahishia tu hapa sisi ndani ya Wizara tumeshafanya maamuzi, sasa wewe kazi kwako kutusukuma hizi shilingi bilioni 11.5 zianze tu kazi haraka sana ya utafiti twende kwenye viwanda, twende kwenye utafiti huo wa kibaiolojia, twende kwenye tafiti nyingine na huo ni msimamo wa Rais wetu na tumemuona Rais wetu anapambana mapambano haya hadharani bila kuficha, tena bila kumuonea aibu mtu yeyote ana nia ya mabadiliko na ninaamni kabisa Jeshi watatusaidia.

Mheshimiwa Spika, kumezungumza hapa masuala ya fidia, namshukuru Waziri wa Fedha ameyaweka vizuri sana kwenye fidia zile ambazo zitaendelea kutolewa kwenye mwaka wa fedha huu 2019/2020, lakini Waheshimiwa Wabunge naomba niwahakikishie kwa mwaka 2020/2021 Wizara imeamua kutenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya fidia kwenye maeneo yaliyotwaliwa. Kwa hiyo, tunafidia kwa bajeti inayoisha ya mwaka huu wa 2020 lakini 2020/2021 tumetenga tena shilingi bilioni 20 kuhakikisha tunaendelea kufidia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la ukarabati wa nyumba za wafanyakazi wa Wizara; Wizara imejipanga tutahakikisha kwamba tunafanya kazi hiyo, lakini kuna ukarabati na ujenzi wa nyumba za askari wenyewe na hilo nalo kwenye bajeti ya maendeleo Wizara imejipanga na tutafanya hiyo kazi, tunachotaka ni kuwa na Jeshi imara, lakini Jeshi imara ni lazima lipate huduma bora na tumeshuhudia Rais wetu akisisitiza na kuonesha kwa mifano umuhimu hata wa kutumia SUMA JKT kuhakikisha kwamba wanatengeneza miundombinu rafiki kwa ajili ya wanajeshi, lakini kwa ajili pia ya mahitaji mengine. Na kweli tupongeze sana wenzetu wa SUMA JKT wamefanya mageuzi makubwa sana kwenye Sekta ya Miundombinu katika nchi yetu ya Tanzania, kwa kweli wamefanya kazi kubwa tunawapongeza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika bajeti ya mwaka 2020/2021 Serikali yetu inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli imeamua kama nilivyosema kwenye hutuba yetu kwamba la kwanza itahakikisha inaimarisha Jeshi na dhana na vifaa vya kisasa tena vyenye mawasiliano na rasilimali watu, jambo hili litafanyika kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeamua kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji wa kazi kwa wajeshi wenyewe ikiwemo mafunzo tena mafunzo bora na ya kisasa kwa kutumia dhana na miundombinu ya kisasa. Kwa hiyo, hiyo ni azima ya Serikali kwenye bajeti ya mwaka huu. Lakini tumeamua kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga

Taifa na kulitumia vizuri na hasa kuwachukua vijana ili wakapate mafunzo ya stadi za kazi kama mlivyotushauri Waheshimiwa Wabunge na jambo hili kwa sasa linahitajika sana na hasa kwa tatizo la ajira. Kwa hiyo, Jeshi letu JKT inaweza ikatumika kama ni njia mbadala ya kuwaandaa vijana wetu ili wapate fursa ya kwenda kujiajiri, kuwaajiri wenzao na kuongeza kujenga uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema mwanzo bajeti yetu imejipanga kwenye masuala ya utafiti, lakini tumejipanga pia kuendelea kuimarisha shughuli zote ambazo zinaendana na mahusiano ya kijamii katika kusaidiana na wananchi, lakini tumesema kwamba tutaendelea kupima na kutathimini hali ya Jeshi letu la kulifanya Jeshi letu liendele kuwa ni Jeshi la kisasa, Jeshi imara, Jeshi la kupigiwa mfano katika ulimwengu wa leo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba baada ya kusema hayo niwashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa mdomo hapa ndani wapatao kama 13, lakini vilevile niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi wapatao kama saba na ninaomba kusema kwamba kwa unyeyekevu mkubwa tunaendeleea kuungana na Wabunge kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi nzuri anayoifanya weledi wake utulivu, uzalendo katika kulitumikia taifa lakini kuongoza Wizara hii muhimu sana katika taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja bajeti ya fedha ambayo nimeisoma kwenye hotuba yangu muda siyo mrefu uliopita baada ya kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge sasa ikubaliwe na Bunge lako tukufu na iweze kupitishwa ili Wizara hii iweze kwenda kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba na hati idhini iliyotoewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Muhagama hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana na tunakupongeza sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya. Sasa Waheshimiwa Wabunge wajibu wangu ni kuwaomba sasa muufanyie uamuzi hoja hii ambayo imetolewa na Mheshimwia Waziri wa Nchi kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 38 - Ngome……………………...……..Sh.1,607,164,984,000
Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa………..........Sh. 350,234,958,000
Funge 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la
Kujenga Taifa.............................................……Sh.19,634,547,000

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 38 - Ngome……………………......……..Sh. 10,000,000,000
Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa……..............Sh. 4,000,000,000
Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la
Kujenga Taifa..................................................Sh. 150,000,000,000

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kura ambazo zimeshapigwa ninazoziona kwenye ubao wangu hapa ni kwamba walioafiki wameshinda, tena kwa kura nyingi kabisa ambazo rekodi yake haijawahi kupatikana inaonesha jinsi ambavyo Bunge letu linaunga mkono Jeshi na hakuna aliyeomba kutokukamata shilingi hiyo ni *standing ovation* ya Wabunge kuna imani kubwa waliyonayo kwa Jeshi letu na kwa niaba basi ya Bunge zima nimpongeze sana Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wetu kwa kweli majeshi yote yametulia, ndiyo maana watanzania tunalala usingizi kwa amani kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawapongeza sana wahusika wa vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama na kipekee Jeshi letu tumpongeze Mheshimiwa Waziri Hussein Mwinyi Dkt. Hussein kwa kazi nzuri anayofanya hongera sana *CDF,* Jenerali Venance Mabeyo hongera sana, hongera sana Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Jenerali Yacoub Mohamed hongera sana, hongera sana Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Charles Mbuge, Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Faraji Mnyepe, watendaji wengine wote katika Jeshi na wanajeshi wote kwa ujumla wenu tunawatakia kila la kheri katika utendaji kazi wenu, muendelee zaidi na zaidi kuboresha kazi zenu na imani ya wananchi wa Tanzania kwa kweli ni kubwa kwa Jeshi na mmeona hata mchango wa Waheshimiwa Wabunge kwa sehemu kubwa imekuwa ni wa kulijenga Jeshi letu na kuonesha imani kubwa waliyonayo kwa Jeshi letu. *(Makofi)*

Basi na mimi ni Mbunge wa Kongwa, nikukumbeshe tu *CDF* kuna watu wanapiga piga maeneo yao sijui yamefanyaje, sijui nini Jeshi kule Kongwa eneo mnalo na hamdaiwi fidia. Kwa hiyo, tuendelee na programu ya kujenga Kambi ya Jeshi Kongwa, pia Mkuu wa JKT eneo mnalo pia na hamdaiwi fidia yoyote, mlikwishalipa pia ule mpango wetu wa kujenga Chuo cha *VETA* cha JKT kule Kongwa tunaomba uendelee, kule mnapokelewa kwa mikoni miwili yaani kambi yoyote inayolalamikiwa huko nyie hamishieni Kongwa tu wala hamna shida hamtapata taabu yoyote ya kulalamimiwa chochote na Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi atapima haraka ardhi hiyo na kuwa ardhi ya Jeshi, sisi tulikaa na wapigania huru nchi zote Kusini mwa Afrika huko. Kwa hiyo, sisi tunajua namna ya kukaa na wanajeshi hatuna shida.*(Makofi)*

Safari moja nilikuwa na mkutano wa hadhara kama Mbunge pale sasa tukawa tunazungumzia ajenda hii ya wanajeshi kurudi na ajenda hii ikawa inashabikiwa sana na akinamama hasa wasichana/mabinti wanajeshi warudi. Lakini wanaume wakawa mmh, mmh, nikauliza kuna nini tena hapa, lakini bahati nzuri akinamama walishinda kwenye hoja hiyo. Kwa hiyo, tunaomba wananchi warudi Kongwa kwa

nguvu kubwa kabisa kwa sababu wana neema nyingi wanajeshi, tunawapenda sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo nina matangazo muhimu ambayo ningependa kuyatoa kabla ya kumaliza shughuli zetu hapa. La kwanza toka Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuteuliwa kuwa Waziri nilikuwa sijakaa hapa mezani, nitumie nafasi hii kukupongeza sana, hongera sana kwa iman ambayo Mheshimiwa Rais amekupa tuko pamoja na tutakuoa kila aina ya ushirikiano hapa Bungeni. *(Makofi)*

Lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge ratiba ya Bunge ambayo tumeitoa inayomalizika tarehe 28, 29 Mei hapo bado ni *tentative*. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi sana, tunavyokwenda kama mtakavyoona ratiba hii karibu ni ya tano toka tumeanza Mkutano huu. Ni kwa sababu kuna mambo mengi sana ya kurekebisha, kuweka sawa, kwa hiyo kunaweza kukawa na tofauti kidogo huko mbele tunakoenda, lakini inatoa mwanga wa jinsi ya kufanya kazi kama tunavyoenda.

Kwa hiyo, kesho tunaye hapa Mheshimiwa Waziri Kigwangalla na baadae atafuata Nishati na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi naye anajiandaa andaa huko, watafuatia hivi karibuni sana. *(Makofi)*

Lingine ningependa kusema kwamba nimepokea au tumepokea barua ya Bwana John Mnyika, Katibu Mkuu wa CHADEMA akimuandikia Katibu wa Bunge. Barua hii anasema kwamba tusimtambue Mheshimiwa Cecil Mwambe kama Mbunge na asipate stahiki zozote, lakini barua yenyewe jinsi alivyoiandika ni fupi niwasomee tu.

Anasema; Bwana Cecil Mwambe alikuwa Mbunge wa Jimbo la Ndanda aliyekuwa amedhaminiwa na CHADEMA, hata hivyo mwezi Februari mwaka huu, alitangaza kupitia vyombo vya habari kwamba amehama chama hicho. Hivyo basi kwa mujibu wa Ibara ya 7(1)(f) ya Katiba

ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekoma kuwa Mbunge na ameacha kiti chake katika Bunge. Kwa hiyo, Bunge lisiendelee kumpatia stahiki zozote na kadhalika.

Sasa namshangaa Mheshimiwa Mnyika kwa sababu hayo maneno anayosema alipaswa aambatanishe na barua ya Mheshimiwa Mwambe inayothibisha haya anayoyasema, hakuambatanisha. *(Makofi)*

Pili, mimi sina barua ya Mwambe ya kusema kwamba kaacha Ubunge kwa hiyari yake mwenyewe, na kama ni chama hiki kimechukua hatua sina viambatanisho vinavyoonesha vikao halali vilivyofanya maamuzi hayo. Kwa hiyo, hii barua haina maana, haina mantiki na kwa nafasi hii nichukue nafasi hii kuwaambia Wabunge wote *including* Wabunge wa CHADEMA na wengine wanaotishwa tishwa huko, msibabaike msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mnae Spika imara, atawalinda mwanzo, mwisho. Habari ya ukandamizaji na ubabaishaji hauna nafasi hapa. Fanyeni kazi zenu kwa kujiamini, mmeaminiwa na wananchi fanyeni kazi zenu, wala msiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Pia nimepata nakala ya hukumu, Spika na Mwanasheria wa Serikali walikuwa wameshtakiwa na Bwana Tundu Lissu kwenye shauri la maombi kwa Mahakama Kuu Namba 42 la mwaka 2019. Nimearifiwa kwamba Mahakama imetupilia mbali maombi hayo ya Bwana Tundu Lissu, tena kwa gharama, kwa hiyo huko aliko ajiandae kulipa maneno huku Tanzania. *(Makofi)*

Pia tumeona kupitia mitandao na vyombo vingine vya habari maelezo au Tangazo la CHADEMA kutoka kwa Mwenyekiti wake Bwana Freeman Mbowe akiwa na nafasi ya Kiongozi wa Upinzani akiwaelekeza Wabunge wa chama hicho humu Bungeni wasihudhurie Vikao vya Bunge kwa muda wa wiki mbili. Nimeshangazwa sana na tangazo lile na nimesikitishwa kweli kweli. Kwa sababu hana mamlaka hayo ya kuitisha utoro na mgomo kwa Wabunge kwa wiki mbili. *(Makofi)*

Anajaribu kuwa kama *prefect* wa shule ya sekondari hivi, yaani hayo mambo nayakumbuka enzi hizo tunagoma sijui chakula kimefanyaje, yaani bado anaendesha mambo kisekondari kabisa. Huwezi kufanya mgomo wa namna hiyo kirahisi rahisi tu, haiwezekani. Taarifa nilizonazo japo wameambiana wakae Dodoma hapa, wako wanazurura nchi nzima. Wanazurura zurura tu huko, wanazagaa zagaa huko. *(Makofi)*

Nitamke rasmi kabisa kwamba barua hiyo si halali kwa maana ya sisi Bunge hapa, kwa hiyo, hatuitambui, haina nafasi, Wabunge hao popote pale walipo warudi Bungeni haraka sana kuendelea na kazi zao. *(Makofi)*

Sasa wale watakaoendelea na huo mgomo wajue, baada ya hizo wiki mbili zao kuisha hawatapokelewa hapa Bungeni, isipokuwa kama kila mmoja wao atakuwa amefanya vipimo vya *Covid-19* na kupata *clearance* kwamba hawana matatizo. Kwa sababu sisi tupo hapa, wao wanazurura nchi nzima, hatuwezi kujua nani anarudi salama, kwa hiyo, itabidi wapate vipimo kwanza kabla hawajakanyaga geti la Bunge kuingia hapa na haya ndio maelekezo. *(Makofi)*

La pili, Wabunge hawa ambao ni watoro, huko mikoani waliko na wananchi wawatambue hivyo, walipokuwa wanaondoka walikuwa wamekwishalipwa fedha za *perdiem* kwa wiki mbili kuanzia tarehe 1 Mei hadi tarehe 17 Mei, 2020. Jumla ya shilingi 110,160,000 kundi hilo kwa ujumla wake.

Kwa hiyo, ukiondoa hawa ambao wameamua kuendelea na vikao hivi ambavyo hatutawadai, lakini nawaagiza Wabunge hawa kuanzia Freeman Mbowe mwenyewe kurudisha shilingi 2,040,000 aliyolipwa, na wenzake wote hawa kurudisha shilingi 2,040,000 ambayo kila mmoja wao amelipwa kwa vile huu ni utoro wa hiyari na hizi ni fedha za wananchi, kwa maneno rahisi ni wizi na ni mfano mbaya sana kwa viongozi, kwamba unalipwa fedha za wananchi maskini hawa, uwafanyie kazi yao. Wewe

unaondoka, unatoroka, unajiwekea migomo ambayo haina kichwa na miguu, lakini fedha ile ipo mfukoni, ndio unazurulia huko nchini. *(Makofi)*

Kwa hiyo irudishwe hii fedha shilingi 2,040,000 kwa kila mmoja wao lakini kuna wengine waliolipwa milioni tatu, tatu. Mheshimwia Catherine Ruge, shilingi milioni tatu rudisha, Mheshimiwa Devotha Minja shilingi milioni tatu, shilingi milioni tatu Mheshimiwa Joyce Mukya, shilingi milioni tatu Mheshimiwa Rhoda Kunchela, shilingi milioni tatu Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, shilingi milioni tatu Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru. Wengine wote waliobaki shilingi 2,040,000.

Maagizo yangu ni nini, hawa kila mmoja wao arudishe hizi fedha, atakaefika getini anapohesabu mgomo wake umeisha bila kuwa amerudisha fedha hizi hataingia katika eneo hili na hatutaweza kumpokea na baada ya tarehe hizo wiki mbili walizojiwekea hizo, kama watakuwa hawajarudisha fedha hizi basi nitapeleka orodha hii katika vyombo vya ulinzi na usalama. Litakuwa sasa ni jambo ambalo sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatusaidia kuona linakwenda kwenda vipi. *(Makofi)*

Lakini mimi kwa hatua kama Spika hawa warudishe kwanza fedha hizi ambazo ni wizi, haraka sana katika akaunti ya Bunge, vingingevyo hatutawapokea hapa. Kwa hiyo, masharti hayo mawili watakuja kwanza wawe wamerudisha hizi fedha, lakini la pili wawe na *clearance* ya *Covid-19* ndio wakanyage kwenye geti hili la Bunge na hatua nyingine zitafuatia. Kwa sababu wao si wababe bwana na wako mwisho mwisho hapa, wajue wanacheza na moto. Yanayofuata yanafurahisha zaidi kwa kundi hili. *(Makofi/ Kicheko)*

Basi kwa vile shughuli za leo zimekamilika naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 11.30 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi Tarehe 7 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*